YA MTAKATIFU TIHONI ASKOFU YA ZANTONSKI YA INCHI RUSIA

# MWENDO KWA MBINGU

CENTRE DE LA MISSION ORTHODOKSE
KOLWEZI KONGO
1998

# YALIYOMO

SEHEMU YA KWANZA
MAPENDO YA MUNGU
Mapendo mbele ya Mungu
Ma alama ya mapendo mbele ya Mungu
Kumbuka mapendo ya Mungu
Heshima kwa Mungu
Madiko ya Mungu
Sheria ya Mungu ni ndani ya moyo yetu

SEHEMU YA MBILI
NJIA YA WOKOVU
Habari Njema (Evangelio) ya wokovu
Ubatizo Takatifu
Kukataa na Malako
Zambi kisha Ubatizo
Njia ya kurudia
Mwokozi
«Taifa takatifu»

SEHEMU YA TATU
MASHINDANO WA ROHO
Mbukomvi katikati mwili na roho
Uhukumu ya maungo wetu
Maangalio ya ndani
Zambi
Maneno ya zambi
Sindano kupingana ya zambi
Majivuno
Zambi ya ulimi
Toka ya uzima utamu
Mbali ya ulevi
Chuki
Mapendo
Saidio ya Mungu
Makumbusho ya Mateso takatifu ya Bwana Yesu
Ufwasi ya uzima ya Kristu

SEHEMU YA INE
NJIA YA KUPASWA
Ma kazi ya kupaswa wakubwa
Ma kazi ya kupaswa watumishi
Ma kazi kupaswa ya wachungaji ya roho
Ma kazi ya kupaswa ya watoto ya roho
Ma kazi ya kupaswa katikati ya mume na muke
Ma kazi ya kupaswa ya wazazi
Ma kazi ya kupaswa ya watoto

Ma kazi ya kupaswa ya Watajiri
Ma kazi kupaswa ya wenye biashara
Ma kazi ya kupaswa wayengaji na watumishi yao
Kazi ya kupaswa ya hurumia
Kazi ya kupaswa ukamilifu

## SEHEMU YA TANO
## KU UZIMA WA MILELE

Mukuangalia mbingu
Mauti
Matisho ya Mungu
Uhukumu wa matata
Uzima wa milele
«Lakini kitu kimoja kinahitajiwa»

# SEHEMU YA KWANZA
# MAPENDO YA MUNGU

## Mapendo mbele ya Mungu

Wa Kristiani wapenzi wangu, sisi tunazombelea kusema: «Ole! Namna gani iko namna mtu moja hasipende Mungu? Kama usipende Mungu, utapenda nani? Ni kweli. Mungu ni Wema mwenye juu, musiyeumba, musiyemwanzo, musiye mwisho na musiye haribifu, Sawa vile jua inangaza daima, sawa vile moto inaleta kivukutu daima, vile na Mungu, mwenye ni Mwema daima, anaonyesha daima mapendo yake, kwa hivi inatwambia Agano Jipya ya kama «Ni mumoja aliye mwema» (Mat. 19, 17). Mikono yake yenye mwenyezi walituumba. Walituumba, ewe watu wapenzi, hapana sawa viumba wengine, bila akili na mahasa. Mikono yake walituumba na uwazo Wake takatifu. «Tufanya mutu kwa mufano wetu. . . »(Mwanzo 1, 26), alisema Mungu. Lakini kwa viumbe wengine «maana ameamuru, nayo yaliumbwa» (Zaburi 148, 5». Lakini juu ya kuumba mutu hasikufanyika hivi. namna gani aliumba mutu? «Tufanya mutu kwa mufano wetu. .» Mapendo ya Mungu ni ajabu. Sifa kwa mutu ni juu pia! Mutu aliumbwa katika mufano ya Mungu. Hakuna kiumbe ingine kustahiliwa hii sifa. Paka mutu alisifu Mungu kumuumba katika mufano Wake. Basi, mutu ni kiumbe muzuri na mupendwa kuliko ya wengine. Kila mutu eko na juu yake mufano ya Mungu kama alama ya ufalme. Mungu, mwenye ni mfalme ya mbingu ni mustahili ya kila sifa. Vile na mutu, mufano wake. Hii neema na sifa alitupatia Mungu, wakati alituumba, ewe wa Kristiani wapenzi wangu! Sasa namna gani sisi tusimupenda?

Tulianguka toka Paradizo chini kabisa na hakuna namna kuria kwa hii kosa yetu. «Lakini mutu hadumu katika heshima; yeye ni kama nyama wanaopotea. Hii njia wao ni upumbafu; hata hivi watu walio nyuma yao wanakubali masemo yao» (Zaburi 49, 12-13). Lakini Mungu mpendwa-wanadamu hatukuache kwa hii hali ya uzima yetu. Alipata namna ya ajabu ya wokovu wetu. Alituma Mwana wake wa pekee, juu ya kutupata, kutuokoa na kutuletea karibu Yake mara ingine. «Kwa maana Mungu alivyopenda ulimwengu, hata kutoa Mwana wake wa pekee, ili kila mutu akimwamini asipotee, lakini apate uzima wa milele» (Yoane 3, 16). Namna gani, basi, Huyu Mungu aliyetupenda hivi mingi, sisi tutakataa kumupenda? Mungu ni Mpenda-wanadamu, sawa vile watu wote wanamuita. Lakini na mtu inapaswa kuwa mpendwa-Mungu. Malipo ya mapendo ni mara ingine paka mapendo kwa mtu mwingine.

Mungu ni Mwema na Musubuko wetu. Anasubuka kwa sisi. Anatupatia chakula, mavazi, na nyumba pahali tunakaa. Jua na mwezi na ma nyota yenye wanatuangaza ni Yake. Tunapata kivukutu na moto yake na tunatayarisha chakula na moto yake. Na maji yake tunakunywa na tunanawa. Ma nyama Yake wanatusaidia. Pepo Yake inatukamata kwa hii uzima. Na ma sauti wadogo uzima yetu ni kwa Mikono na mapendo na wema yake. Bila wema wake hatuweze kuishi. Basi, namna gani iko namna kuishi bila kupenda Huyu Mungu na Mwema wetu? Ngapi kuliko tunapaswa kupenda Mungu Mufazili wetu, mingi kabisa ya maungo na vitu vyetu vyote! Kuumba ya ulimwengu na mtu ni viumbe ya Mungu. «Inchi na kujaa kwake ni mali ya Bwana, dunia, nao wanaokaa ndani yake» (Zaburi 24, 1).

Mungu ni Baba wetu. Wakati tunaomba Kwake tunamsema: « Baba yetu uliye mbinguni». Namna gani iko namna kukataa kumpenda Mungu-Baba? Watoto wazuri wanapenda baba wao bila mawazo mbaya. Basi, kama na sisi tunataka kuwa watoto wa kweli ya Mungu na kumuita Baba, tunapaswa kumpenda. Ni kweli, basi, hii ulizo: « Namna gani usitapende Mungu»?

Lakini, sawa vile kila fazila, hivi na mapendo inapaswa aishi ndani ya roho. Kama hakuna ndani ya roho, hakuna na kwa matendo yetu. Kwani Mungu hasikuseme paka kwa masikio yetu, «penda, nyenyekevu, wema, omba», lakini alituwambia hivi juu ya roho yetu. Basi, sisi tunapaswa kuishi na mapendo, unyenyekevu, wema na sala na ma fazila ingine yote ndani ya roho yetu. Na,

kama ni ndani ya roho yetu, iko namna kuonekana na inje ya uzima yetu, sawa vile inatoka inje kivukutu toka moto na arufu toka manukato.

Vile na Mt. Nabii na Mfalme Daudi mapendo yake alionyesha mbele ya Mungu na maombi na mwimbo: «Bwana ni mwamba wangu na boma langu, na mwokozi wangu; Mungu wangu, mwamba wangu, ninayemukimbilia; Ngabo yangu, na pembe ya wokovu wangu na ngome yangu. Nitaita Bwana, anayestahili kusifiwa; hivi nitaponyeshwa kwa adui zangu» (Zaburi 18, 2-3). Mapendo inajifichama ndani ya roho, lakini hasiweze kujifichama pale daima. Inaonekana na ma alama yake inje kwa uzima yake.

## Ma alama ya mapendo mbele ya Mungu

Lakini sasa twende kuona ma nani ni ma alama ya mapendo mbele ya Mungu juu ya tusikona fundisho ya wongo kwa hii mapendo. Kwani mutu anajilanda sana kabisa kwa hii mambo ya mapendo, ma alama ya mapendo ya kweli ni hii:

1.

Mwana mumoja anatufundisa na anasema hivi: «Aliye na amri zangu, na kuzitii, yeye ndiye mwenye kunipenda» ( Yoane 14, 21). Huyu mtu anayependa kweli Mungu na anakombana kuishi mbali ya zambi na kutii ma sauti Yake, huyu mtu anampenda Mungu. Basi, iko namna kusikia watu wote ya kama wale Wakristiani awaonyeshe mafa kwa maamri ya Kristu, awakuwa na mapendo kwa Mungu. Katikati ya wao weko wenye watu mbaya, wenye kulewa, wenye wevi, wanyanganyi, wasiyohaki, wenye mwovu, wafumu, wenye kulanda na wadanganyifu. Tena ni na walozi, wenye wanawaita ma nyumba yao na kusema na sauti moja wote wazulumu. Wao watu, sawa vile hawapende sheria ya Mungu, vile hawapende na Huyu mumoja. Wao watu wanapenda maungo wao na zambi wao na hapana Mungu na Sheria Yake takatifu.

2.

Alama ya kuonekana kwa mapendo yetu ya Mungu ni na furaha ya roho yetu. Kwani ni kweli kusikia furaha kwa kila kintu tunaipenda. Vile na mapendo yetu kwa Mungu, bila furaha hakuna namna kuisikia. Mara ngapi mtu moja anasikia ndani ya roho yake mapendo utamu ya Mungu, hata mara mingi anajaza kwa furaha roho yake. Sawa vile sari inatupatia furaha, kama tunaikula, vile na mapendo ya Mungu inatufurahi roho yetu, kwani tunapima na tunaona ya kama Bwana ni Mwema (Zaburi 34, 9). Hii furaha kwa Mungu inaonekana ma fasi mengi ndani ya Madiko Takatifu na kabisa ma Zaburi ya Nabii Daudi. Hii furaha katika roho na wa mbingu ni kupima furaha utamu ya uzima ya milele.

3.

Huyu mtu anayependa kweli Mungu, anatembea paka kwa Huyu na anazarau dunia na vitu vyote vyake. Sifa, utukufu, feza na mashangilio yote ya dunia wanawatakia paka watu ya hii wakati, lakini mtu moja ya Mungu anaangalia hii yote vitu sawa kintu kimoja ya bure. Mtu ya Mungu anapenda paka ndani ya Mungu kupata utukufu, utajiri na furaha. Kwa huyu mtu Mungu ni zahabu mkubwa na mbele Yake hakuna kintu kuliko stahili. Huyu mtu hasipende hata kintu kimoja ya hii dunia, hata mbingu, hata inchi, paka anapenda kuikaa karibu ya Mungu. Hii mapendo wanatuonyesha na ma sauti ya Zaburi moja: «Nina nani mbinguni ila wewe? wala hakuna duniani ninayemutaka kuliko wewe. Mwili wangu na moyo wangu inapunguka: lakini Mungu ni nguvu ya moyo wangu na sehemu yangu milele» (Zab. 74, 25-26). Mutu anatumia chakula, na maji na mavazi paka ya ma lazima yake na hapana juu ya furaha wa zambi.

Huyu mtu anayependa dunia hasipende Mungu katika ushuhuda ya Mtume Yoane: «Mutu akipenda dunia, mapendo ya Baba si ndani yake» (Barua ya kwanza ya Mt. Yoane, 2, 15). Hawa watu ni wenye wanataka kuishi maisha yao na majivuno, na ma vitu wengi, na ma nyumba vizuri, wanatembea na ma motokaa wao makubwa, wanavaa kabisa nzuri na wanataka kuwatukuza na kuwasifu watu wengine. Hawa watu wanapenda uzima ya mwili, utukufu ya bure na uzima ya majivuno, nikusema kila kintu inayezarau na inaihukumu Mungu.

4.

Huyu mtu anayependa kweli Mungu, anamukumbuka daima mu akili yake; anakumbuka mapendo na mafazili Yake. Hii mambo tunaiona na kwa mapendo katikati ya watu. Yule mtu tunampenda tunamkumbuka kila siku. Vile inafanyika na kwa mapendo yetu mbele ya Mungu. Huyu anayempenda, anamkumbuka daima, anamuwaza, anapumzika karibu yake na anamuangalia na ajabu. « kwa maana pahali hazina yako iko, pahali moyo wako utakapokuwa vilevile» (Matayo 6, 21). Kwake zahabu mupendwa na mweshifiwa ni Mungu. Kwa hivi na roho yake iko daima karibu ya Bwana. Kwa hivi anakumbuka kila siku Jina takatifu ya Mungu. Na kama roho inajaza kwa mapendo ya Mungu, inaonyesha na inje hii ma alama ya mapendo yake kwa Mungu. . Ninyi wote wanasahabu Mungu, hawamupende. Usahabu ni alama ya kama mapendo hakuna. Huyu anayependa hasiweze kusahabu Mupendwa wake.

5.

Kama watu wa wili wanapendwa, wanataka kuwa daima pamoja. Ni kweli ya kama wa Kristiani wengi wanapenda kuwa pamoja na Kristu kwa utukufu Wake, lakini hawapende kuwa pamoja na Ye na kwa Msalaba na mateso Yake. Wanaomba Kwake kuriti Ufalme Wake, lakini hawapende kuvumilia pamoja na Ye. Vile wanaonyesha ya kama roho yao hasitembee ya kunioloka na hawapende kweli Kristu. Na, kama tunataka kusema na sauti kweli, hawa watu wanapenda kuliko maugo wao na hapana Kristu. Kwa hivi Bwana anasema: «Naye asiyechukua musalaba wake na kunifuata hanistahili» (Matayo 10, 38). Murafiki yetu ya kweli anaonekana kwa sikitiko wetu. Vile na huyu mtu anayependa kweli Kristu; kwa hii dunia anatembea pamoja na Kristu, roho yake inaunganishwa na Yeye, anavumilia mateso na msalaba Yake pamoja bila kuria. Yeye atakuwa kwa milele karibu ya Kristu. Huyu mtu anasema toka ndani ya moyo yake kwa Kristu: «lakini ni vizuri kwangu kukaribia Mungu» (Zaburi 73, 28).

6.

Uonyesho ingine ya mapendo yetu kwa Mungu ni na mapendo yetu mbele ya mukaribifu wetu. Huyu mtu anayependa kweli Mungu, huyu anapenda na kila ndugu wake. Chemchem ya mapendo mbele ya mukaribifu ni mapendo kwa Mungu. Na kupindua, mapendo mbele ya Mungu inaonekana toka mapendo yetu mbele ya wa ndugu wetu. Ni kweli, basi, ya kama huyu asiyependa mukaribifu yake, asipende na Mungu, sawa vile anatufundisha na Mtume: «Kama mutu akisema: Ninapenda Mungu, naye anachukia ndugu yake, ni muwongo; kwa maana asiyependa ndugu yake aliyemwona, hawezi kupenda Mungu asiyemwona. Na amri hii tumepewa naye; mwenye kupenda Mungu imemupasa kupenda ndugu yake vile» (Barua ya Mt. Yoane 4, 20-21).

Hii ni ma alama ya mapendo yetu mbele ya Mungu.

Wa Kristiani wapenzi wangu, tunapaswa kutubu na kuzarau mashangilio ya hii dunia. Tunapaswa kusafisha moyo wetu na toba na machozi juu ya kuikaa ndani yetu mapendo ya Mungu. «Mungu ni mapendo, naye anayekaa katika mapendo, anakaa ndani ya Mungu, na Mungu anakaa ndani yake» ( Barua ya kwanza ya Mt. Yoane 4, 16).

Mungu ni Wema kuliko juu pia, na toka Huyu inatoka yoyote matendo mazuri na uzima ya milele.

Bila Mungu kila furaha ni wenye mafigo na umasikini, uzima ni lufu na furaha na utamu ni uchungu. Lakini pamoja na Mungu kila sikitiko ni heri, umaskini ni utajiri, usiyeutukufu ni utukufu, usiyesifa ni sifa, mateso inajaza na utulivu. Bila Mungu hakuna namna kupata pumziko ukweli, amani na utulivu.

Kwa hivi endelea kumupenda Mungu kama Wema moja ukubwa kabisa na kama Uzima moja mwenye milele. Umupenda Mungu yulu ya kila kiumbe, kupita ya baba na ya mama yako, kupita ya bibi na watoto wako. Tena umupenda yulu ya maungo yako. Paka Kwake umupatia roho yako na kuliko mingi ya kila kintu ingine Huyu utamupenda, utamutakia na utamufata. Kwani Mungu ni furaha yako wa milele na wema wako wa milele. . Bila Huyu hata kwa hii uzima, hata kwa uzima ya milele hakuna uzima mwenye heri.

Kila kiumbe ya Mungu ni ukweli, lakini Muumba yao ni kuliko Muzuri. Basi, penda na tafuta Huyu, mwenye ni umoja Wema, usiyemwanzo, wa milele, ma fasi yote ya dunia na usiyeharibifu na toka Huyu waliumbwa yoyote viumbe vyote.

## Kumbuka mapendo ya Mungu

Ma siku yote kwa matendo yako yote kumbuka na mapendo Bwana na Mungu wako na mapendo Yake kwa sisi yote. Ninyi wote unaona kwa mbingu na inchi, mu fasi ya nyumba yako, wanakuonyesha ya kukumbuka Bwana yako na mapendo Yake, inayefunga ndani yake na sisi.

Kila kiumbe ya Mungu inatuonyesha mapendo yake kwa sisi. Mukuona, basi, na mukufurahi viumbe vyake, sema ya ndani yako:

Hii ni tendo ya Mikono ya Bwana na Mungu wangu na iliumbwa kwa ajili ya mapendo yake kwa mimi.

Hawa ma nyota makubwa ya mbingu kwa mufano jua, mwezi na wengine ma nyota ni viumbe ya Bwana wangu juu ya kuangaza ulimwengu na mimi.

Hii inchi, pahali na mimi ninaishi, inapatia matunda yake kwa mimi na ma nyama yangu; hii pamoja na kila kintu ni juu yake ni kiumba ya Bwana wangu.

Hii maji inanifurahi mimi na ma nyama yangu ni wema ya Bwana wangu.

Hawa ma nyama wenye wananisaidia ni viumba ya Bwana wangu na alinipatia kwa saidio yangu.

Hii nyumba, pahali ninaikaa, ni zawadi ya Mungu na alinipatia kwa pumziko yango.

Hii chakula ile ninaikula ni wema ya Mungu na ananipatia juu ya utulivu na nguvu ya mwili yangu.

Hii nguo ninayevaa aliniipatia Bwana na Mungu wangu juu ya kufunika mwili yangu.

Hii Uso ya Bwana Yesu ni Uso ya Mwokozi wangu, aliyeshuka mu dunia umaskini, kwa ajili ya saidio yangu kuniokoa, kwani nilikuwa kondoo mupotevu. Yeye alitesa na alikufa kwa mimi na vile aliniuza toka zambi, toka shetani, toka lufu, na Hadeze. Ninasujudu upendwa-wanadamu wake!

Hii Uso ya Mzazi-Mungu ni Uso ya Binti Mtakatifu, aliyezala bila bwana Bwana wangu na Mungu Yesu Kristu. «Umebarikiwa wewe katika wanawake, na uzao wa tumbo lako umebarikiwa. » (Luka 1, 42). «Heri tumbo lililokuzaa, na maziwa uliyonyonya! » (Luka, 11, 27).

Hii Uso ya Mtakatifu Yoane Mubatizaji ni uso ya Nabii mkubwa, aliyemutuma Mungu mbele ya Uso ya Mwokozi wangu. Huyu alitangaza kwa watu ufikisho Yake na alimuonyesha hivi: «Tazama Mwana-kondoo wa Mungu anayechukua zambi ya ulimwengu. » (Yoane 1, 29), na ku mwisho alistahiliwa kumubatiza ndani ya maji ya mtoni Yorodani.

Hii uso ya Mtume ni uso ya mwanafunji ya Mwokozi wangu, aliyemuona mumoja, alitembea na Yeye, alimusikia kuhubiri Wake, alimuona kutenda miujiza na kisha kuteswa juu ya wokovu ya watu wote, alimuona kufufua toka wafu na kupanda mbinguni.

Hii uso ya Mushahidi ni uso ya yule mkubwa, aliyekombana mpaka kumwanga damu yake juu ya kuchunga sifa ya Mwokozi wangu Yesu Kristu na kwa ajili ya Jina Yake alitoa na uzima yake. Vile na matoleo ya damu yake alisingi imani yetu inaye iko paka hii wa pekee ya kweli.

Hii sauti takatifu ninaisikia ni Madiko Takatifu, ni sauti ya Mungu, ni ma sauti toka kinywa yake. Midomo Yake waliisema; na sasa Mungu ananiambia hivi: «Sheria ya kinywa chako ni njema kwangu kuliko elfu za zahabu na feza» (Zaburi 119, 72).

-Ee Bwana, unipe masikio, juu ya kusikia sauti yako takatifu!

Huyu Nyumba takatifu, kanisa, pahali na mimi niko, ni Hekalu ya Mungu na ndani inajitoa uabudu na utukufu kwa Mungu Bwana wangu. Hii wimbo na ma sauti na maombi wanapanda kwa Jina Yake takatifu.

Huyu mtu mtakatifu, askofu ao mpadri ni karibu kabisa musaidizi ya Mungu wangu na yeye anamutuma maombi kwa mimi mwenye zambi na kwa dunia nzima.

Huyu mtu anayekuhubiri Fundisho takatifu ni mufwasi ya Mungu wangu na anaonyesha kwa mimi na kwa wa ndugu wengine njia ya wokovu.

Huyu mtu, mukaribifu yangu, kila mtu, ni ndugu wangu. Ni kiumbe kuliko mupendwa ya viumbe wengine na aliumbwa sawa na mimi kwa mufano ya Mungu. Na huyu mutu alianguka, alikosa, lakini aliuzwa, sawa vile na mimi- na Damu ya Mwana ya Mungu, Mwokozi wangu na aliitwa kwa uzima ya milele. Inapaswa kumupenda, kwani ni kiumbe mupendwa kabisa ya Mungu wangu. Inapaswa kumupenda kama maungo wangu. Aipaswe kumufanysia kintu kimoja ile misikupende kufanyika kwa maungo wangu, kwani na Mungu wangu vile aliniamuru.

Ku mwisho, ee Mukristu, kila jabo na kila kintu iko namna na inapaswa kusimamisha ndani yako makumbusho na mapendo kwa Bwana wako na kuonyesha mara moja na mapendo Yake kwako. Kwani, tena na hii malipizo ao kipimo inayetutuma mara mingi inatoka kwa ajili ya mapendo Yake kwa sisi, sawa vile na Madiko Takatifu inatuonyesha: «Maana mutu Bwana anayemupenda anamwonya» (Mezali 3, 12).

Basi, kumbuka daima kwa kila wakati na kwa kila mambo Jina ya Bwana na Mungu wako. Sopoka usisahabu Mufazili na Musaidizi wako, wakati unabeba ma bintu yake, kwa sababu usahabu mbele ya Mufazili ni alama ya kama hasisikie kusema shukrani Kwake.

Usisahabu tena ya kama Ufazili ukubwa kabisa iliyetupatia Kristu Mwana wa pekee ni ya kama alikuja mu inchi yetu na katika Damu na Mateso Yake alitutosha toka mikono ya shetani, Hadeze na lufu. Vile na hii Tendo yake wa milele ilifunguliwa kwa Kizazi ya wanadamu, chemchem ya rehema Takatifu.

Basi, tunapaswa na sisi ma siku yote kuangalia na imani hii Tendo ukubwa ya Mungu na kuikumbuka daima. Mungu, aliyetupenda sana sisi wenye wasiyostahili, inapaswa kumushukuru toka ndani kabisa ya roho yetu, kumusujudu, kumuimbia na kumutukuza Jina yake takatifu na roho na midomo yetu: «Atukuzwe Bwana, Mungu wa Israeli; kwani amekuja kwa watu wake, na kuwakomboa. Ametunyanyulia pembe ya wokovu, katika nyumba ya mutumihsi wake Daudi; » (Luka 1, 68-69).

## Heshima kwa Mungu

Mungu inapaswa kumusifu hapana na vitu vya hii dunia na ma onyesho ya bure, lakini na moyo safi, na boka, na mapendo na utii na shukrani, na sala na imani. Kwa sababu Mungu ni Roho bila materiale ya hii dunia na kwa hii maneno hakuna namna ingine kumusifu paka «katika roho na ukweli».

Ita na sema Jina ya Mungu na kila sifa, boka na heshima. Utafanya hivi kwa kila fasi na wakati ni lazima. Kwani Jina ya Mungu ni takatifu na wale wanaisema bila heshima, wanafanya zambi. Basi, sifa na heshima jina ya Mungu, sawa vile unaheshima Huyu mumoja.

Kama unasema na heshima jina ya mfalme ya hii inchi- na vile iko lazima- ngapi kuliko mingi heshima na sifa unapaswa kusema Jina ya Mungu, mwenye ni Mfalme ya ma mbingu, na Jina Yake upendwa na utamu kabisa inajiimbia toka wa malaika na ma nafsi ya Watakatifu?

Tunatumia Jina ya Mungu kwa maombi, kwa Doksologia, kwa Mashukuru, kwa Masifu na wimbo ya roho na mazungumuzo na masuburio ya wa Kristiani, nikusema wakati wanasuburia juu ya Sheria Yake, Evangelio na Sauti yake, juu ya Ufikisho yake mu dunia, juu ya uzima Yake kwa hii inchi, Mateso, Musalaba Yake, lufu, Ufufuo Yake, Uhukumu na Gehena na uzima ya milele na ingine.

Bila kuwa lazima mnene, usitumie Jina ya Mungu. Kama ni lazima utaisema Jina yake na pasopo na heshima mingi. Kama unasema ma sauti ya macheko na wongo ya kucheza usiseme Jina ya Mungu, kwani Uhaki wake atakuhukumu, kwani Mungu ni moto ya kulungua.

Ni kintu mbaya kama Mukristu moja anatumia Jina ya Mungu bila lazima kwa mazungumuzo yake ya bure mukusema: Ni Mushuuda Mungu, kwa jina ya Kristu, anaona Mungu na ingine ma sauti. Ni kweli ya kama hivi tunazarau Jina ya Mungu na tunapotea baraka Yake mu uzima yetu.

Wewe, Mukristu wangu, chunga nzuri roho na uzima yako toka hii zambi. Kama ni lazima kukikiri sauti moja ao neno moja ukweli, sopoka kutenda hii neno ya Kristu: « Maneno yenu yawe, ndiyo, ndiyo; siyo siyo, kwa maana neno zaidi ya haya linatoka kwa yule mwovu» (Matayo 5, 37).

*****

Boka ya Mungu inazala toka uwazo ya kama Mungu ni ma fasi yote ya dunia na anafamia vitu vyote. Uzima yake mzima inajaza ulimwengu nzima. Kwa kila fasi sisi tuko Mungu ni pamoja na sisi. Kila kintu na kazi tunafanya, tunasema ao tunawaza chini ya ma macho Yake. Tena na matendo yetu ile tunawaza kufanya ku mbele Mungu anajua kuliko ya sisi.

Basi, sopoka, ewe Mukristu, na saidio ya Mungu itazaliwa ndani yako boka yake. Na, kama utaipata hii boka, itakuchunga na itakutengeneza kila kosa na tendo yako. Itakuepuka kwa kila tendo kibaya na itakushauria kwa kila kazi kizuri. Vile kila siku utafanyika kupita Mukristu muzuri.

Kamata kila siku mbele ya ma macho ya moyo yako Mungu na vile utachunga daima boka yake ndani yako na utakumbuka Mwimbaji Daudi aliyesema: «Nimeweka Bwana mbele yangu daima; kwa sababu yeye ni kwa mukono wangu wa kuume, sitaondoshwa» ( Zaburi 16, 8).

## Madiko ya Mungu

Madiko Takatifu ni neno ya Mungu na ilifika kwa sisi toka ma nabii na Mitume. Inapaswa kuipenda sawa vile unapenda Mungu, kwani ni neno ya midomo yake. Kama unapenda Mungu, bila shaka utapenda na neno Yake.

Madiko Takatifu ni tangazo, barua ya Mungu kwa sisi wasiyostahili na iko zawadi Yake kuliko mnene mbele ya wengine. Alitupatia hii barua kwa wokovu wetu. Basi, kama unapenda huyu aliyekutuma hii barua, inapaswa kutuma na Barua inayekutuma.

Neno ya Mungu ilijitoa kwa mimi, kwa wewe, kwa kila mtu; na huyu anayetakia wokovu wake, anaweza na saidio ya hii neno kuipata.

Wakati mfalme ya hii dunia anakutuma barua, unaipokelea na shukrani, unaisoma na mafa na furaha mingi. Ngapi kuliko mingi sisi inapaswa kupenda hii barua ya Mfalme wa mbingu- neno ya Mungu- na ngapi mafa inapaswa kuisoma?

Neno Takatifu ilitupatia hapana kuwa paka ndani ya Kitabu, lakini ilitupatia juu ya kutayarisha wokovu yetu, kutakaswa, juu ya kufamia ma njia ya wokovu, juu ya kuponyesha ma zambi yetu na kutengeneza uzima yetu na vile tutakuwa wenye heri mbele ya Mungu.

Basi, kama unataka kuwa Mukristu wa kweli, inapaswa kukombana kuishi katika ma amri ya neno ya Mungu. Neno ya Mungu ni mbego ya mbingu. Basi, ni lazima kuzala ndani yetu matunda, nikusema mafazila takatifu na furaha ya mbingu. Kama tusifanye hivi Mungu atatuhukumu kwa ile siku ya uhukumu wake mbele ya Kiti yake takatifu.

Basi, kombana kuishi, katika fundisho ya Madiko Takatifu na vile utasaidia maungo wako kutembea ku mbele.

Ma Fumbo makubwa ya Utatu Mtakatifu, ya Komonyo Takatifu na wengine neno takatifu ya Mungu hasitufunua juu ya kuisikia na akili yetu. Kwa hivi usikombane kuisikia na akili yako, kwani ni hatari kuanguka kwa makila ya shetani, kisha usitaweze kutoka na utaharibifu.

Chunga ndani ya akili yako ya kama ni hatari mingi sana kufafanusha mtu moja hii Bintu takatifu ya Imani yetu. Kama unatafuta maana ya hii ma Fumbo Takatifu yetu, utapotesha akili yako na ma fazila ya Kristu. Paka amini kwa kila fundisho inatufundisha Madiko Takatifu na sawa vile inaamini na inatushauria Kanisa yetu Takatifu.

Usifate matendo ya watu wengine, wenye wanataka na akili yao kusikia maana ya ma Fumbo ya Kanisa yetu. Kama utafanya hivi pole-pole inapanda imani kwa maungo yako na

heshima na boka mbele ya Imani ya Mungu inashuka sana. Paka sopoka kwa hii neno Mungu anakuwambia.

## Sheria ya Mungu ni ndani ya moyo yetu

Wakati aliumba Mungu mtu aliweka ndani ya roho yake na moyo. Hii moyo inamusaidia kutembea na pasopo na inamuongoza kufanya nini na kuepuka toka kazi nini. Moyo haina kintu ingine paka sheria ya Mungu ndani ya kila mtu toka mwanzo ya kuumba yake. Hii sheria ni umoja na sheria ya kuandika, kwa sababu kila amri inatufundisha sheria ya Mungu, vile inatufundisha na moyo yetu.

Sheria ya Mungu inatuwambia kuamini paka kwa Mungu moja; vile inatuonyesha na moyo yetu. Kwa hivi na watu wa pagano mengi na shauria ya moyo yao, walifamia paka Mungu moja.

Sheria ya Mungu inatuwambia kuheshimiwa juu ya kila kiumbe ya dunia Muumba yetu na kwake paka inapaswa kuonyesha sifa ukubwa yetu; vile na moyo yetu inatuwambia.

Sheria ya Mungu inatufundisha hapana kusadiki ya kama mtu fulani ni pamoja na Mungu; hivi inatuwambia na moyo yetu.

Sheria ya Mungu inatuamuru kuonyesha utii kwa Mungu kama mkubwa mwenyezi wetu; vile inatuwambia na moyo yetu.

Sheria ya Mungu inatushauria kuogopa Mungu kama Muhukumu mwenye haki; vile tunasikia kutuwambia na moyo yetu.

Sheria Takatifu ya Mungu inahamuru kujilipiza wale watu wanachabula Jina ya Mungu; lakini na moyo yetu hasivumilia chabulana mbele ya Mungu.

Sheria ya Mungu inatushauria kutii kwa Mungu kuliko ya kila mamlaka ya hii dunia; vile na moyo inatuwambia, kwa sababu ma Mamlaka ya hii dunia ni chini ya Nguvu ya Mungu.

Sheria ya Mungu inaomba sisi kupenda Mungu kuliko ya bintu yoyote ya hii dunia; vile na moyo yetu inaomba, kwani Mungu ni Wema kabisa juu pia na Mwenyezi na chemchem ya kila kintu kizuri. Kwa hivi inapaswa sisi kumupenda kuliko ya kila kiumbe ingine.

Sheria ya Mungu inatuwambia kumushukuru Mungu juu ya yoyote matendo na bintu yake; vile inatufundisha na moyo; inatushauria kumushukuru Mungu na inatuwambia kumueshimiwa.

Sheria ya Mungu inatuwambia kukobeka kila kitumaini yetu kwa Mungu; vile na moyo. Kwani Mungu anaweza kufanya matendo yoyote kwani ni Mwenyezi, lakini kila kiumbe bila Mungu na mbali ya Mungu ni kintu kidogo na bila nguvu; kwa hivi na kitumaini yetu kwa matendo ya hii dunia ni ya wakati kidogo na bila nguvu.

Sheria ya Mungu inatufundisha kutii na kusifu wazazi wetu na wa kubwa wetu wote, kwani Mungu aliwapatia kuuongoza; vile tunasikia kutuwambia na moyo yetu.

Sheria ya Mungu inakataza sisi kufanya kazi kibaya kwa ndugu wetu ao kumuuwa; vile na moyo inatuwambia.

Sheria ya Mungu inakataza kufanya zambi ya mwili pamoja na ma bibi wengine; lakini na moyo ya mtu inafanyika makari na inahukumu hii zambi kwani hasipende kuharibifu maungo yake na hii zambi mbaya.

Sheria ya Mungu hasiache sisi kubeba bintu ya watu wengine, bila ruhusa yao; hii sauti inatuwambia na moyo yetu.

Sheria ya Mungu inatuwambia kupatia kwa kila mtu anayeomba moja saidio; vile na moyo yetu inatushauria.

Sheria ya Mungu inakataza kusema ma sauti wongo, kundaganya ao kulanda watu wengine; lakini na vile inatakaza na moyo yetu.

Sheria hasitake kusitake mukaribifu wetu; vile inatwambia na moyo wetu.

Sheria ya Mungu inatuamuru tusipende kuiba bintu ya watu wengine; vile inatuwambia na moyo yetu.

Basi, tunaona ya kama sheria ya Mungu na moyo ni pamoja na wanapenda kutusaidia kufika mu fasi moja nikusema kwa heri yetu.

Vile iko namna kusikia ya kama na wa pagano katika mwangaza ya mafundisho ya akili waliandika mawazo mazuri. Hii mafundisho yao juu ya Mungu moja kwa mufano ilitoka toka sheria ya moyo yao na somo ya bintu yote ya dunia.

Basi, kila mutu anayekosa kwa moyo yake, anakosa mbele ya sheria takatifu na mbele ya Mungu Muumba ya sheria. Huyu mtu mwenye hasitii kwa moyo yake, hasitii kwa sheria takatifu na kwa Mungu. Hasipende kusikia ma sauti ya moyo yake? Hii inatuonyesha ya kama hasitii hata kwa sheria, hata kwa Mungu. Moyo yake inasirika? Anasirika na huyu Mungu mumoja.

Hawa wa Kristiani wanayekanyanga moyo yao, hawasifu Mungu mukweli, lakini weko wadanganyifu. Tusisahabu ya kama bila moyo safi na kunioloka hakuna namna mtu moja kusifu na Mungu.

Mukristu ya kweli anasopoka juu hapana kukanyanga moyo yake, kwa sababu hasipende kukanyanga Sheria ya Mungu. Anapenda kutesa na hapana kufanya zambi. Paka kama moyo ni hivi Mukristu moja anapumzika na paka vile mtu ni mwenye furaha. Kama iko moyo safi iko na imani na furaha.

Sawa vile sheria ya Mungu anahukumu mtu kwa kila zambi, vile na moyo. Hii inaonekana kama watasikia moja neno ya uhukumu. Ile wakati wenye zambi katika moyo yao wanasikia haya na uhukumu.

Vile na mtu moja mupotevu anasikia haya, kama anasikia neno juu ya uzima upotevu. Wanasikia haya ma mwivi na manyanganyi, wakati watasikia neno juu ya kuiba na kunyanganya; wale wanasema wongo, wanasikia haya kama watasikia neno juu ya kuhukumu zambi ya wongo na ma zambi ingine.

Hawa watu wote wanasikia haya na wanaionyesha na ma alama ya inje. Ndani yao inatumika uhukumu ya moyo yao.

Sawa vile sheria ya Mungu anahukumu mwenye zambi na boka ya Uhukumu ya Mwisho, vile na moyo inafokea ndani yake: «Ee mtu, ukona mambo mnene juu ya wokovu wako»!

Sawa vile hapa inaunganishwa tendo ya sheria takatifu na tendo ya moyo, vile wataunganishwa na kwa Uhukumu ya Kristu: Pale sheria ya Mungu itahukumu mtu mwenye zambi, mwenye alikanyanga hii sheria; tena itamuhukumu na moyo yake kwa ajili ya zambi yake. Basi, pale kwa Uhukumu ya Mungu watakuwa wa wili washuhuda ya kusitake na kuhukumu: Sheria ya Mungu na moyo.

Iko namna wakati fulani moyo ya mtu moja kuwa ya kulala. Lakini inalamuka wakati moja na inaanza kuhukumu huyu mwenye zambi. Ile wakati inasimama ndani yake mahukumu toka moyo yake na kwa sababu hasiweze kuivumilia, mara ingine huyu mwenye zambi anakata maendeleo ya uzima yake na anaweka mwisho kwa uzima yake.

Lakini hakuna pumziko kuliko nzuri sawa hii pumziko ya moyo safi, kwani hivi hakuna tetemeko na uhukumu. Na, kama hapa hii uhukumu ya moyo yake inamuteswa mingi, ngapi mateso atasikia kwa uzima ya milele, ile wakati watakuwa zambi yake yote na watamuteswa sana!

Wa ndugu wangu, wenye zambi pamoja na mimi! Juu ya nini tunalala? Iko lazima kulamuka na kusafisha na kitubio na machozi zambi yetu; iko lazima kutengeneza maungo wetu na kusimama kufanya zambi na kufanya bilonda kwa moyo yetu. Namna gani tutasimama mbele ya Uhukumu ya Mungu, kama moyo yetu iko na uchafu na watafunguliwa ma Kitabu ya kila moyo yetu na kila mtu atabeba katika matendo yake?

# SEHEMU YA MBILI
# NJIA YA WOKOVU

## Habari Njema (Evangelio) ya wokovu

Hakuna kintu ingine kwa sisi wenye zambi utamu na upendwa na mwenye furaha kuliko ya Evangelio. Evangelio iko kuliko lazima kwa wenye zambi, kama wanafamia hali ya roho yao. «Maana Mwana wa watu alikuja kutafuta na kuokoa yule aliyepotea» (Luka 19, 10). Hii neno ni neno ya utulivu ya Evangelio ya Kristu. Ni nani Huyu «Mwana wa watu»? Ni Mwana wa Mungu, mfalme ya mbingu na mwana wa mfalme, aliyetumwa kwa sisi toka Baba wake mwenye mbingu. Kwa ajili ya mapendo yetu Yeye alitaka kuitwa «Mwana wa mtu». Juu ya nini alikuja mu inchi yetu? Juu ya kutafuta na kuokoa sisi wenye wapotevu na kutukokota mu Ufalwe wake wa mbinguni. Kintu ingine nini kabisa upendwa na kwa furaha itakuwa namna kutupatia Mungu kwa sisi wenye zambi?

Lakini sasa iko lazima kuangalia ni nini Evangelion inaomba nini ya sisi na inatumwa kwa nani?

A.

Evangelion ni, sawa inatuonyesha maana yake, ni moja habari ya furaha. Inakuhubiri mu dunia mzima Kristu kama Mwokozi ya dunia, aliyekuja kutafuta na kuokoa kondoo mupotevu. Musikieni mweye wote watu wenye zambi wa potevu! Musikieni habari ya furaha ya Evangelion. Inaita kwa sisi wote: . «Maana Mwana wa watu alikuja kutafuta na kuokoa yule aliyepotea» (Luka 19, 10).

Ni mambo matata kama mtu moja anaishi katika zambi mbele ya Mungu, lakini Evangelio inatukikiri ya kama zambi wetu wanasamehewa katika Jina ya Kristu na ya kama Kristu ni wokovu wetu.

Ni mambo matata kuishi chini ya hasira ya Mungu, lakini Evangelion inatuhubiri ya kama Kristu alituungana pamoja na Mungu: «Akakuja na kuhubiri salama kwenu muliokuwa mbali, na salama kwao waliokuwa karibu» (Waefeso 2, 17).

Ni matata «laana ya torati» kwa sisi, kwani sisi wote toko wenye zambi na hii sheria ya Agano la kale inaongoza kila mwenye zambi kwa malipizo ya sasa na ya milele. Lakini Evangelio inakikiri ya kama «Kristu alitukomboa kwa laana ya torati, akiwa alifanywa laana kwa ajili yetu, kama ilivyoandikwa».

Lufu ni matata kwa kizazi ubinadamu. Lakini Evangelio inatufundisha ya kama Kristu ni Ufufuo na Uzima wetu. Hadeze na Gehena ni matata. Lakini Evangelio inatukuhubiri ya kama Kristu alituuhuru toka Hadeze na mateso yoyote. Ni kintu kibaya kuepuka ya Mungu na Ufalme wake wa milele, lakini Evangelio inatukikiri ya kama tutakuwa pamoja daima na Kristu wetu kwa Ufalme wake ya milele.

Wa Kristiani wapenzi wangu, huyu sauti ya Evangelio ni kabisa butamu: «Onjeni mwone ya kuwa Bwana ni mwema» (Zaburi 34, 9). « Kwa maana Mungu alivyopenda ulimwengu, hata kutoa Mwana wake wa pekee, ili kila mutu akimwamini asipotee, lakini apate uzima wa milele. Maana Mungu hakutuma Mwana wake ulimwenguni kuhukumu ulimwengu, lakini ulimwengu uokolewe naye. Anayemwamini hahukumiwi, asiyemwamini amekwisha kuhukumiwa, kwa sababu hakuamini jina la Mwana wa pekee wa Mungu». (Yoane 3, 16-18). «Atukuzwe Bwana, Mungu wa Israeli; kwani amekuja kwa watu wake, na kuwakomboa. Ametunyanyulia pembe ya wokovu, katika nyumba ya mutumishi wake Daudi; » (Luka 1, 68-69).

B.

Tuliona ni nini Evangelio, sasa inapaswa kusopoka inaomba nini ya sisi.

Wa ndugu wangu, Evangelion inaomba kupokelea na shukrani hii habari iliyekuja toka mbingu na kushukuru daima Mungu mufazili wetu na roho yetu safi kwa hii ufazili Yake. Hii shukrani yetu inapaswa kuonyesha kama tunatii na tunasikia amri Yake. Tena na moyo umoja wetu inatushauria kuwa wenye shukrani mbele ya wafazili wetu.

Bwana alitupenda sisi wasiyostahili. Na sisi inapaswa kumupenda Huyu ambaye ni stahili ya mapendo yetu. Lakini mapendo inataka usileta haya kwake unamupenda na ma zambi yako. Mungu anasikia haya kwa zambi yetu. Kwa hivi tunapaswa kuepuka ya kila zambi yetu na kisha kumaliza Mapenzi takatifu Yake juu ya tusilete haya kwa Mungu Baba na Mufazili wetu. « Baba yetu, uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama mbinguni. . . ».

G.

Evangelio ya Kristu kwa nani inakuhubiriwa? Kristu anatujibu: «Roho ya Bwana ni juu yangu kwa sababu amenitia mafuta kuhubiri Habari Njema kwa masikini; Kuhubiri wokovu kwa wafungwa, na vipofu kupata kuona tena, kufungua waliochubuka, Kuhubiri mwaka wa Bwana uliokubaliwa». (Luka 4, 18-19). Nikusema, kwa wale watu wanasikia zambi wao, wanaona ya kama ni masikini kwa roho yao, wanasikia hali kibaya yao, wekona boka ya Uhukumu ya Mungu na roho ya kuvunjika; kwao inakuhubiriwa Evangelio, sawa vile tunaweka moja nguo na ndawa julu ya moja kilonda.

Wa roho wapenzi wangu, musikieni sauti kabisa butamu ya Evangelion: «Maana Mwana wa watu alikuja kutafuta na kuokoa yule aliyepotea» (Luka 19, 10). Muwekeni hii nguo ya uponyesho yulu ya ma nafsi yenu waliijaza na bilonda ya zambi yao. Paka na hii ndawa ya wokovu itaponyeshwa ma roho yenu: ««Maana Mwana wa watu alikuja kutafuta na kuokoa yule aliyepotea».

Mungu atatafuta na ataokoa na mweye kwani na mweye muko ya wale watu aliyekuja kutafuta na kuokoa. Mufamieni na mukikiri uzima yenu wa zambi mbele ya Mungu. Zambi yenu itasamehewa kwa ajili ya Jina ya Kristu. Mutobeni juu ya zambi yenu na musikieni taambu katika Mungu. Itatayarishwa na kwa mweye wokovu toka Mungu Mupendwa wetu. « Neno hili ni amilifu, na linastahili kukubaliwa na watu wote, ya kwamba Kristu Yesu alikuja kwa dunia kuokoa wenye zambi; na mimi ya kwanza wao». (Barua ya Kwanza ya Timoteo 1, 15). Roho Mtakatifu anamiambia na mutumishi Wake Daudi: «Zabihu za Mungu ni roho ya kuvunjika, moyo uliovunjika na wa toba hutauzarau, ee Mungu» (Zaburi 51, 19). Hii zabihu ya roho inayevunjika na inatoba ni kabisa wa shukrani mbele ya kila ingine matoleo. Moja zabihu sawa hii Mungu anaiona na mapendo na anatuma baraka Yake: «Lakini nitaangalia mutu huyu: mutu aliye masikini, mwenye roho ya kupondeka, na anayetetemeka kwa ajili ya neno langu» (Isaya 66, 2).

Kisha hii mafundisho, utaweza kusikia, ndugu wangu, ya kama Evangelio hasikujipatia kwa wale wa Kristiani wanaishi na uzulumu na bila boka ya Mungu na awafamia zambi yao, hali matata ya uzima yao kwa ajili ya zambi yao na hakuna kwao roho ya kuvunjika. Faida gani iko kama tunamwanga mwamba moja na mafuta? Nguo ya tunzo tunaiweka pa moja kilonda ya mtu moja anayeomba tunzo yake na anapokelea hii ndawa.

Kwa wale watu ni muzuri kusema hii ma neno: «Huzunisheni na kuomboleza na kulia. Macheko yenu yageuke kuwa maombolezo, na furaha yenu igeuke kuwa masikitiko. Mujinyenyekeze mbele ya Bwana, na ye atawanyanyua ninyi». Barua Yakobo 4, 9-19). Tena: «Na shoka limekwisha kuwekwa katika shina la miti; basi kila muti usiozaa matunda mazuri unakatwa, na unatupwa katika moto» (Matayo 3, 10).

Ee wandugu wenye zambi, tunaogopa ile siku ya Uhukumu ya Mungu na tunatumika juu ya kupata «roho ya kuvunjika, moyo uliovunjika», juu ya kukokota na sisi toka Evangelio kama chemchem ya wokovu, Maji muzima, ya utulivu ya furaha na vile ma nafsi yetu watapata furaha ya milele.

## Ubatizo Takatifu

« Anayeamini na kubatizwa ataokolewa» (Marko 16, 16). Huyu neno aliisema Mwokozi wetu juu ya kupata sisi nguvu na utulivu. Ni nini kuliko utulivu kwa nafsi moja kama anasikia hii ma neno na anajua ya kama atapata wokovu ya milele?

Utukufu kwa Mungu, wa Kristiani wapenzi, kwa sababu na sisi tunaamini Evangelio na tulipata nuru katika Ubatizo takatifu mu Kanisa Orthodokse. Ni stahili sasa kuangalia na nguvu yake, tena kuona tulikuwa nini mbele ya Ubatizo yetu, tulifanyikwa nini kisha Ubatizo yetu na hivi tutasikia utulivu mnene.

Katika Ubatizo Takatifu tuliokolewa toka yoyote mateso na tulibeba Neema ya Mungu nikusema furaha ya kweli. Mbele ya kubatiziwa tulikwa mbali kabisa ya Mungu; Lakini na Ubatizo yake tulimukaribia Mungu. Mbele ya Ubatizo yetu tulikuwa wa adui ya Mungu; kisha Ubatizo tuliunganishwa na Ye na Huyu pamoja na sisi. Mbele ya Ubatizo yetu tulikuwa watoto ya hasira; lakini kisha Ubatizo tulifanyikwa ma chombo ya rehema takatifu. Mbele ya Ubatizo tulikwa watoto ya giza na shetani; kisha tulifanyikwa watoto ya nuru na ya Mungu. Mbele ya Ubatizo yetu tulikuwa wenye zambi; kisha Ubatizo tulisafishwa, tuliangazwa na tulipata uhaki. Mbele ya Ubatizo tulikuwa wapotevu; kisha tulifanyikwa wenye wokovu. Mbele ya Ubatizo milango ku ufalme ya milele walikuwa ya kufungwa; kisha walifungula na wanaingia na uhuru ninyi wote walichunga neema ya Ubatizo safi.

Hii ma baraka na wengine mengi tunabeba na Ubatizo mu kanisa yetu. Tunabeba hii ma rehema bila kuwa sisi wenye stahili, paka katika wanadamu ya Mungu, kwa sababu mtu moja mwenye zambi ikona nini stahili na utukufu? Basi, utukufu kwa wema ya Mungu, utukufu kwa wanadamu Yake, utukufu kwa mapendo yake, utukufu kwa ma rehema yake! «Jina la Bwana lihimidiwe tangu sasa, na mupaka milele» ( Zaburi 113, 2).

Hii rehema mingi ya Mungu alituletea kwa sisi Mwana wake wa pekee Yesu Kristu; alituletea hii rehema kwa sisi katika Damu na Lufu Yake.

Wa Kristiani wapenzi, inapaswa kukumbuka Ubatizo Takatifu na kuangalia sisi maungo wetu: Tunaishi sawa vile inapaswa hii neema ya Ubatizo Takatifu wetu? Aipaswe kufanyika huyu Ubatizo yetu malipizo kwa ile siku ya Uhukumu ya Kristu, pahali Mungu atahukumu kila neno na uwazo na tendo yetu.

## Kukataa na Malako

Ubatizo Takatifu ni mulango pahali wanaingia wenye ubatizo mu kanisa na wanafanyikwa «wenyeji pamoja na watakatifu na watu wa nyumba ya Mungu» ( Waefeso 2, 19). Hii tendo hasifanyikwe bio-bio, kwani mbele ya Ubatizo iko lazima mtu kukataa na kulaka malako filani.

A.

Sisi wote tulikataa shetani na yoyote matendo yake. Shetani ni roho mbaya na mwovu. Aliumbwa toka Mungu mwema, lakini pamoja na wa ndugu wake alijiepuka toka Mungu na vile alifanyikwa mwenye giza, mbele alikuwa mwenye nuru, alifanyikwa mwovu lakini mbele alikuwa mwema. Matendo yake ni kuwabudu ma sanamu, majivuno, matendo ya kulanda watu wengine, wongo, udanganyifu, uovu, tamaa, chuki, zambi usharati na kila zambi ya mwili, chabulana na kila zambi, kwani huyu shetani ni muumba ya zambi. Huyu ndani ya Paradizo alilanda ma Babu wetu ya kwanza na aliwatupa mu zambi na aliwaepuka toka Mungu. Huyu basi, roho musiyesafi na matendo yake waovu wote tunakataa mbele ya kubeba Ubatizo ya Mungu.

B.

Tulikataa kila furaha ya hii dunia, majivuno na ma furaha ya hawa watu ya hii dunia kwani alituita Mungu kwa uzima ya milele na uzima mupya.

G.

Tulijilaka ya kama tutatumika na imani na roho kweli Kristu, Mwana wa Mungu pamoja na Baba na Roho Mtakatifu na hivi tutafata ma mwendo Wake.

D.

Kwa hivi ilifanyikwa katikati yetu moja masikilizano: Sisi tulikataa shetani na tulilaka kutumika Mungu na kuwa waminifu Wake; na Mungu anatupokelea kwa rehema yake na anatulaka uriti ya uzima ya milele na ufalme na kwa sababu tuko wenye buchafu kwa ajili ya zambi yetu Yeye anatusafisha na nguvu ya Ubatizo, anatutakasa, anatupatia haki yake, sawa vile hivi anasema na Ibada ya Ubatizo ya Kanisa yetu: «Ulihakikishwa, uliaangazwa, ulitakaswa, kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristu na kwa Roho wa Mungu wetu».

*****

Wakristiani wapenzi wangu, tunakumbuka kila siku ma sauti yetu ya kukataa na kulaka kwa Mungu na tunauliza maungo wetu kama sisi tunaifata. Kwa sababu ni zambi mnene kama mtu moja anasema wongo kwa Mungu na wale wanaonga wanapata hatari.

Tena basi, tunapaswa kuangalia kama mtu moja katikati yetu alirudia kwa shetani na alikataa Kristu. Mu fasi wapi tuko sisi? Mu fasi ya shetani ao Kristu? Kama mtu moja anafanya mapenzi ya shetani eko pamoja naye na, kama anafanya mapenzi ya Mungu, ni pamoja na Yeye.

Mtu moja anakataa Kristu hapana paka kama anakataa Jina yake na anakataa kumukikiri kama Mwana wa Mungu na Mwokozi wake, lakini na huyu ambaye bila moyo, bila boka anakanyanga ma amri Yake takatifu. Hii sauti ni fundisho ya wa Mitume, kwa sababu Mtume anatuwambia: «Wanakiri ya kwamba wanajua Mungu, lakini kwa matendo yao wanamukataa; » (Tito 1, 16).

Unaona ya kama hapana paka na midomo, lakini na matendo watu wanakataa Mungu? Mtu moja anaishi na zambi ya mwili na analewa? Anakataa Kristu. Anasirika mwingine kupigana ya mukaribifu yake na anaomba nyakati nzuri juu ya kumufanyisia kazi kibaya? Yeye ni mbali ya Kristu. Analanda mtu mwingine ndugu wake? Hakuna namna kuwa pamoja na Kristu.

Vile mtu moja anatumika chini ya mamlaka ya adui. Vile asifata amri ya Mungu na malako aliipatia kwa Mungu na anaonga mbele ya Mungu.

Wapenzi wangu, iko lazima kuuliza moyo yetu na uzima yetu tuko mu fasi gani; mu fasi ya Kristu ao mu fasi ya adui yetu? Mu fasi ya njia mbaya ao mu njia nzuri: mu njia ya wenye wokovu ao mu njia ya wenye kupotea? Huyu asiye kuwa pamoja na Kristu ni kupigana Kristu, sawa vile anatuonyesha na Bwana mumoja: «Mutu asiye pamoja nami ni juu yangu; naye asiyeokota pamoja nami anasambaza». (Matayo 12, 30).

Wa ndugu wangu, tunasopoka mingi juu ya kuwa pamoja na Kristu kwa hii dunia, sawa vile tulilaka Kwake ile wakati ya Ubatizo yetu. Kama tuko sisi hapa pamoja na Kristu, tutakuwa pamoja na kwa uzima ya milele, katika malako yake yasipo wongo: «Kama mutu akinitumikia, anifuate; na pahali nilipo, pale mutumishi wangu atakaa; kama mutu akinitumikia, Baba yangu atamuheshimu». ( Yoane 12, 26).

Tunakombana kumutumikia hapa kama Mfalme wetu na Mungu wetu juu ya kutufamia ile siku ya Uhukumu kama watumishi wake na kutuhesabu pamoja na waminifu watumishi Wake na kutufungula mulango ya furaha wa milele. Amina.

## Zambi kisha Ubatizo

Hakuna namna kusema ao kuandika mtu fulani hali ya yule Mukristu alijitoa, kisha Ubatizo yake, mu zambi: Anapotesha yoyote ile ma baraka aliistahiliwa kukamata kisha Ubatizo zake, na neema ya Mungu na ananguka kupita chini mu zambi ya ile hali alikuwa mbele ya Ubatizo zake. Kwani alifamia fundisho ukweli, lakini hasikutake kuishi kwake. Alifamia Mungu, lakini

asikutake kumufata. Alifamia njia inayeongoza mu heri ya milele, lakini alikataa kuitembea. Alifunda na alilaka kutumika Bwana Yesu, lakini alikataa kufata malako yake. Alinawa, aliangazwa, alihakikishwa, lakini kisha alipotesha yoyote bintu takatifu. Alifanyika mtoto ya Mungu, lakini kisha alipotesha hii baraka kimungu. Alifanyika muriti ya uzima ya milele na ufalme, lakini alipotesha hii uriti. Kwa huyu mtu na wale wanamufata anaria Mtume Petro hivi: «Maana ingekuwa heri kwao kama wasingalijua njia ya haki, kuliko kujua, kisha kuacha ile amri takatifu waliyopewa» (barua ya mbili ya Mt. Petro 2, 21).

Unaona, ndugu wangu, uharibifu nini ni kama Mukristu moja atafanya zambi? Na uwaza ya kama hii uharibifu hasionekane sasa, kwa sababu hasionekane na ma macho ya mwili yetu, lakini na ma macho ya roho. Itakuwa ya kufamia ile wakati matendo yetu yote wataonekana mbele ya dunia mzima, nikusema kwa Ufikisho ya Mbili ya Bwana Yesu Kristu.

Ile wakati huyu Mukristu mupotevu ataona na atasikia hii mateso na uharibifu mnene.

Ni kweli, ngapi machozi na maombolezo iko lazima kutosha huyu Mukristu kama anaishi kwa hii hali ya hatari? Sawa huyu mtu aliyenawa ndani ya maji na kisha alitelemuka na alijaza na uchafu, vile na Mukristu aliyenawa ndani ya Maji takatifu ya Ubatizo, anapata uchafu kwa ajili ya zambi yake.

Huyu Mukristu anayefanya zambi, kisha Ubatizo yake, anafanana na mtu moja mbunji, ambaye walimuvaa na manguo mazuri, lakini yeye alitupa hii mavazi nzuri na alivaa mara ingine ma nguo yake mbaya ya zamani. Mukristiani na ma kilako ya zambi yake alivaa mavazi ya haki ya Kristu; lakini anatupa hii mavazi ya Mungu na anavaa mara ingine ma kilako yake ya wenye zambi.

Huyu Mukristu ambaye alitoka ya giza ya zambi yake kwa nuru ya Kristu, nuru ukweli na kisha alirudia mara ingine pale aliishi zamani anafanana sawa yule mtu alitoka ya giza kwa nuru na kisha alirudia mara ingine ndani ya giza. Huyu Mukristu ambaye anafanya zambi anafanana sawa huyu mtu ni muhuru, lakini kisha anarudia mu uzima ya utumwa yake.

Kwa hii fasi mbaya niko hawa watu:

1. Wenye zambi ya mwili na wapotevu na wote watu wanayefanya kila zambi ya mwili.
2. Ma mwivi, wanyanganyi, na ninyi wote na namna ya kuachana wanakombana kuiba bintu ya watu wengine.
3. Watu wenye mbaya na ninyi wote wanakombana kuharabisha uzima ya wakaribifu wao.
4. Wadanganyifu, wenye waovu na ninyi wote wanaishi na namna uwovu mbele ya watu wengine.
5. Wenye kuchabula, wenye kukombana na wenye kuchukua.
6. Ninyi wote wa mwamuzi wenye wanahukumu kila mambo na makuta na hapana katika malako ilipatia na katika kweli.
7. Wakubwa watu, wenye awaonyesha mapendo na wema kwa watumishi wao.
8. Ninyi watu wa biashara, wenye wanauza bintu yao mbaya na makuta mengi, wanauza bintu ya kuoza kama bintu mazuri, wanaomba makuta mengi na yulu ya bei yao ya nzuri.
9. Ninyi wote wanafanya matendo ya malozi, tena wale wanaenda kwa mafumu ao wanawaita ma nyumba yao.
10. Ninyi wote wanakanyanga ma amri ya Mungu bila boka na wanafanya kila zambi.

*****

Wa Kristiani wapenzi, wenye mulisafishwa na maji ya Ubatizo Takatifu! Sisi wote inapaswa kuangalia maungo wetu kama tuliepuka toka Kristu wetu na tulianguka mu uzima ya shetani. Kila mutu anayekuja kupindua ya sheria kimungu, anatumika kwa shetani na anajiepuka toka Yesu Kristu.

Ole kwa wale wa Kristiani wanayefanya zambi, kisha Ubatizo yao! «Itakuwa kuvumilika kwa Sodomo na Gomora katika siku ya hukumu kuliko muji ule» (Matayo 10, 15), na hapana kwa wale wa Kristiani!

Ee Mukristu mwenye masikini, angalia nzuri maungo yako na sopoka usifanyika daima mutumwa ya shetani na uharibifu. «pahali pasipokoma funza lao wala moto hauzimiki» (Marko 9, 48).

Ee Mungu wangu,
penda kiumbe yako wa akili,
uliyemuomba
katika mufano wako. . .

## Njia ya kurudia

Huyu mtu anayefanya zambi, kisha Ubatizo yake, kitumaini moja wa pekee ilibakia kitubio yake ya kweli. Utukufu kwa Mungu ya hii toba! Utukufu kwa Mungu, kwa sababu tusikuharibifu kamili! Ilitubakia kwa sisi kitumaini moja. Bado tena kuisha ma wema ya Mungu. Tena inakuhubiriwa kwa wenye zambi toba. Tena watu wenye masikini wanasikia tangazo ya wokovu. Tena inazambalishwa ma fasi yote ya dunia ma rehema ya Mufalme ya mbinguni. Bado kufungwa milango ya upenda-wanadamu ya Mungu wetu. Neema ya Mungu inajitoa kwa sisi wote. Tena inafundishwa Evangelio na «Kondoo wa Mungu anayezibeba zambi za dunia». Tena inatangazwa Ufalme ya Mungu. Tena wanaokolewa wa Kristiani wenye kutubu; wanaingia mu Ufalme ya Mungu watuzakodi na wenye usharati kisha kitubio ukweli yao. Tena Mungu mupenda-wanadamu anaita na anongolea karibu Yake wakafiri wote na anawalaka rehema yake. Tena Baba mupenda ya watoto wake anapokea wa mwana wapotevu wake, wenye wanarudia toka inchi ya mbali; na anafungula milango ya nyumba Yake na anawapatia kuvaa mavazi ya kwanza na anawapatia mu kilole yao pete na bilato kwa miguu yao na anawashauria wote watakatifu kufurahi mukusema:

Ee Wamalaika, mufurahi mweye wote na Watakatifu wangu wote! Hawa wenye zambi, watu, viumbe vyangu walijiumbwa katika mufano wangu wanaokolewa, hawa wenye wapotevu walionekana na wenye wafu walifufuka na wapotevu walirudia.

Utukufu kwa wema Wake! Utukufu kwa upenda-wanadamu Wake
Utukufu kwa mapendo ya watu Wake!

Ee wenye zambi na wa masikini, juu ya nini sisi tunachelewa kuikaa ku inchi ya mbali na tusirudie kwa Baba wetu? Juu ya nini tunakufa kwa njaa? Juu ya nini tunakombana kuziba na ma zambi yoyote, sawa yule mwana mupotevu alikuja matunda ya kukauka? Mu nyumba ya Baba wetu iko ma bintu yote. Pale watumishi yake wanaziba na sisi tunakufa mbali kwa njaa?

Baba wetu anatuongolea na mapendo na uvumilia mingi. Sisi wenye tunataka kurudia kwake, Yeye atatuangalia ya mbali na macho ya mapendo na furaha ya kujaza. Atakuja bio, ataanguka pa singo yetu, atatubatia, atatubusu, atatulivu bila kukumbuka mazulumu na zambi yetu. Ile wakati wataanza pempeni yetu kufurahi na kushangilia Wamalaika wote na Watakatifu wake wote.

Basi, inapaswa kulamuka na kurudia bio Kwake Baba wetu na kila mtu kumwambia na unyenyekevu na umivu: «Baba, nimefanya zambi juu ya mbingu na mbele yako; sistahili tena kuitwa mwana wako, unifanye kuwa kama mumoja wa watumishi wako wa mushahara» (Luka 15, 18-19).

Ee wa ndugu wenye zambi, tunapaswa bio sasa kurudia, wakati bado kupitisha, sasa Baba wetu anatuongolea; sasa twende kurudia kwa sababu bado kufungwa milango ya Nyumba yake takatifu!

*****

Ee Ndugu wangu, kama ulifanya zambi kisha Ubatizo yako, kama ulitubu kweli, usipotee kitumaini yako. Kamata msaada neema ya Mungu. Kama ulifanya zambi kuliko mnene, usipotee

kitumaini yako, kwa sababu neema ya Mungu ni kupita ukubwa na mnene. Lakini sopoka kisha mu uzima yako, usikose mara ingine na tembea katika Sheria kimungu.

Kama ulikosa kama mtu wa zambi mu njia ya maisha yako, usipotee kitumaini yako. Sikia mara moja zambi na kosa yako, pika magoti yako chini na unyenyekevu mbele ya macho wa mapendo ya Mungu omba rehema yake kama mtu mutozakodi: «Mungu unirehemu mimi mwenye zambi» (Luka 18, 13), na zambi yako itasamehewa.

Wa ndugu wangu, tunatubu sasa kwa sababu inatumika tena upenda-wema ya Mungu; hivi tutaepuka tendo ya haki kimungu Yake na tusiende mu Gehena.

## Mwokozi

Ufikisho ya Mwana wa Mungu katika mwili Yake mu dunia wanapatia nguvu kwa watu wenye zambi, kwani wanapata wakati kutubu.

Ya mtu gani gani alishuka chini Kristu? Juu ya sisi wenye zambi. Na ya mambo gani? Juu ya wokovu wetu. O, ngapi tendo ukubwa ni wokovu wetu mu akili ya Mungu wetu! Kwa ajili ya wokovu wetu, ewe wa ndugu wenye zambi, alikuja Huyu mumoja duniani. Musikieni hii habari mweye wote wa ndugu wenye zambi na muwazeni: Mungu mumoja alikuja hapa kwa ajili ya wokovu wetu na tena alikuja na uso yetu kama mutu. «Ni pasipo shaka, siri ya utawa ni kubwa: Mungu alionekana katika mwili» (Barua ya kwanza kwaTimoteo 3, 16). «Bwana, mutu ni kitu gani hata unamujua? Ao mwana wa watu, hata unamwangalia? (Zaburi 144, 3).

Kweli neema ya Mungu kwa mutu ni wa ajabu! Tendo yake ni stahili ya ajabu! Hii aliona ku mbele Nabii, alipaza sauti na boka na alisema: «Ee Bwana, nimesikia habari zako, na ninaogopa; ee Bwana, fufua kazi yako katikati ya miaka; » (Habakuki 3, 1-2).

Ee wa ndugu wenye zambi, tunakumbuka sasa hii tendo ukubwa ya Mungu, iliyefanyikwa kwa ajili yetu na inapaswa kutubu. Tunawaza sasa ya kama alizaliwa toka Bikira Maria kwa ajili yetu, alifanyikwa mtoto mdogo na alikunywa mazimba! Alikuwa pasipo kuonekana na alifanyika ya kuonekana kama mutu katikati yetu; alikuwa bila mwanzo na alikamata mwanzo na alifungwa na ma sanda kama mtoto mdogo; alikuwa bila mwili na alikamata mwili lakini bila zambi!

Tena inapaswa kukumbuka namna gani, wakati alikuwa mtoto mdogo, alikimbia kufijichama toka mfalme Herode mubaya. Tena tunakumbuka ya kama aliishi na alitembea mu inchi yetu; tena ya kama kwa ajili ya wokovu wetu alitembea mu kila muji na mukini na alichoka; huyu aliyekuwa namna kumukaribia majeshi ya Keruvimi na ma Serafimi, mu inchi yetu alitembea pamoja na watu wenye zambi; ya kama alikuwa na Kiti mbingu na kibasa inchi na aliikaa ndani ya nuru yasiyokaribia, lakini mu inchi yetu hasikukuwa na fasi ya kupumzika kichwa yake; tena alikuwa mutajiri sana, lakini alifanyikwa masikini juu ya kuwa sisi watajiri (Barua ya mbili kwa Korinto 8, 9).

Tena inapaswa kukumbuka ya kama Huyu aliyevaa nuru kama nguo (Zaburi 104, 12), alivaa mavazi (mwili) yetu ya bure; aliyepatia chakula kwa kila nyama (Zaburi 136, 25) kwa inchi yetu aliishi na mukate ya inchi yetu; huyu mwenyezi alionekana kama mutu pasipo nguvu na huyu anayepatia nguvu mu dunia, alichoka hapa kama mutu ya bure.

Tena tunakumbuka namna gani Huyu aliyekuwa mukubwa ya kila utukufu na sifa, alijichabula toka midomo ya watu wenye zambi, walimuchabula na matusi mbaya na walimuchokoza. Tena tunakumbuka namna gani aligonjwa, alitaambu, alisikitika, aliria, alisikia uovu; namna gani alijitoa toka mwanafunji mukafiri wake na alijiuzisha na bei ya makuta 30 na wanafunji wengine walimuacha; namna gani walimukokota kwa uhukumu, namna gani walimuhukumu wenye wazulumu na wasiyohaki; namna gani walimupika na fimbo, walimuvaa nguo ya kumuchokoza, walimuchabula na walimuwambia ma neno ya udanganyifu sawa hivi: «salamu ee mfalme wa Wayuda»! Namna gani walimuweka pa kichwa yake taji ya miimba, walimupika na simbala na alisikia Yesu toka ma kinywa ya Wayuda: «Umwondoshe, umwondoshw, umusulibishe! » (Yoane 19, 15).

Tena tunapaswa kukumbuka ya kama wanyanganyi wa wili waliwaongoza pamoja na Yeye juu ya kuwasulubia pempeni Yake. Na ku mwisho alikufa Mwokozi wetu pa Musalaba!

Hii matendo yake yote alitenda Mwana wa Mungu kwa ajili ya wokovu wetu! Ee wa ndugu wangu wenye zambi, sisi wote tumepotesha wokovu wetu kwa uso ya Adamu, tena na kila furaha; lakini Kristu Mwana wa Mungu na wema ya Baba wake wa mbingu alituokoa.

Basi, Mungu hasitukuache sisi wenye zambi. Kwa ajili ya wokovu wetu Damu ya Kristu ilijimwanga pa Musalaba. Mateso yake ni lazima kutusaidia juu ya kutubu na tusipotee wokovu ya milele. Bila toba, hakuna wokovu hata ya mtu moja; lakini mtu mwenye zambi hasisubuka juu ya hii kazi ya wokovu wake.

Mungu ni mupenda-wanadamu na alionyesha hii mapendo yake na matendo Yake. Kama utatubu kweli utaokolea; lakini mtu mwenye zambi hasisubuke hii kazi.

Kristu, Mwana wa Mungu, ufunua ndani ya Evangelio ufikisho Yake mu dunia kwa ajili ya wokovu ya dunia. Anaonyesha unyenyekevu ukubwa Yake, machoko, maumivu, ma taabu na lufu Yake, -lufu pa Musalaba-na anasena kwa kila mtu:

-Ee Mutu, hii matendo yote nilifanya kwa ajili yako na kwa wokovu yako nilivumilia na nilipokea na weye unazarau wokovu yako! Unazarau, kwani usipende kutubu, kuepuka toka zambi na kukunywa Damu Yangu juu ya kupata Uzima mupya ndani yako.

Lakini mtu mwenye zambi anasikia sauti utamu na katika ombi ya Yesu, lakini anamuzarau. Kristu anamulaka kusahabu zambi na mazulumu yake, kama atarudi Kwake, lakini mtu mwenye zambi hasipende kumusikia.

Kristu anamuita kuja karibu yake na anamulaka pumziko, lakini huyu mwenye zambi hasipende kuonyesha mafa. Anabakia bila toba, sawa vile alikuwa zamani; anazulumu sawa vile alizulumu zamani; anafanya matendo ya uwovu, sawa zamani; anapenda giza, sawa aliipenda na zamani; anachukia mwangaza, sawa vile aliichukia na zamani. Vile hasikuje ku nuru, lakini anabakia pamoja na shetani, mkubwa ya giza.

Ee mwenye zambi, mtu maskini, lamuka na kuja kuona moyo yako, kwa sababu Huyu Damu ya Kristu atakuhukumu, kwani uliizarau. Huyu Damu ilimwangishwa toka mbavu ya Kristu kwa ajili ya wokovu yako.

## «Taifa takatifu»

«Tazameni, ni mapendo namna gani tuliyopewa na baba, tuitwe wana wa Mungu» (Barua ya Kwanza ya Yoane 3, 1). O, ni ngapi wema na upenda-wanadamu ya Mungu! Matendo ngapi alionyesha Mungu kwa sisi! Na ma namna gani Neema yake alitutembelea! Zamani tulikuwa wenye masikini na wenye kuzarawa na sasa tulifanyikwa watoto ya Mungu!

Hii mambo ya ajabu anaona Mtume ya Kristu na anapaza sauti kusema: «Tazameni, ni mapendo namna gani tuliyopewa na Baba, tuitwe wana wa Mungu». Basi, ni kuliko ajabu kama mtu moja mwenye zambi atafanyikwa mwana wa Mungu? Hii kazi alifanya mapendo ya Mungu kwa mtu.

Basi, kama wa Kristiani ni watoto wa Mungu, ni na «wariti wa Mungu na wariti pamoja na Kristu» (Kwa WaRoma 8, 17). Kama hawa weko watoto wa Mungu, wataongopa nani na juu ya nini? Juu ya nini wataogopa wa adui, shetani, lufu na hadeze? Mungu ni pamoja yao; na «kama Mungu akiwa upanda wetu, ni nani aliye juu yetu? » (Kwa WaRoma 8, 31). Hii zawadi juu pia ya Mungu, nikusema kuwa watoto Wake, tunaibeba kwa Ubatizo yetu. Tangu ile saa mtu anazaliwa katika neema ya Mungu na anabeba jina mupya kuitwa «mwana wa Mungu».

*****

Wa ndugu wapenzi wangu, misiweze kuajabu stahili wema mingi ya Mungu na upenda - wanadamu wake iliyeonyesha kwa sisi wenye zambi. Wakati ninawaza hii wema Yake, ninasema

pamoja na Nabii Daudi: «Bwana, mutu ni kitu gani hata unamujua? ao mwana wa watu, hata unamwangalia? » (Zaburi 144, 3).

Wakati ninawaza utukufu ngapi alipatia Bwana kwa mtu, ninashangaa! Sifa na mwanzo ya uzima yake iliyepatia Mungu mpenda-wanadamu kwa mtu ni hata ukubwa kabisa na sisi tusiweze kuiandika ao kuifafanusha na maneno yetu; tena hakuna namna kuisikia hii mapendo yake. « Lakini ninyi ni taifa chaguliwa, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu walio mali ya Mungu mwenyewe, mupate kutangaza uzuri wake aliyewaita ninyi toka giza mwingie katika nuru yake ya ajabu» (barua ya kwanza ya Petro 2, 9), anasema kwa wakristiani ya kweli Mtume Petro. Kwa hii sauti ya Mtume sisi tunaona wema ukubwa na ubinadamu ya Mungu kwa kila mtu.

Lakini sisi twende kukombana juu ya kusikia na ma macho ya roho yetu hii sifa na utukufu yetu katika Kristu, juu ya kuanza na mapendo mingi kutafuta hii utukufu yake.

Ee ndugu wangu, fugula, basi, masikio ya nafsi yako na sikia:

A.

Mukristu ya kweli anaitwa na eko mtoto ya Mungu. Ni nani jina ingine kuliko utukufu ya hii jina kwa mtu? Vile anandika Mtume Yoane na anasema wa ajabu kwa wa Kristiani: «Tazaameni, ni mapendo namna gani tuliyopewa na Baba, tuitwe wana wa Mungu» (Barua ya kwanza ya Yoane 3, 1). Kwa hivi na wa Kristiani wanaita Mungu kama Baba wao na wanasema: « Baba yetu uliye mbinguni. . . »

Ni kintu ya utukufu kama uko mwana ya mfalme moja ya hii dunia; lakini kuliko ya utukufu ni kama uko mwana wa Mungu, Mfalme wa mbinguni. Sifa, utukufu na stahili na jina mukubwa na yoyote matukufu ya hii dunia hakuna hata stahili moja mbele ya hii sifa: kuwa mwana wa Mungu. Utukufu kwa Mungu mpenda wanadamu!

O, muujiza ukubwa! Sisi watu wenye zambi tunasema kwa Mungu: «Baba yetu. . . ». Ufwasi na sifa yetu ngapi ni urefu, wa ndugu wapenzi wangu! Baba ya Mwana Wake wa pekee ni na Baba wetu, Mungu Wake ni na Mungu wetu, sawa vile na Huyu mumoja inatukikiri kwa furaha yetu: «Ninapanda kwa baba yangu na Baba yenu; na kwa Mungu wangu na Mungu wenu». (Yoane 20, 17).

Wandugu wapenzi wangu, tunakumbuka sasa Ubatizo yetu takatifu na neema ukubwa ya Mungu, ile tulibeba ile wakati ya Ubatizo yetu; tulifanyikwa watoto ya Mungu. Utukufu kwa Mungu juu ya hii zawadi yake.

Lakini watoto wanafanana kwa wazazi wao; «Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho» (Yoane 3, 6). Nikusema na wa Kristiani inapaswa kufanana na Mungu, kwani walizaliwa toka Mungu.

Basi, tunapaswa na sisi kuonyesha na matendo yetu ya kama tuko watoto ya Mungu. Mungu ni Mtakatifu? Na sisi tunapaswa kuwa watakatifu. Yeye ni mwenye Haki? Na sisi tunapaswa kuwa wenye haki. Yeye ni mwema, «sababu yeye anaangazia jua lake waovu na wema, naye ananyesha mvua wenye haki na wasio haki»? (Matayo 5, 45). Na sisi tunapaswa kuwa wema kama tunafanya kazi kizuri kwa watu marafiki na wa adui yetu. Mungu anajaza katika wema wake? Na sisi tunapaswa kuwa wapenzi-wema na kuonyesha wema wetu kwa ndugu wetu wenye waumivu. Yule anachukia zambi? Na sisi tunapaswa kuichukia na kutoka mbali yake. Mungu anatupenda? Na sisi twende kupenda moja kwa mwingine. Yeye anasamehe zambi yetu? Na sisi twende kusaamehe zambi ya wa ndugu wetu. Kwa hii ma shauria yote na Mtume Paulo anatuwambia hivi: « Basi mufuate Mungu kama watoto wanaopendwa; » (Kwa Waefeso 5, 1).

B.

Mukristu ya kweli eko na ungano na ushirika nguvu pamoja na Baba na Mwana Wake Yesu Kristu, sawa vile anatutangaza na Mtume mukuandika hivi: «Na ushirika wetu ni pamoja na Baba na pamoja na mwana wake, Yesu Kristu». (Barua ya kwanza ya Yoane 1, 3). Kintu ngapi ukubwa ni hii kila mtu anaweza kuisikia.

Watu wanaona ya kama urafiki na ushirika pamoja na mfalme ya inchi yao ni kitu kizuri sana. Lakini ngapi kuliko ukubwa ni kama tukona ushirika na urafiki na Mungu wa mbinguni, ambaye ni «mfalme ya wafalme na Bwana ya wa bwana» na anaikaa ndani ya nuru! Matendo ya

ajabu ma ngapi alifanya kwa ajili yetu wema na upenda-wanadamu ya Mungu! Angalia na ajabu, ee ndugu wangu, kizazi na utukufu yako wa Kristu: Ukona ushirika na ungano pamoja na Mungu mukubwa na musiyekusikia!

Ee Bwana ilijijaza na ilijistaajabu wema na upenda-wanadamu Wako kwa mutu mwenye zambi na maskini kuliko na juu ya kila sauti yetu na uwazo yetu!

G.

Mungu wa mbinguni, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu anafurahi kuikaa ndani ya mwaminifu moja kama hekalu nzima. Anasema karibu Bwana Yesu: «Kama mutu akinipenda, atatii neno langu, na Baba yangu atamupenda, nasi tutakuja kwake, na tutafanya makao yetu kwake». (Yoane 14, 23). Kintu nini kupita kabaila na ukubwa anaweza kutakia nafsi moja, kama Mungu ya Utatu Mutakatifu anapenda kuikaa kwake?

Kama ni sifa mnene watu kupokelea mfalme ya hii inchi mu nyumba yao, ngapi sifa ukubwa itakuwa kama watapokelea mu nyumba ya nafsi yao Mfalme ya dunia mzima, ambaye atabakia ndani ya roho yao ya milele? Nini heri ukubwa kwa nafsi moja kama ndani yake anaikaa daima Mungu? Paradizo ya furaha na shangilio ni ndani yake. O, wenye heri! O, utukufu! O, sifa ya nafsi wa Kristu! Mapendo kamili, wasiyomwanzo na usiyomwisho, mwema kamili na usiyokiumba, nikusema Mungu anapenda kuishi ndani ya nafsi takatifu wa Kristu kupita mingi mbele ya mbingu na ndani ya kanisa moja.

Ewe Mungu mwema kamili na kujaza katika mapendo,
Muumba na Muyengazi wetu,
kuja kututembelea
ma nafsi yetu waliyejaza na bilonda,
ma nafsi waliyeumbwa toka Weye
katika mufano na mwenye sura yetu!

D.

Mukristu ya kweli ni sehemu ya Mwili ya Kristu ya siri, ya Mfalme wa wafalme na ya Bwana wa Wabwana. Katika sauti ya Mtume «kwa kuwa sisi ni viungo vya mwili wake» (Wa Efeso 5, 30).

Ma nafsi watakatifu wa Kristu! Munyanyueni juu pia richo yenu na muangalieni anaikaa wapi Kichwa yenu. Ni mu fasi ya kuume ya Mungu, kwa utukufu ya Baba Wake. Wa nani wanamsifu na wanamsujudu? Wa malaika, wa Malaika ya kwanza na yoyote Majeshi ya mbingu na dunia znima. «Kwa hivi Mungu vilevile alimutukuza sana, na kumupa jina lililo juu ya kila jina; hata kwa jina ya Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni na vya duniani, na chini ya dunia, na kila ulimi ukiri ya kuwa Yesu Kristu ni Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba». (WaFilipi 2, 9-11).

Na mweye muko ma sehemu ya Huyu Kichwa wa juu pia. Kichwa inatukuzwa? Na ma sehemu Yake wanashirika kwa utukufu Wake. Hii ni utukufu ya waminifu wa kweli; hii ni ufikisho ya utukufu na ustahili yao. Wa Kristiani weko ma sehemu ya Kichwa yenye utukufu kamili, ya Kristu!

E.

Nafsi ya mwaminifu ya kweli ikona ndowa na Bwana-Arusi wa mbingu, Yesu Kristu, sawa vile anatuwambia na Mutume: «kwa maana niliwapatanisha ninyi kwa mume mumoja, ili niletee Kristu bikira safi» (barua ya mbili kwa Wakorinto 11, 2). «Siri hii ni kubwa» (Kwa WaEfeso 5, 32). Mutukufu ni Bwana-Arusi? Eko pamoja na Bibi-Arusi kwa utukufu Wake. Ni nini kupita utukufu na ukubwa kama iko Kristu, Mwana wa Mungu pamoja na nafsi yetu? Ni ninyi kuliko mnene na usifiwa kama nafsi moja ya mwaminifu iko na ndowa na Yule Mwana wa Mungu, Yesu Kristu?

ST.

Mwaminifu ya kweli ni «muriti wa Mungu na muriti pamoja na Kristu» (WaRoma 8, 17). Ufalme wa mbinguni na bintu takatifu yoyote ni yake. «Jicho halikuona, wala sikio halikusikia,

wala hayakuingia katika moyo wa mutu, maneno Mungu aliyotengenezea wenye kumupende» (Barua ya mbili kwa Wa Korinto 2, 9).

Hii na ma jina ingine ya utukufu ni ma jina ya Mukristu ya kweli, wakati anabeba alama ya Roho Mtakatifu. Ee Ndugu wangu, unaona, basi, utukufu na sifa wa Kristu? Utukufu yote ya hii dunia ni kama buchafu na maiti mbele ya utukufu ya Mungu.

Basi, kikiri ya kama hakuna ingine kintu kuliko utukufu mbele ya mwaminifu moja ya kweli. Uwaza tena ya kama hii ufukisho na utukufu alitupatia Yesu Kristu, Mwana wa Mungu katika mateso na Lufu Yake.

Hii utukufu na sifa inaingia ndani yetu ao inatoka paka ndani ya hii dunia. Inakuja ndani yetu kwa imani na toba ukweli; na inatoka kama tunaishi bila imani na toba.

Ee weye ndugu, unayetafuta utukufu ya hii dunia ya bure na unajivuna na unasema ma sauti ya kujivuna kwa ajili ya utukufu ya kizazi yako, jina ukubwa yako na ma sifu ya jina yako! Pindula macho yako kwa utukufu na kizazi wa Kristu yako! Hii utukufu unapaswa kuitafuta juu ya kufanyika kweli mutukufu na mweshifiwa. Utukufu ya mwaminifu wa kweli ni kweli ya kama sasa hasionekane-paka kwa imani unaweza kuisikia kidogo- lakini itaangaziwa «kwa ufunuo wa wana wa Mungu»(Wa Roma 8, 19).

«Wapenzi», anasema Mutume, «sasa tuko wana wa Mungu wala haijaonekana bado tutakuwa namna gani; lakini tunajua wakati atakapoonekana tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo». (Barua ya Kwanza ya Yoane 3, 2). «Halafu wenye haki watangaa kama jua katika ufalme wa Baba yao» (Matayo 13, 43).

# SEHEMU YA TATU
# MASHINDANO WA ROHO

## Mbukomvi katikati mwili na roho

Kwa kila Mukristu tunaona mazalio wa mbili: Uzalio ya zamani na ya upya. Uzalio ya kwanza alibeba toka wazazi wake. Kwa hii uzalio anazaliwa katika makosa toka mama yake. Uzalio ya mbili anaifanya toka Kristu; kwa hivi anaitwa Mukristu, kwani kila mutu anayezaliwa anabeba na Jina ya Mkubwa yake. Kwa hii uzalio upya inaingia kwa uzima ya roho, takatifu na wa mbingu. Uzalio wa mwili ni paka mwili na uzalio wa roho ni paka roho. «Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa roho ni roho» (Yoane 3, 6).

Kwa sababu hii mazalio ya mbili ni katikati yao kupindua, kwa hivi tukona na mbukomvi na nvita katikati ya mwili na roho kwa kila mwaminifu; «Kwa sababu mwili unatamani ukishindana na Roho, na Roho anashindana na mwili» (Wa Galatia 5, 17).

Mwili inataka kuuwa roho, lakini na roho inataka kuuwa mwili.

Mwili anataka kushinda roho, na roho anataka kushinda mwili.

Mwili anataka kuishi juu ya roho na roho anataka kuwa juu ya mwili.

Mwili anataka kujivuna, kujipanda juu na kuwa ukubwa; lakini roho anataka kunyenyekevu.

Mwili yetu anataka kusirika, kuchukia, kukelele, kufanya matendo mbaya na kusema maneno mbaya; lakini roho anatakia kusamehe makosa yoyote na wema na upole.

Mwili yetu anataka kuishi na zambi, kufanya masharati, lakini roho anaizarau hii yote na anatakia utakaso na uzima ubikira.

Mwili anataka kuiba bintu ya watu wengine na kunyanganya na namna mengi; lakini roho anataka kusaidia na bintu yake.

Mwili anapenda matendo waovu, ma sauti waongo, matendo ya kulanda, mapendo kwa watu ya majivuno; lakini roho anakataa hii yote na anatakia sauti ukweli na upole.

Mwili anapendeza kuchukia watu wengine, lakini roho anawapenda wote.

Mwili anataka kuishi katika uzaifu na uvivu; lakini roho anazarau hii namna kimbaya na anatakia kuishi na muchoko ya matendo wa imani ya Kristu.

Mwili anataka machezo, malevi, machakula na ma furaha; lakini roho anataka kuishi na upole na kidogo chakula.

Mwili anatafuta kwa hii dunia utukufu na ma sifu na mali; lakini roho anawazarau hii yote na anapindula paka kutafuta bintu takatifu ya milele.

Vile mwili anafanya mbukomvi kupigana ya roho na roho kupigana ya mwili. Mukristu, kwani ni mtu mwenye kuzaliwa mara ya mbili katika Roho ya Mungu, anaishi hapana katika matakio ya mwili yake, lakini katika Roho na anashinda mwili yake kwa mamlaka ya roho katika shauria ya Mutume: «Basi ninasema: Kwendeni kwa Roho, wala hamutatimiza tamaa za mwili». (Wa Galatia 5, 16). Hii sauti ya Mtume inatuwambia kusulumbisha mwili pamoja na mawazo mabaya na tamaa mbaya»(Wa Galat. 5, 24) na tusifikili mahitaji ya mwili, kutimiza tamaa zake» (Wa Roma 13, 14). «Wapenzi, . . . mukatae tamaa za mwili zinazopigana na roho». (Barua ya kwanza ya Petro 2, 11); «Tutembee katika upya wa uzima vilevile» (Wa Roma 6, 4) Kwa mwili yetu tusiache zambi kutawala ndani ya miili yatu(Wa Roma 6, 12); paka tunapaswa kuishi paka katika Kristu aliyekufa na kufufuliwa kwa ajili yetu. (Barua ya mbili kwa Wakorinto. 5, 15).

Wa ndugu wangu, twende kuangalia maungo wetu: Tunaishi, basi, hii mbukomvi? Tunakombana hii sindano ya wokovu wetu? Tunatembea katika uzima upya? Tunakombana kupigana ma tamaa na matakio ya mwili yetu? Tunaacha kutawala yulu wetu na kuingia ndani kila zambi?

Wanafata Kristu paka wenye wanasulumbisha mwili yao pamoja na makosa na matakio na zambi yao. Kwa sababu faida gani unasikia kama unaitwa Mukristu, lakini usiwe? Mukristu wa kweli hana huyu anaye eko na hii jina, lakini sindano yake kupigana kwa mwili na kila zambi.

Tusipatie kwa mwili yetu kila kintu inayeomba. Inaomba mwili yetu chakula, maji, manguo, pumziko na bintu ingine ya lazima? Tutaipatia kila kintu iko na lazima kabisa. Lakini, kama inaomba kintu kimoja inaye iko kupigana ya mapenzi ya Mungu, tusiipatia hii kintu. Vile tutakuwa wa Kristiani hapana paka kwa jina, lakini kwa uzima na matendo yetu.

*****

Ee Mukristu kwa Ubatizo tunaingia kwa uzima moja takatifu na upya. Tunatosha kama nguo mbaya na wa zamani mtu yetu mbaya na tunavaa mtu mupya na wa roho. Tunakana mapendo kwa zambi ya mtu wa zamani na wa zambi na tunapokea mapendo kwa ma fazila ya Adamu mupya, ambaye eko Bwana Yesu Kristu. Vile tunafanyikwa, katika Mutume, kiumbe upya: « Hivi kama mutu akiwa ndani ya Kristu, yeye ni kiumbe kipya» (Barua ya mbili ya wa Korinto 5, 17).

Mbele ya Ubatizo yetu tulikuwa wafu kwa ajili ya zambi yetu, wasipo nguvu kutenda matendo mazuri, kwa sababu anaweza kufanya ninyi mtu moja mufu? Tuko mbele ya ma macho ya Mungu bila uzima, kwa sababu kwa Mungu anaishi paka yule mtu anayekufa kwa kila zambi. Lakini kwa Ubatizo takatifu tunazaliwa mara ya mbili katika neema takatifu, tunaacha zambi na tunafanyikwa wapya, wa nguvu kwa hii uzima takatifu na weshimiwa.

*****

Kutoka uzalio ya mwili inakuja majivuno, mawazo ya majivuno, hali kimbaya, uzarau kwa wakaribifu wetu. Lakini toka uzalio ya roho inazaliwa unyenyekevu, uzarau ya maungo yetu na uhukumu ya uzima na matendo yetu kwa ajili ya unyenyekevu.

Mu uzalio ya mwili inazaliwa usiyeimani, lakini kwa uzalio ya roho inazaliwa imani.

Kwa uzalio ya mwili inatoka usiyeboka ya Mungu, lakini kwa uzima ya roho boka ya Mungu. Kwa uzalio ya mwili inakuja uzima bila kutii kwa mapenzi ya Mungu, lakini kwa uzalio ya roho inazaliwa utii, wema na upole.

Kwa uzalio ya mwili hakuna shukrani kwa Mungu na mukaribifu wetu, lakini kwa uzalio ya roho ni shukrani kwa Mungu. Kwa uzalio ya mwili hakuna sifa na utukufu kwa Mungu; kwa uzalio ya roho ni usubuko na mafa ya wa ndugu wetu. Kwa uzalio ya mwili ni imani kwa maungo na ma nguvu wetu, lakini kwa uzalio ya roho tukona kitumaini mingi paka kwa Mungu na hapana kwa mali, ma sifa na mamlaka wetu.

Kwa uzalio ya mwili inazaliwa hasira, kisilani, umbaya na chuki, lakini kwa uzima ya roho inakuja upole, uzima bila hali mbaya na uvumilia kwa makosa ya wa ndugu wetu. Kwa uzima ya mwili tukona mapendo kwa maungo wetu, lakini kwa uzima ya roho inazaliwa ndani yetu mapendo ya Mungu na upenda-wanadamu na kwa wa ndugu wetu. Kwa uzalio ya mwili inazaliwa upenda-feza, choyo na hakuna mapendo ya watu wengine, lakini kwa uzima ya roho inakuja mapendo ya watu wote, wema na saidio kwa wakaribifu wetu.

Mu uzima ya mwili ni tamaa na matendo mbaya ingine yake, lakini kwa uzima ya roho ni mapendo na wema kwa taabu na furaha ya ndugu wetu. Mu uzima ya mwili inazaliwa kazi ya kuiba na kunyanganya na kuzulumu, lakini mu uzima ya roho iko uzima wa haki. Mu uzima ya hii dunia ni mapendo ya hii dunia, matakio ya mwili, matakio ya sifa na matukufu na hekima ya hii dunia; lakini uzima ya roho inazarau dunia na yoyote matendo ya bure yake na anatafuta kufamia ma hekima ya mbingu na wema ya milele. Juu ya kusema na sauti moja: Mu uzalio ya mwili inatembea pamoja mapendo ya kila kazi kibaya; lakini mu uzalio ya roho inatembea pamoja kila kintu kizuri. Basi, tazama, ma nani ni matunda ya uzalio katika mwili na katika roho. Madiko Takatifu wakati inatushauria kuepuka ya zambi, inatushauria kutoka ya ma tunda ya uzalio wa

zambi. Na, wakati inatufundisha kufanya kazi kizuri, inatufundisha kuonyesha matunda ya uzalio upya; «Uache mabaya ukatende mema; tafuta salama, na kuifata» (Zaburi 34, 14). Tena «Kila mutu anayetaja jina la Bwana aache uovu» (Barua ya mbili kwa Timotheo 2, 19).

Wa ndugu wapenzi wangu, utukufu kwa Mungu, kwani tulizaliwa na tulipata uzima upya kwa Ubatizo takatifu ya Kanisa yetu Orthodokse. Lakini tukona matunda ya hii uzima upya? Tunaishi katika amri ya hii uzima upya?

Uzalio haina kintu fulani ya kufa, lakini ni kintu ya nzima; basi inapaswa kuzala na matunda ya nzima. Basi, na sisi tunapaswa kuonyesha ma tunda wastahili kwa uzalio yetu ya upya juu tusionekana mbele ya Bwana wetu wasipo matunda na kusikia neno yake wa matata: «Siwajui ninyi» (matayo 25, 12).

## Uhukumu ya maungo wetu

Utukufu kwa Mungu! Sisi wote tunaitwa wa kristiani; wote tunasadiki kwa Mungu ya Utatu Mtakatifu, Mungu mwene mzima na musiyekufa; wote sisi tulibatizwa kwa Jina ya Utatu Mutakatifu mwenye asili moja ya Baba na ya Mwana na ya Roho Mtakatifu; sisi wote tunasadiki kwa Mwenye sulubiwa Yesu Kristu, Mwana wa Mungu na mukukikiri hii imani yetu, tunafanya pa maungo wetu alama Yake, alama ya Musalaba; sisi wote tunaenda mu Kanisa na tunaomba Kwake, tunamuimbia, tunamutukuza Mungu wetu; sisi wote tunapumunika Mwili na Damu ya Kristu, sisi wote tuko kwa mwito ya uzima ya milele na ufalme ya wa mbinguni, sawa vile tunakikiri na kwa Simvolo ya Imani yetu: «Natumaini Ufufuo wa wafu na uzima wa milele mbele utakayokuja».

Utukufu kwa Mungu juu ya yoyote hii matendo yake! Ma Fumbu ya Kristianisme ni watukufu kabisa na wa ajabu kamili, wa ndugu wangu! Kama sisi tuko wa Kristiani ni jabo ukubwa na weshimiwa kabisa! Basi, inapaswa kuangalia na kupima maungo yetu, kama tuko wa Kristiani wa kweli. Mutume Paulo anatuwambia sisi kuangalia maungo yetu kama tuko kwa imani, kwa sababu bila imani hasiweze hata Mukristu moja kuwa mwaminifu ya kweli (Ona Barua ya mbili kwa WaKorinto 13, 5).

Tukona maonyesho ya uzima yetu wa Kristu, ili tuliandika yulu, lakini tukona kweli ndani yetu Kristanisme ya kweli? Hii matendo yoyote ya inje hana na mamlaka bila matendo mazuri ya ndani. Na matendo ya inje bila ma alama ya kweli, bila sauti ukweli na wongo na udanganyifu.

Sisi wote tunatukuza kwa sababu tunasadiki Kristu. Lakini tunatenda matendo ma stahili kwa imani yetu, sawa vile anatuwaambia Mutume: «Unionyesha imani yako ya matendo yako» (Yakobo 2, 18). Tunaitwa wa Kristiani toka Jina ya Kristu. Lakini tulisulubisha mwili yetu na makosa na matakio yetu, sawa vile iko kweli kwa Mukristu moja, anayesadiki kwa Kristu, sawa vile anatuwambia na Mutume? «Nao walio watu wa Kristu waamesulibisha mwili pamoja na mawazo mabaya na tamaa mbaya» (Wa Galatia 5, 24).

Tunasadiki kwa Evangelio. Lakini tunaishi katika amri ya Evangelio? Tunatukuza Mungu mwenye kweli na tunamuita kwa sala yetu. Lakini tunamushukuru na imani na moyo yetu usafi, kwani Huyu anaomba moyo yetu usafi? Tunasikia Neno ya Mungu. Lakini tunamuweka ndani ya roho yetu na tunatengeneza na uzima yetu kufata hii ma amri yake? Tunapewa Mwili na Damu Yake, lakini tunazaliwa toka hii Komonyo Takatifu na tunapanda kwa uzima ya roho yetu?

Hii yote na ingine tunapaswa kuangalia na kuuliza sisi moyo yetu. Tuendelea kuangalia namna gani tunaishi, namna gani tunatembea, namna gani tunawaza, namna gani tunasuburia, namna gani tunatumika, ni nani roho yetu mbele ya Mungu mwenye kuona yoyote matendo yetu na ni ninyi hali ya uzima yetu mbele ya wakaribifu wetu.

Kisha kila uhukumu na maangalio sisi inapaswa kukombana juu ya kuangalia yulu mu uzima ya roho; na paka vile tutaishi hapana kwa jina, lakini na kwa uzima na matendo yetu wa Kristiani ya kweli.

## Maangalio ya ndani

Usisopoke kintu ingine kuliko mingi paka kabisa matengenezo ya hali ya roho yako na ongezo ya mapenzi yako. Nguvu ya imani ya Kristu inanioloka kwa hii makangamano.

Kila kintu ya inje, bila tunda ya ndani yetu, haina hata mamlaka moja. Kama hakuna kintu ndani ya roho yetu, kwa tendo yetu ya inje ni ya bure. Fazila yetu haina ya kweli, kama hasitoke ya roho yetu. Safisha roho yako na hali ya moyo yako na utakuwa mufazili. Paka hivi na matendo yako ya inje itakuwa takatifu. Hali ya ndani yetu ni mwanzo ya ile ya inje.

Wakati ndani ya roho hakuna kintu kimbaya, hata hasionekana inje. Mikono awatafanya kazi kimbaya, miguu awataenda mu kazi kimbaya, ulimi na ma midomo awataseme ma neno mbaya, masikio awatasikie ma tangazo na ma sauti mbaya, ma macho awataone kintu moja kimbaya. Kwa sababu mapenzi na roho wanakataa njia kimbaya.

Toka chemchem moja inatelemusha maji safi, kama na chemchem ni usafi. Kwa hivi itatoka ya roho matendo mazuri, kama na hii roho ni usafi. Kupindua, bila roho ufazili hakuna namna kufanya matendo mazuri, sawa vile toka chemchem moja ya uchafu hakuna namna kutoka maji usafi, lakini maji uchafu na yenye sumu.

Basi, safisha roho yako na akili yako na utakuwa Mukristu ya kweli; utafanyika kiumbe upya, kwani kila mtu ni muzuri ao mbaya katika usimamizi ya moyo na roho yake. Roho moja ni njema kama inatii na inafata mapenzi ya Mungu. Roho kimbaya ni kama inasimama kupigana kwa mapenzi ya Mungu na inakataa kuifata.

Mama ya akili nzuri na roho ya kunioloka ni imani, sawa vile anatuwambia na Mt. Amvrosios. Basi, pahali fasi inalofa roho nzuri, pale hakuna na imani nguvu.

Kwa hivi, ndugu wangu, kombana kutengeneza mtu yako yenye ndani yako na hivi utakuwa kweli mufazili. Kama usifanye hivi utabakia daima bila matunda ya roho. Hivi utaweza kusikia ya kama imani anazaa mtu mara ya mbili na ni shina ya kila kazi nzuri.

Usiweze kusaidia maungo yako, kama usikombana kutafuta kila matakio na zambi inayefichamwa ndani ya roho yako na ili inakuleta uharibifu ya roho. Bila ufamio ugonjwa inabakia ndani bila kutunzwa.

Mwanzo ya uzima katika Kristu ni ufamio ya matendo mbaya yetu na hali ya moyo yetu. kama mtu moja alitafuta na alisadiki ya kama ni mugonjwa, kisha atakataa kuomba uponyesho? Na nani, kama alifamia mateso yake kwa ajili ya zambi yake, kisha atakataa kukombana juu ya kuponyeshwa?

Angalia na tafuta na weye hii hali mbaya iko ndani ya roho yako na kombana kuokolewa. Matakio mbaya wanafuchama ndani yetu ni kwa mufano majivuno ya akili, imani kwa maungo na nguvu yetu, tamaa, chuki, upenda-feza, uchafu na kila zambi ya mwili. Kutoka hii makosa na mazambi inatoka kama maji ma zambi ingine ya kuachana. Basi, kama unaangalia ma siku yote ndani ya roho yako, pole-pole utatafuta matakio na makosa yako yote.

Ugonjwa moja inayesiponyeshwa inaleta lufu. Moyo mbaya inayembakia hivi iko namna kuleta lufu ya milele. Ufamio ya zambi yetu ndani inafata na ufamio na uzima maskini katika roho. Hii ufamio inafata boka juu ya uzima ya milele, unyenyekevu, ombolezo, matakio na makangamano kurudia toka hii njia ya uharibifu.

Mungu anapatia neema kwa wenye unyenyekevu, inayetengeneza na inazala na uzalio upya. Kama mtu atafamia maungo yake na anaanza kuitengeneza, bio-bio moyo yake itatembea ku mbele. Basi, famia maungo yako na utaitengeneza katika Kristu.

Inafuchamwa ninyi ndani ya roho ya mtu moja, hii inafunuwa na mateso na masikitiko ya kila siku yake. Mateso inafanana na moja ndawa ya kutapika. Ni ninyi ndani ya tumbo inaonekana na moja kutapika; ni ninyi ndani ya mutu moja inaonekana mateso na masikitiko ya ma siku yake.

Neno takatifu ya Mungu na ma Kitabu ingine ya Kristu wanatuonekana uzima yetu ya kuharabika. Lakini kwa majaribu na mateso sisi tunasikia hali ya uzima yetu mara moja.

Upenda ya utukufu inafunuwa kwa upotevu ya hii utukufu, upenda ya feza inaonekana kwa upotevu ya hii mali, tamaa inaonekana kwa utajira ya mukaribifu yetu na hasira kwa shauria.

Basi, kama unakutana, ee Mukristu wangu, majaribu na mateso, uwaza ya kama Mungu iko namna kupatia baraka Yake juu ya kupata weye faida mnene ya roho, kwa sababu hivi utafunda inafuchamwa ninyi ndani ya roho yako, na vile utaanza kutengeneza kukiko nzuri roho yako.

## Zambi

Hakuna namna kuria mtu moja, ya mingi hii uharibifu na laana iliyefamia kizazi ya ubinadamu, kisha kosa ya wa babu ya kwanza Adamu na Eva.

Hakuna kintu ingine kuliko mbaya kwa mtu ya zambi, lakini na hakuna kintu ingine ya kumukokota sawa zambi. Minasema ya huyu mtu, kiumbe ya Mungu aliyejivaa kama nguo nuru ya Mungu. Huyu mtu aliyeumbwa katika mufano ya Mungu na katika sura Yake.

Ee wandugu wangu, ngapi kabisa chini adui yetu shetani alitutupa sumu yake ndani yetu! Ngapi uharibifu alileta yule nyoka (shetani) na sumu yake wa lufu kwa kizazi yetu iliyekuwa usafi na wasiyouharibifu! Tangu ile wakati kila mutu inatelemuka bila kizimbirio kwa kila zambi. Nabii Daudi anaria juu ya hii laana na uharibifi na anaandika: «lakini mutu hadumu katika heshima; yeye ni kama nyama wanaopotea» (Zaburi 49, 12). Nikusema ma zambi inajionekana ma nyama, sasa wanaonekana na kwa watu.

Nyama moja inasirika na inakuwa makari? Vile tunaona na kwa mtu moja; na huyu anasirika na eko na makari kama nyama. Nyama moja ekona tamaa? Na mutu eko na tamaa. Ma nyama katikati yao wananyanganya moja mwingine? Vile anafanya na mtu mbele ya ndugu yake. Anaiba nyama moja? Na mtu anaiba. Anakula mingi nyama moja? Vile anakula na mtu. Nyama iko na matakio mbaya ya mwili? Na mutu anamufanana. Tena mambo ya matata kabisa ni hii: Hii matakio mbaya unapata kwa kila nyama, yoyote matakio unapata paka kwa mtu moja. Nikusema Mutu moja eko na pamoja hii matakio: Eko na majivuno, anafokea, anasirika, eko na uwazo mbaya, ekona tamaa, anapenda kufanya zambi ya mwili kama iko namna na kila siku, anakula kuliko mingi ya nyama moja, anaomba kuiba bintu ya watu wageni. Hii matakio mbaya na ingine mengi eko nayo.

Ewe Kiumbe upendwa ya Mungu, ilifanyikwa ninyi roho yako usafi, hii mufano ya Mungu na Sura yako katika Mungu? Iko wapi ubikira na utakaso na moyo yako kweli? «lakini mutu hadumu katika heshima; yeye ni kama nyama wanaopotea» (Zaburi 49, 12).

Mtume Paulo anatuelejea namna gani wanaishi wale watu wenye bado kuzaliwa katika neema ya Kristu: «Hakuna mwenye haki, hata mumoja. Hakuna mwenye kufahamu, hakuna mwenye kutafuta Mungu. Wote wametoka kwa njia, wote waaamekuwa pasipo faida; hakuna mwenye kufanya mema, hata mumoja. Koo lao ni kaburi wazi; kwa ndimi zao, wamedanganya; Sumu ya nyoka ni chini ya midomo yao. Vinywa vyao vimejaa laana na uchungu: Miguu yao ina mbio kumwanga damu. Kuharibu na taabu ni katika njia zao; na njia ya salama hawakuijua. Hakuna woga wa Mungu mbele ya macho yao» (Wa Roma 3, 10-18).

A.

Kwa ajili ya zambi sisi tunaleta haya na kisilani kwa Mungu Mkubwa yetu. Yule aliyetuumba toka zero katika mufano na Sura yake; mwenye kwa ajili ya sisi wenye zambi alituma mu dunia Mwana wake wa pekee; Yule ambaye kila siku na saa anatupatia ma zawadi Yake, anatupatia chakula, anatupatia maji, anatuvaa, anatupumzika na anatufanyisia watajiri; Yule ku mwisho atahukumu kila mwenye zambi juu ya zambi yake mbele ya dunia nzima. O, kweli zambi ni moja kintu kimbaya kabisa, kwa sababu kwa ajili yake sisi tunaleta haya kwa Mungu Mkubwa yetu na matendo Yake!

B.

Hata mtu moja hasiweze kutosha mtu mwingine toka hatari ya zambi, paka Mwana wa Mungu. Huyu alikuja mu dunia kwa maondoleo ya zambi yetu; alikuja, aliteswa na alifariki juu ya kuzimisha zambi. «Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alionekana, ili avunje kazi za Shetani» (barua ya kwanza ya Yonae 3, 8). «Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu anayechukua zambi ya ulimwengu» (Yoane a, 29). Utukufu kwa upenda-wanadamu Wake.

G.

Zambi inazala lufu; « Kwa maana mushahara wa zambi ni mauti» (Wa Roma 6, 23). Hivi wa Babu wetu kwa sababu walikosana ndani ya Paradizo, walipata lufu. Ilikuwa namna kubakia daima ndani ya lufu na mbali ya Mungu, kama hasikukuje Kristu, mwana wa Mungu juu ya kuwapatia uzima upya ya kumwangisha Damu Yake.

Lakini « Yesu Kristu ni sawasawa jana, leo na hata milele» ( Wa Ebrania 13, 8). Basi Damu Yake takatifu ilimwangishwa mu dunia nzima, leo na jana na anazala ya roho kila mwenye zambi, anayedantiki kwake.

D.

Kila zambi inayefanya mtu moja anapokea uhukumu ya moyo yake inayemuteswa bila rehema kila siku. Tena mara ingine huyu mtu mwenye zambi anatundikwa kwa sababu hasiweze kuvumilia uhukumu ya moyo yake.

E.

Kwa ajili ya zambi yetu wanakuja kwa sisi malipizo ya wakati kidogo, sawa vile njaa, moto ya kulungua, ma nvita, malari na magonjwa ingine ya kuachana, matetemeko na mateso ingine. Mtakatifu Yoane Krisostomo anatuwambia ya kama «maneno ya matendo mbaya yoyote ni zambi yetu».

*********

Munaona kintu kimbaya ngapi ni zambi? Ni kazi kimbaya kuliko mbaya ya kazi ingine. Ee ndugu wangu, ni kweli ya kama iko kupita nzuri kutembea bunji bila mavazi na hapana kufanya zambi. Ni kuliko nzuri kuwa mufungwa mu buloko na mutumwa na hapana kufanya zambi. Ni kupita nzuri kuwa mugonjwa na mwenye kilonda na hapana kufanya zambi. Ni kuliko nzuri kuikaa ndani ya giza na hapana kufanya zambi. Ni kuliko nzuri kuvumilia matusi, machokozo, maneno ya haya, ma kofi na bilonda na hapana kufanya zambi. Ku mwisho ni kupita nzuri kuvumilia kila kazi kimbaya ndani ya hii dunia na hapana kukosa mbele ya Mungu! Kwa sababu hii yote mateso wanatesa ya wakati kidogo, kwani lufu italeta mwisho ya matendo mbaya yote, ili tunateswa; hapa itaisha kila uharibifu. Lakini zambi inatesa na itaendelesha kuteswa kwa milele mwili na nafsi yetu.

Tulisema ku mbele ya kama zambi ni maneno ya matendo yoyote wanayefanya watu ya hii dunia. Nikusema kama hasikukuje zambi, hasitakukuje taabu na muchoko. Aliingia ndani ya dunia zambi na waliifata mateso mengi. Matunda ya zambi, basi, ni machungu, lakini hii zambi inaonekana inje kama tunda utamu. Lakini mbego buchungu itazala matunda ya buchungu. Kwa hivi inapaswa kuepuka mbali ya kila zambi yetu. Unajua ya kama sumu inaleta hatari kwa watu na inapaswa hawa kuiepuka na kuitupa; unajua ya kama nyoka inauwa watu na hawa wanasopoka kwa mwendo yao; unajua ya kama wanyanganyi wanaiba na wanauwa na weye unasopoka. Lakini zambi inaharabika kuliko mingi ya kila sumu; ni kona sumu kupita mingi ya kila nyoka; inaharabika kuliko mingi ya kila munyanganyi. Zambi inatutosha ya yoyote matendo mazuri ya hii na ingine uzima ya milele, kwani inauwa nafsi na mwili yetu. Hii ni matunda ya hii mbego buchungu ya zambi.

Uwaza ya kama ni kuliko mbaya zambi moja ya moja shetani. Kwa sababu na huyu shetani zambi ilimufanyisia shetani. Yeye ya kwanza alikuwa malaika mwenye mwangaza na mwema; lakini kisha aliharabika toka zambi na alitupa ndani ya giza.

Huyu mtu ambaye hasifamia sasa ya kama zambi ni kazi kuliko mbaya ya kila kazi ingine na hasikombane kuchunga maungo yake, huyu mutu atapima bucgungu ya zambi kwa uzima ya milele na ile wakati atasikia kazi ya zambi ngapi ni kimbaya, lakini itakuwa ya kuchelewa sana! . . . Kwa hivi inapaswa tangu sasa kufamia giza ya zambi na kutoka ya matendo mbaya yake.

Ee Kristu, nuru mwenye kweli, unayeangazia vipofu, angaza na ma macho ya roho yangu juu ya kusikia zambi na kuepuka mbali yake! Kwani mwanzo ya wokovu yangu ni ufamio ya makosa yangu.

## Maneno ya zambi

Huyu mutu anayetaka kuwa Mukristu ya kweli na kupata wokovu ya milele na saidio ya Bwana Yesu, inapaswa vila shaka kuonyesha mapendo juu ya kusindana kupigana kwa kila zambi na hapana kupatia nguvu kwa zambi juu yake: «Basi, musiache zambi kutawala ndani ya miili yenu ya kufa, hata mutii tamaa zake; » (Wa Roma 6, 12), anatuwambia Mutume Paulo kwa wakristiani, kwa sababu hii inaomba imani yao. «Nmi nitakuonyesha imani yangu kwa njia ya matendo yangu» (Yakobo, 2, 18), anatuwambia Mutume Yakobo.

Ee Ndugu wangu, uwaza: Mukristu anafamiwa hapana kwa ajili ya ma sauti; : «Ee Bwana, Bwana», lakini kwa ajili ya sindano yake kupindua ya kila uso ya zambi. Askari ya kweli ni huyu askari anayekamata fasi na anakombana adui yake; na huyu Mukristu ambaye alianza nvita bila masikilizano kupigana ya zambi yeye ni askari ya kweli ya Kristu.

Sasa tutatafuta kujua maneno nani kila mtu anafanya zambi na hivi, ninawaza, tutasaidia sindano yetu kupigana ya kila zambi. Sasa tutaandika maneno ya tano:

A.

Uharibifu ya uzima ubinadamu.

Mutu anazaliwa katika zambi, sawa vile anasema na Nabii Dauti: «Tazama, niliumbwa katika hali ya uovu; na katika makosa mama yangu alinichukua mimba». (Zaburi 51, 5). Ma zoezo mbaya inayeleta pamoja naye kila mutu, wanamukokota mu zambi. «Ole wangu mimi mutu wa taabu! Nani atayeniokoa na mwili huu wa kufa? « (Wa Roma 7, 24).

Uharibifu na taabu ya mtu walianza na kosa ya Adamu. Tangu ile wakati kila mtu anafata zambi. Watoto wanazaliwa ya kufanana na wazazi wao: «Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho» (Yoane 3, 6).

Lakini Mukristu na saidio ya Ubatizo Takatifu anapaswa katika malako yako ya zamani ya Hii Fumbo kukombana kupigana matakio na zambi yake; aipaswe kuacha hii matakio kumuharabisha hali ya roho yake.

B.

Shetani anakokota mtu mu zambi. Mutume Petro anashauria Waminifu wote kuchunga nzuri toka nguvu ya shetani: «Muwe na kiasi na kuangalia; adui yenu shetani, kama simba ya kunguruma anazungukuzunguka akitafuta mutu amumeze. Nanyi mushindane naye katika imani yenu, mukijua ya kuwa mateso yale yanatimizwa kwa ndugu zenu walio duniani» (barua ya kwanza ya Petro 5, 8-9). Na Mtume Paulo anaongezeka hivi: «Basi kwa kumaliza, muzidi kuwa hodari katika Bwana, na katika uwezo wa nguvu zake. Vaeni silaha zote za Mungu, mupate kuweza kusimama juu ya hila za Shetani. Kwa maana kushindana kwetu si juu ya damu na nyama, lakini juu ya falme na mamlaka, juu ya watawala wa ulimwengu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo mabaya katika pahali pa mbingu». (Kwa wa Efeso 6, 10-12).

Hawa wa adui wasipoonekana wanasindana kwa uharibifu wetu na wanakombana kututupa mu zambi. na sisi basi, aipaswe kulala.

G.

Majaribu ya dunia wanatusukuma mu zambi.

Kila zambi iko na zambalishwa ma fasi yote kabisa. Mtu moja anafanya hii zambi; mwingine anaiona hii kazi yake ao anaisikia na anaifata bila kuwaza. Hii ma kwazo wanafanana kama moja ugonjwa inayezambalishwa bio ma fasi ingine: Anakamata hii malari mtu moja bio, anakamata na mwingine. «Ole wa dunia kwa sababu ya mambo ya kukosesha! kwa maana sharti mambo yaha yafike; lakini ole wa mutu yule anayeyaleta! » (Matayo 18, 7).

D.

Mwanzo ya zambi inaanza kwa ajili ya fundisho mbaya ya watoto wetu. Hawa watoto, wenye awakupate ma shauria na mafundisho nzuri, wakati watakomea wanaingia ndani ya kiwanja ya zambi na matendo mbaya. Wazazi wekona jukumu mnene kwa sababu awakusopoke nzuri watoto wao. Na mweye wa mama na wa baba musikieni hii mambo! . . .

E.

Inasukumu mu zambi tena na zwezo mbaya.

Hii mambo tunaiona na sisi kila siku. Wenye watu wanakunywa vinyo na ingine kila siku wanapenda kulewa; wenye wanaiba hawaweze kusimama hii kazi mbaya yao ya kuiba, wenye zambi ya mwili wanapenda kufanya hii zambi kila siku na hivi wote wenye zambi wanapenda kufata zwezo mbaya yao kama iko na namna na kila siku. Nikusema zwezo inawakokota kama kamba na inawatupa mu zambi. Sawa vile huyu mwenye njaa anaomba mukate na mwenye kunywa anaomba maji vile na wale watu wanapenda kutelemuka mu zambi yao.

Ninawaza hii ni maneno ya tano kwa ajili yao kila mtu anapenda kukosa mbele ya Mungu na zambi yake. Lakini weye, ndugu wangu, unayependa kuokolewa na kuonyesha imani yako mu uzima yako, sindana kila siku bila usimamisho kupingana ya kila zambi. Hii yote maneno, sababu na nyakati ya zambi ni wa adui wasiyo mapendo ya wokovu yako: Mwili kama nyama makari anataka kwa matakio na zambi mbaya kusimama juu ya roho yako. Shetani adui yako, ambaye anachukia wokovu yako hasisimame kuuzi na kukombana mu uzima yako kila siku na usiku. Majaribu ya dunia wanavimba na wanakomea matakio mbaya ya mwili yako kila siku, sawa vile pepo inavimba moto. Lakini mambo ya sikitiko ni hii: Kwa yule mtu alizombelea kazi moja kimbaya, yeye hasiweze kusimamisha hii matakio yake, kiwa sababu ndani yake inazala sawa moja nguvu ya mbili kwa mwili yake.

## Sindano kupingana ya zambi

Ninaichika ya kama sindano kupingana ya zambi ni nguvu sana; lakini ni lazima kabisa. Watu mengi wanakombana na wanashinda ma taifa wengine; lakini hawa ni watumwa na watumishi kwa matakio na zambi yao. Hakuna ushindi kuliko utukufu toka hii ushindi ya maungo yetu. Taji na utukufu bila ushindi hakuna. Ushindi vila sindano kupingana ya adui hakuna.

Ndugu wangu, twende kuanza hii sindano juu ya kupata na saidio ya Kristu ushindi ya utukufu na tutakamata toka Huyu Mungu taji ya fazila na tutatukuzwa kwa milele ndani ya Ufalme wake. Sasa twende kuandika mawazo filani juu ya kupata nguvu kwa hii sindano yetu:

A.

Unasikia na kombana kusikia na akili yako neno ya Mungu. Ndani ya hii fundisho ya Mungu tunafamia sisi zambi na fazila; paka vile tutaepuka zambi na tutafata fazila ya Mungu: «Kila andiko limepewa kwa maongozi ya Mungu, na linafaa kwa mafundisho, na kwa kuonya watu juu ya makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa mafundisho katika haki; ili mutu wa Mungu awe mukamilifu, ametengenezwa kabisa kwa kila tendo jema». (Barua ya mbili ya Timoteo 3, 16-17). Neno ya Mungu ni kisu ya Roho (Wa Efeso 6, 17), na kwa hii kisu tunakata adui yetu, adui ya nafsi yetu.

B.

Mungu eko ma fasi yote. Pahali fasi sisi tuko Yeye ni karibu yetu. Kila kazi sisi tunafanya, tunaifanya mbele ya ma Macho Takatifu yake. Basi, namna gani tutafanya zambi na tutakanyanga mapenzi Yake takatifu mbele ya ma Macho yake?

Unasikia haya na unaogopa kusimama na kibego mbele ya mfalme wa inchi ao mbele ya musaidizi yake. Lakini haya na heshima ngapi mingi inapaswa kuonyesha kama unasimama mbele ya Mungu? Usisahabu ya kama kila zambi ni kibego na uzulumu mbele Yake.

G.

Kumbuka tena na ma siku ya mwisho yako, lufu, Uhukumu ya Kristu, Hadeze, ufalme wa mbinguni. Hii makumbusho itakusaidia kutoka mbali ya zambi yako. Madiko takatifu inatushauria ya kama kwa kila neno yako kumbuka ma siku yako ya mwisho na usitafanye zambi.

D.

Epuka mbali ya ma zwezo ile wanakukokota mu zambi sawa kwa mufano machezo, mazungumuzo mbaya, sawa vile hivi anatushauria na Mtume paulo: «Musidanganyike: mazungumuzo mabaya yanaharibu adabu». (Barua ya kwanza kwa wa Korinto 15, 33).

E.

Kamata ndani ya uwazo na akili yako ya kama iko namna akufe mtu kwa hii saa ya zambi yake na hivi atapotea ya milele. Faraoni, mfalme ya Misiri, alifukuza taifa ya wa Yuda na alitaka kuwarudisha mukongo mu ufalme wake; lakini wakati aliwafukuza, alifariki ( Angalia Kitabu ya Biblia Kutoka 14, 27-28). Na Abusaloma, mwana wa Daudi, alitaka kuuwa baba mtakatifu yake na alikufa kwa hii kazi kibaya yake (Wa Samweli ya mbili 18, 14).

Vile inafanyikwa na sasa: Tunaona ya kama wenye wapotevu na wenye zambi ya mwili wanajipika ya lufu mara mingi ile wakati wanafanya tendo yao kibaya, wenye chabulana wanakufa wakati wanachabula Mungu ao wa ndugu wao, wenye wa mwivi mu kazi yao ya kuiba na hivi wanakufa mengi. Nikusema uhukumu wa haki ya Mungu anapika hawa wenye zambi juu ya kuogopa na sisi na tusifanye zambi mara ingine.

ST.

Uwaza ya kama Kristu, mwana wa Mungu, aliteswa na alifariki kwa ajili ya zambi yako. «lakini aliumizwa kwa makosa yetu, alichubuka kwa maovu yetu. Azabu ya salama yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona» (Isaya 53, 5). Na weye, ee Mukristu, unapenda kufanya hii kazi, nikusema kumusulumbia Kristu ambaye alikunywa kilauri uchungu ya mateso yake? (Angalia na wa Ebrania 6, 6).

Z.

Tusiangalie watu wengine wanafanya ninyi, lakini Neno ya Mungu inatufundisha ninyi. Vile hakuna namna kufata sisi majaribu ya hii dunia. «Salama kubwa ni yao wanaopenda sheria yako; nao hawana njia ya kukwaa» (Zaburi 119, 165). Penda sheria ya Mungu, ee Mukristu, na hawataweze kuharabisha majaribu ya hii dunia.

H.

Makangamano na ma sindano yetu kupingana ya zambi hakuna namna kutuletea matunda bila kuomba na sisi saidio ya Mungu. Basi, ni lazima kuunganish sindano na sala juu ya kutusaidia Bwana kwa hii mambo nguvu sana. Mungu anasaidia wenye kumupenda na wanasindana bila uzaifu na ku mwisho anawapatia taji ya uzima ya milele.

Ee Ndugu wangu! Unaona wa adui ya ma nafsi yetu, wenye wanataka kutuharabisha hapana ya wakati kidogo, lakini kwa milele. Unaona na saidio ya Mungu kwa hii sindano yatu kupingana kwao. Basi, twende kukombana, twende kukamata fasi ya sindano na kubeba silaha na nguvu ya Yesu Kristu Mwenyezi. Tutakamata naziri ya kama tutawafukuza daima na tutawatupa inje ya uzima yetu. Paka vile tutabeba taji toka mikono ya Bwana Yesu.

Ee Bwana Yesu, mushindi ya mauti na Hadeze, utusaidie; bila Kwako tusiweze kufanya kintu, lakini pamoja na Weye tutafanya yoyote. Amina!

## Majivuno

Zambi ya majivuni ni kibaya kabisa. Lakini sisi tunaifamia kidogo, kwa sababu inafuchama ndani chini ya ma roho yetu. Shina ya majivuno ni kama sisi hatujue maungo yetu. Hii giza inayeiko ndani yetu inafunga macho ya roho ya mtu na hivi yeye anajivuna.

Kama, iko namna mtu kufamia maungo na moyo yake, ilikuwa namna kufamia maskini ya roho yake, ya kama ni kintu moja ya bure, ya kama ni mtu mupotevu na mwenye zambi na kisha hasitapende kujivuna! Mutu ni mubaya sana, kwa sababu hasione na hasipokelee ya kama ni mtu

mwenye zambi na ya bure mbele ya Mungu. Majivuno inaonekana kabisa katikati ya matendo yetu, sawa vile muti moja inaonekana toka matunda yake. Lakini ma nani matunda ya hii mbego buchungu ineyeitwa majivuno?

1.

Mutu mwenye majivuno anaomba na namna mengi ma sifu na matukufu na ma sauti ya utamu kwa maungo yake. Anataka daima kuonekana ya kama ni kintu kinene. Anataka kuangalia na kuhamuru watu wengine na kama mtu mwingine atakataa kumutii na kusimama mbele ya mapenzi yake, huyu anasirika na anakuwa makari sana.

2.

Kama atapotea sifa na mamlaka, anasimanga, anasirika na anasema ma sauti mbaya: Fasi wapi mimi nilikosa? Namna gani mimi ni mukosefu? Hii malipo mimi nikona stahili kubeba? Na mara ingine huyu mtu anafika mpaka kuandikwa na kuuwa maungo yake.

3.

Huyu mtu mwenye majivuno anaanza matendo yulu ya ma nguvu yake, lakini hasiweze kufika ku mwisho. Ee Mutu mumbafu, juu ya ninyi unakaribia hii uzito ile usiweze kuipanda yulu yako?

4.

Anapenda kuingia katikati ya ma mambo ya watu wengine. Anataka kuangalia mambo yoyote na watu wote, bila kujua anafanya ninyi. Hivi mingi inamufanyisia kipofu zambi ya majivuno.

5.

Anatukuza na anapanda na ma sauti yake maungo yake, bila haya: Na anasema hivi: Mimi nilifanya hii tendo. Nilitoa mu ushirika ayetu hii na hii filani matumishi na ma kazi mazuri na mengi». Ee mtu, unabalula ma kazi yako, lakini juu ya ninyi usiseme na zambi yako? Kama unasikia haya kuonyesha na zambi yako, inapaswa kusikia haya, kama unasema matendo yako.

6.

Huyu mtu anazarau na ananyenyekevu watu wengine. Vile anasema: «Huyu mtu ni mwovu, ni muzaifu, ni mubaya na ingine matusi na masimango mbaya». Ee mtu, huyu mutu weye unamuhukumu ni mtu sawa na weye; sawa na weye na sisi wote tuko watu wenye zambi. Alikosa yulu ndugu? Uwaza ya kama na weye utafanya zambi siku ingine.

Alianguka mtu moja mu zambi na kosa fulani? Na weye utaanguka mu hii ao ingine kosa. «Kwa sababu wote wamefanya zambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu». (Wa Roma 3, 23).

7. Huyu mtu mwenye majivuno anakataa kutii kwa wazazi na wakubwa wake, anakataa kuomba hurumia, kama anakosa kwao, kwa sababu singo ya wenye majivuno ni ugumu na usiyetengwa. daima wanataka kufata watu wengine ma sauti na mapenzi yao.

8.

Kila kazi na tendo kizuri ekona moja mwenye majivuno, anasadiki ya kama aliifanya paka na maungo yake, paka na ma nguvu na akili na mapenzi na machoko yake na anakataa kusema ya kama alimusaidia Mungu. Ee mutu mumbafu, kintu ninyi unaweza kufanya weye paka na maungo yako? Usikutoke mbunji toka tumbo ya mama yako. Unaweza kufanya ninyi weye, kama Mungu, ambaye eko chemchem ya kila tendo kizuri, hasitakupatie? Machoko na manguvu yako wanaweza kufanya ninyi, bila saidio ya Bwana, ambaye eko mwenye nguvu na sisi bila Huyu tuko kintu ya bure, kama kimbuli moja bila mwili?

9.

Huyu mtu hasipende watu wengine kumuonyesha ma kosa yake. Tena hasipokelee ma shauria ya watu wengine. Anafokea, anasirika na mara mingi anachabula.

11.

Anaonyesha kwa ma sauti na matendo yake ya kama eko mkubwa na anapenda sana paka uzima na maungo yake.

Hii ni matunda ya majivuno, ile wanachukia na Mungu na watu. Basi, matunda ni ya buchungu na mbego iliyewazala. «Kwani maneno watu wanayoyazania kuwa bora ni chukizo

mbele ya Mungu»( Luka 16, 15) na «kwa maana kila mutu anayejitukuza mwenyewe atanyenyekezwa, naye mwenye kujinyenyekeza atatukuzwa» (Luka 14, 11).

Mu majivuno fazila ya unyenyekevu ni chukizo. Lakini mbele ya Mungu na ya watu wengine unyenyekevu nu kuliko upendwa na wanaipokelea nzuri. Mungu Mwenyezi hasiangalie hata kintu ingine na mapendo mingi, sawa huyu mtu anayeishi na roho unyenyekevu na upole. Kwa hivi na Mzazi-Mungu anasema juu ya mungo yake: «Maana ametazama unyenyekevu wa mujakazi wake; kwani tazama, tangu leo vizazi vyote wataniita heri». (Luka 1, 48).

Kama inaepuka ya mtu moja majivuno inaikaa ndani yake unyenyekevu. Kama inashusha hii moja, inapanda ingine, kwani yote wa mbili na mbali yao kabisa na kupingana katikati yao. Inatoka giza na inakuja mwangaza. Giza ni majivuno na mwangaza ni unyenyekevu.

Kama tunahukumu maungo yetu na tunafamia uzima yetu mbaya na upotevu, paka hivi tunasaidia moyo yetu kupata unyenyekevu.

Tunazaliwa sisi wenye bunji na wenye kuria. Tunaishi ndani ya mateso, makosa na ma zambi. Tunakufa na tetemeko na maombolezo. Tunamazikwa mu bulongo na tunafanyikwa mara ingine bulongo. Hakuna uchanisho pale ndani ya bulongo ni nani mutajiri, nani masikini, nani mwenye heri, mwenye sikitiko, nani eko mkubwa, mwenye akili, ao musiyeakili. Watu wote walifanyikwa pamoja maivi. Basi, juu ya ninyi hii bulongo na maivi inajivuna?

Ee Ndugu wangu, tunapaswa kufamia usikini na taabu ya uzima yetu. «Mujinyenyekeze basi chini ya mukono wa uwezo wa Mungu, ili awatukuze ninyi kwa wakati wake» (Barua ya kwanza ya Petro 5, 6). Mupendwa wangu, inapaswa kufamia sisi wa Kristiani ya kama tunatoka ya Kristu, ambaye ni mupole na munyenyekevu kwa roho yake. Ni haya na hali yetu kibaya kujivuna Mukristu, wakati Kristu, Huyu Mungu mwenyezi na Mkubwa, alinyenyekeza Maungo yake. Ni haya sisi watumishi Wake kunjivuna, lakini Bwana wetu ni munyenyekevu. Hakuna namna Mukristu moja kuishi na majivuno, kwa sababu haina stahili kuitwa Mukristu, tena, kama anapenda kupenda yulu mu uzima yake? Paka na unyenyekevu na hapana kwa majivuno ataweza kupanda kwa ma fazila ya Kristu.

Toka unyenyekevu inafamiwa mtu moja kama ni mwanafunzi ya kweli ya Bwana Yesu ambaye eko mupole na munyenyekevu kwa roho Yake. Basi, kama unataka kushuhuda ya kama uko Mukristu ya kweli, funda toka Kristu kunyenyekeza, sawa vile na Mumoja anatuwambia: « Mufundishiwe nami, kwa sababu mimi ni mupole na munyenyekevu wa moyo» (Matayo 11, 29). Andika nguvu mu akili yako hii ma neneo ya Mutume: «kwa sababu Mungu anashindana na wenye kiburi, lakini anawapa wanyenyekevu neema» Barua ya mbili ya Petro 5, 5).

## Zambi ya ulimi

Usichokoze watu wengine, lakini tembea na suburia mbele kwao na upole, sawa vile unataka na weye kwa maungo yako. Sawa vile unaonyesha hali ya uzima yako ya inje mbele kwao, vile utasikia na ndani yako. Kila sauti unasema na midomo yako, vile inapaswa kusadiki kwa roho yako.

Udanganyifu na uchokozo ni matendo ya watu wa bure, kwani ndani ya ma roho yao anaishi shetani na anawafundisha wongo na udanganyifu juu ya kuharabisha uzima yao.

Basi, usitembee pamoja na mukaribifu ndugu yako katika uwovu na siri, kwa sababu utaacha fasi kuingia shetani kwa roho yako na utakuwa mutumishi yake.

Ishi na pasopo mingi na usisikitike mtu mwingine ao na ma neno ao na matendo yako, kwani ni hii zambi mnene kabisa. Kama unachokoza mtu moja ni sawa kuchokoza Mungu, ambaye anapenda kila mtu. Ni kweli ya kama sikitiko kwa ndugu yako inanioloka kupingana kwa Mungu yako. Huyu mtu anayekosa kupingana ya kiumbe, anakosa mbele ya Mungu.

Sawa vile unasikia, hii ni kintu matata kabisa. Kwa hivi, kama utauzi mukaribifu yako, kimbia bio na omba hurumia katika unyenyekevu na hivi usianguke kwa uhukumu ya Mungu.

*****

Hakuna faida ya roho kama unaangalia matendo ya watu wengine. Hii maangalio inapatia mwanzo ya kuchukia, masimango na zambi ingine. Ni nani lazima kuangalia matendo ya wa ndugu wako? Ya kwanza angalia na hukumu na famia maungo yako.

Kumbuka zambi yako ya zamani na safisha hii zambi kwa toba na kuvunjika ya roho yako; vile usitaangalia watu wengine wanafanya ninyi. Angalia kila siku ndani yako kama inakaa pale hata moja zwezo mbaya na hivi utafurahi kutafuta makosa yako ndani ya maungo na roho yako. Ni kweli ya kama haina namna kuangalia sisi kweli na safi roho yetu, lakini tunaweza kujua ya kama ndani yake inafuchama kila kazi kibaya. Hii uhukumu itakusaidia kwa sababu inazala unyenyekevu, boka ya Mungu, maendeleo ya maungo yako, upandisho kwa sala na mapendo ya Mungu.

Uhukumu ya ma kosa wa watu wengine ni kupindua chemchem ya kila zambi. Na mbele ya macho ya Mungu na ya watu wote hii uhukumu ni zambi na inaleta chuki. Basi, chunga moyo yako toka hii zambi.

Kama utaona ao utasikia mtu moja ambaye akafanya zambi fulani, usimuhukumu. Kama weye utasema zambi yake kwa mtu mwingine, yeye ataisema kwa mtu wa mbili, yule kwa mtu wa tatu, wa ine na hivi watasikia watu wote zambi yake; kisha watamuhukumu na hii zambi yao itakuwa mnene. Basi, sababu ya hii yote hali uko weye, aliyesimanga ya kwanza zambi yake ndugu yako.

Ninyi wote wanahukumu na wanachabula wa ndugu wao, wanafanana na wenye wagonjwa ya lepre, wenye wanauzi na buchafu yao na watu wengine; ao wanafanana na wale walipata malari ya kuzambalishwa na kwa watu wengine na hivi wanapeleka hii malari yao na kwa watu wengine na hivi wanaleta mateso ma fasi yote. Kwa hivi usichabula mukaribifu yako, kwa sababu unakosa nguvu sana na weye na unaleta maneno na kwa watu wengine kufanya zambi ya kuhukumu.

Tena toka ya zambi ya uhukumu, kwa sababu kila mtu «kwa bwana yake mwenyewe anasimama ao anaanguka» (Wa Roma 14, 4). Lakini na weye uko mwenye zambi; na kama huyu mwenye haki haipaswe kuhukumu na kusimanga, ngapi kuliko mingi haipaswe kusimanga moja mwenye zambi?

Uhukumu ya watu ni kazi paka ya Bwana Yesu, kwani Mungu Baba Yake alimupatia hii mamlaka. Huyu atahukumu wenye kufa na wenye mzima na kwa hii uhukumu utakuwa na weye. Basi, sopoka, kama unaiba mamlaka ya Bwana Yesu, kwani ni zambi mnene sana.

Usihukumu watu wenye wanafanana na weye, kwa sababu utakuwa kwa Uhukumu wa milele mukosefu sana na utahukumwa kwa gehena ya milele. Pindula macho yako na uwazo yako paka kwa maungo yako; umuangalie maungo yako, umufungula na umuhukumu paka maungo yako mbele ya Mungu kwa ajili ya zambi yako, kwa sababu hivi utapata toba. Omba toka Mungu rehema kwa saidio ya maungo yako mukosefu, sawa vile na muto zakodi, juu ya kupata haki katika wema Wake.

Sikia, anasema ninyi Bwana Yesu Kristu kwa huyu anayehukumu: «Kwa nini unaona kitakataka ndani ya jicho la ndugu yako, lakini hufikili boriti iliyo ndani ya jicho lako mwenyewe? Ao namna gani utamwambia nfugu yako: Unipe rehusa nitoe kitakataka ndani ya jicho lako; na tazama boriti ni ndani ya jicho lako mwenyewe? Mudanganyifu, uondoe kwanza boriti ndani ya jicho lako mwenyewe; kisha utaona wazi kitakataka ndani ya jicho la ndugu yako» (Matayo 7, 3-5).

Unaona ya kama ninyi wote wanahukumu na wanasimanga watu wengine ni wadanganyifu na wa Krisrtiani wa wongo? Hawa wa Kristiani, wenye wanaonekana inje kama watakatifu, wekona zambi ya siri hawapende kuiona na hivi hawajue maungo yao ya kweli.

## Toka ya uzima utamu

Swa vile unatoka moja ugonjwa kibaya, vile toka na uzima utamu, kwani hii uzima inaleta malari mu nafsi yako. Hii uzima utamu inatakia bintu ya mageni, inafanya uzulumu kwa ndugu mwingine na inakufundisha kukataa afanya huruma, inaye iko lazima kwa kila Mukristu.

Uzima ya furaha inafanana kama tumbo moja inayesiziba hata kidogo; inafanana kama hadeze inayekunywa kila kintu kizuri. Inaomba ma bintu mengi na kisha anaacha hii ya zamani na inaomba bintu ingine: Kwa mufano, nyumba yangu haina nzuri; inapaswa kuyenga ingine upya». « Hii nguo yangu ni mbaya; inapaswa kusona ingine». «Ninasikia haya kutoka inje na hii motokaa ya zamani; inapaswa kuuza ingine upya». « Hii chakula inanileta uzarau; inapaswa kufanya chakula ingine». «Misiweze kunywa hii vinyo; inapaswa kuuza ingine upya». «Haipaswe kunisaidia watumishi wangu na mimi ninavaa hii mavazi; nitauza kuvaa manguo mapya na kupita mazuri. . . »

Kwa hii namna matakio ya uzima butamu inakokota mafa yako yote na inaharabisha akili yako. Basi, sopoka mingi toka hii matakio kibaya.

Uzima yetu iko namna kuishi sisi na ma bintu madogo. Kwa hivi usipembe mwili yako na mavazi mapya na nzuri kabisa, sawa vile wanafanya watu mengi. Vazi nzuri ni kwa weye jina yako. Ma Pambo ya Mukristu ni ma zawadi yenye wanapamba nafsi na hapana mwili yake. Upambo ya nafsi ni picha ya Mungu kwani sisi hivi tumeumbwa. Hii upambo na weye tafuta mu uzima yako na inenea kwako.

## Mbali ya ulevi

Ulevi ni zambi moja mnene. «Wala wizi, wala wenye tamaa, wala walevi, wala watukanaji, wala wanyanganyi hawatariti ufalme wa Mungu» (Barua ya kwanza kwa wa Korinto 6, 10), katika fundisho ya Mtume Paulo. Lakini na Kristu mumoja anatwambia hivi: «Mujiangalie mioyo yenu isipate kulemewa na ulafi na ulevi, na masubuko na maisha haya siku ile isije kwenu gafula kama mutego» (Luka 21, 34). Tena inafanyiwa maneno ya zambi ingine kabisa matata: Inazala makele na ma funjo na toka yao inakuja mauwanji na ma bilonda. . Hii ulevi inaleta machabulana na ma mbukomvi na ma sauti mbaya. Hii zambi inaleta mazulumu na ma taabu kwa wa ndugu wetu. Inafundisha wongo, chuki, unyanganyi na kuiba wa ndugu wetu. Tena hii zambi inajaza maungo ya yule mulevi na kisilani, hasira na inasukuma watu kuanguka kwa uchafu ya zambi ya mwili sawa vile ma ngurumbe wananawa ndani ya buchafu.

Na ma sauti kidogo kusema hii zambi inafanya mtu moja kama nyama. Mungu alimufanyisa mwenye akili lakini hii ulevi inamufanyisia wasipo akili. Inageuza hali ya roho, lakini na hali ya mwili yake ya inje. Kwa hivi Mt. Yoane Krisostomo anatuwambia ya kama shetani hasipende kintu ingine kuliko mingi paka ulevi na uzima ya zambi ya mwili, kwa sababu hasifanye mtu mwingine hii ma zambi kupita paka huyu mulevi.

Lakini ulevi haina maneno paka ya matendo mbaya katika roho, lakini ni maneno ya matendo ya mwili:

1. Mwili inaharabisha na inaingia teketeke malari ya kuachana.

2. Inaongoza mu upotevu na usikini. Madiko Takatifu anasema ya kama mulevi moja hakuna namna kuwa mutajiri.

3. Inaharabisha sifa na jina nzuri ya yule mulevi; inamutupa ku uzarau, usiyoutukufu na inamuepuka mbali wa ndugu yake.

4. Ulevi inaleta kwa wajirani, wenye ya nyumba na warafiki huzuni ya roho; lakini kwa wa adui inaleta furaha.

5. Ulevi inaharabisha mutu na yeye hasiweze kutumika. Kazi gani anaweza kufanya mulevi moja? Paka mateso na ma hatari yeye anaweza kuleta na hapana kazi nzuri. Mt. Yoane

Krisostomo anandika hivi: «Ulevi hasina kintu ingine paka utoaji ya akili na mateso ya kuichekwa na malari ya kuichokozwa. Ulevi ni shetani. Kama munataka kuchunga maungo yenu na kusaidia na watu wengine mufata hii ma shauria inaifwatayo:

1. Wa kijana haipaswe kunywa vinyo na ingine-ingine, kwa sababu wanaizombelea bio na kila zwezo atafunda mtu moja kwa udogo wake, anaiendelea mu uzima yake yote.
2. Musiwaache wa kijana watu kutembea pamoja na walevi na watu wapotevu.
3. Wenye wakubwa kwa kipimo haipaswe kunywa vinyo bila lazima mnene.
4. Muepukeni ya kila mapatano mbaya na machezo.
5. Mufundisheni wa ndugu wenu ya kama ni nguvu sana mtu moja kusimamisha hii zambi ya ulevi na tena ya kama watu mengi waliharabisha mwili na nafsi yao.
6. Wale watu walizombelea hii zwezo kibaya ya ulevi, inapaswa kukamata silaha nguvu kupingana yake. Inapaswa kusimama na uvumilia, bila kulekea, inapaswa kuomba kwa Mungu juu ya kupata saidio na neema yake.
7. Tena wale watu inapaswa kuleta mu akili yao ile mateso wanaishi ile saa ya ulevi yao na kisha watawaza namna gani ni uzima ya mtu moja mwenye akili na musiyekunywa.
8. Tena inapaswa kuwaza ya kama watu mengi wanakufa pa hii zambi ya ulevi na wanasafiri toka hii nyakati kwa nyakati ya milele, bila mahasa na bila toba!

## Chuki

Chuki ni moja ya zamani na ya wakati mingi hasira. Wakati hasira hasiangusha, inageuzwa kwa chuki. Kwa Mutume anatushauria na anatuwambia kufukuza hasira bio, kabisa bio: «Mukasirike na musifanye zambi; jua lisishuke na uchungu wenu hauja kwisha bado; wala musimupe shetani nafasi» (Kwa wa Efeso 4, 26-27). Hivi tunaona ya kama huyu mtu anayechunga hasira na chuki kupingana ya mukaribifu yake, anaacha shetani kuikaa ndani yake. Huyu shetani kwani ni roho ya chuki anamunyanganya na anamukokota kama mutumwa yake.

Chuki inazaliwa ao toka tamaa- Kaina kwa mufano alikuwa na tamaa kupingana ya ndugu yake Abeli; alitamaa maendeleo yake mu kazi yake, kisha alimuchukia na alimuuwa (Mwanazo 4, 8)- ao inazaliwa toka mazulumu wanayefanya watu kwa wa ndugu wao wengine. Nikusema watu wanasirika na wanachunga chuki kupingana ya yule mutu aliyewazulumu na wanataka na namna ya kuachana kuwafanyisia tendo moja kibaya.

Hii zambi ya chuki na upumbafu na upotevu sana. Zambi ingine wanapata kidogo furaha kwa huyu mtu mwenye zambi: Kwa mufano huyu mwivi anaiba juu ya kupata kila kintu inayependa roho yake; mwenye zambi ya mwili anafanya zambi yake juu ya kufurahisha mwili yake; lakini huyu anayechukia hana na kintu kimoja ya furaha. Anafanya zambi na anateswa sana, anakanyanga sheria ya Mungu na anaharabisha uzima yake, anachukia na huyu mumoja anateswa kwa ajili ya matakio kutenda kazi kibaya kwa ndugu yake. Chuki yake ni malipizo na mateso yake.

Kama ilikuwa namna kuangalia mtu moja roho ya yule mwenye kuchukia, ilikuwa namna kuona paka mateso ya gehena ndani ya roho yake. Vile inaelezewa juu ya ninyi watu wa chuki wanajaza na giza na wanasikitika na buchungu mu uso yao. Chuki kama sumu inakula mwili yao.

O, zambi mnene ni hii! Ni zwezo matata na ya kuharabika roho ya yule mtu iko nayo ndani ya roho yake. Kama hasitafanye kangamano kukata hii zambi, itamuletea mu uzima yake uharibifu mingi, sawa vile moto inavimba mu nyumba moya na inalungua yoyote. Kama hasitasimamishwa na haraka, inazambalishwa kama moto pa kuni ya kukauka, sawa vile anatuwambia Mt. Yoane Krisostomo.

Chuki inaonekana na namna mengi:

Na uharabisho ya afya ya mtu mwingine.

Ya kuuwa mutu mwingine sawa vile alifanya Kaina kwa ndugu yake Abeli.

Ya kusema ma sauti mbaya na kumusitaka. Nikusema, huyu mtu mwenye chuki anatafuta kufanya kazi kibaya kwa ndugu yake; kama hasiweze, anatafuta namna ingine, nikusema anasema

wongo kwa watu wengine ya kama huyu mtu anayemuchukia alifanya zambi fulani na hivi anamuchukia sana. Wakati ingine anakomea kazi moja yake kidogo. Nikusema hii kitakataka inaiona kama boriti kwa ndugu yake (Ona na Matayo 7, 3-5).

Vile watu mengi wanatesa kwa ajili ya ma sauti wongo ya watu wengine. Maneno yao ni chuki.

Mara mingi, ninyi wanachukia wengine wanatukuzwa wao wenyewe juu ya hii kazi kibaya waliifanya kwa ndugu yao: «Mimi nilimusimanga sana, ao nilimupika sana, ao nilimuchabula sana. Atanikumbuka mu uzima yake yote». Kwao ni lazima kusikia sauti ya Nabii Daudi: «Kwa nini unajisifu kwa uovu, ee wewe mutu mwenye uwezo? Rehema ya Mungu ni daima» (Zaburi 52, 1). Anafurahi na anajisifu kwa sababu aliharabisha uzima ya ndugu yake!

Ngapi ni uharibifu na wenye makari hii uonyesho ya chuki! Wakati ngapi alipaswa kutaabu na kuria huyu mwenye chuki, kwa sababu alikosa kupingana ya Mungu na mukaribifu yake? lakini anajisifu na anajivuna, wakati anafanya zambi yake na anatukuza maungo yake kwa zambi yake. Anakanyanga sheria ya Mungu na anavimba kwa ajili ya uzulumu yake, kwani ndani yake inatumika hii chuki kibaya na upotevu.

Ee mutu mwenye taabu! sasa unatukuzwa na unafurahi kwa ajili ya matendo mbaya na mazulumu yako! Lakini kama usitatubu, itakuja wakati na utaomboleza, utaria na utatosha ngozi ya mwili yako kwa ajili ya sikitiko yako; ile wakati matendo yako yote wataonekana mbele yako na mbele ya ma macho ya watu wote, sawa vile hii mambo itafanyikwa na kwa matendo ya watu wote ya dunia. Ile wakati utasikia na utaona uharibifu yako.

Chuki inakomea na inavimba ndani ya ma roho ya watu mengi, lakini hawa wanasema bila boka: «Na mimi mitapotea, lakini na huyu misitamuache kuishi na kimya! . . . »O, kiumbe ustahili ya machozi mingi! Usijue, basi, ni ninyi maana ya uharibifu? Karibia mukono yako mu moto na utasikia kidogo. Hii mambo usiweze kuivumilia; basi, utaweza kuvumilia hii mateso mu moto ya Gehena, pahali utatupwa muzima ndani na chini yake, bila kulunguwa kamili kwa milele? Kama utaangalia paka weye wenyewe maungo yako, utasikia ya kama shetani, roho ya chuki, inakusema hii ma neno kwa kinywa yako.

Munaona, wa ndugu wangu, zambi matana ninyi ni zambi ya chuki na namna gani iko nguvu kuitosha mtu moja ya roho yake? Na matunda yake ni ma buchungu. Buchungu na sumu ni na hii inawazala.

Chuki ni mateso mu dunia yetu! Inaharabisha watu wote, sawa vile tulisema. Hata mtu moja hasiweze kuchungwa toka hii zambi ya chuki. Kama hasiweze kufanya tendo mbaya kwa ndugu yake, anaanza kumuchabula na ma sauti ya wongo. Mateso ma ngapi na masikitiko ma ngapi ni mu dunia yetu na mwanzo yao ni paka chuki!

Chuki na zambi matata mu dunia yetu. Lakini mateso ingine kuliko mingi ni kwa wale watu wenye wanachukia wa ndugu wao. Kwa sababu wanaharabisha hapana mawili ya watu wengine, lakini na nafsi yao; wanauwa ma mwili ya watu wengine na ma nafsi yao; wanasimamisha uzima hii ya ndugu yao, lakini na nafsi yao wanaiongoza mu gehena. Hii ni matunda matata ya chuki.

Wale watu wanafata hii zambi ya chuki, kama hawapende kuharabishwa, ni lazima kutubu na kugeuza ma roho yao. Juu ya kuwasadia sisi, tunaongeza hii mafundisho inafuatayo:

Ni kazi matata kuchukiwa wa Kristiani katikati yao, kwa sababu Bwana Yesu Kristu alitushauria kupenda sisi hapana paka ma rafiki, lakini na wa adui yetu. Ni kazi bila kuisikia sisi kama wa Kristiani wanafanya hii kazi kibaya, lakini wekona amri kusaidia na kuonyesha mapendo yao kwa wale wanawachukia.

Ni matata kwa wa Kristiani kutafuta namna juu ya kujilipiza kisasi, lakini walijihamuru kusamehe makosa ya wa ndugu wao. Huyu anayejilipiza kisasi, ataanguka kwa mikono ya Mwenye Kisasi Mungu; Ni kweli ya kama «Ni neno la kuongopa kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai»! (Wa Ebrania 10, 31).

Hiyu nafsi anayechunga vhuki ndani yake inapaswa kuwaza hii yote na kutosha sumu ya hii zambi yake paka na toba na maombolezo ya roho yake; kama hasitafanye hivi. Ataonekana na ma zambi yake mbele ya Uhukumu matata ya Kristu juu ya kubeba matunda ya matendo yake.

Iko namna hii kazi kibaya anatayarisha kufanya mtu moja mwenye chuki kwa ndugu yake, anafanya hii tendo kwa maungo yake. Hii sumu anayeitayarisha kwa watu wengine, anaikunya yeye mwenyewe. Hii zimu aliitayarisha juu ya ndugu yake, anaanguka yeye. Hii sauti anatuwambia na Nabii Daudi hivi: «Amefanya shimo, amelichimba, na ameanguka ndani ya shimo alilolifanya. Uharibifu wake utarudi juu ya kichwa chake mwenyewe na ukali wake utamuchukia utosini» (Zaburi 7, 16-17).

Sikia tena na shauria na Mutume, ee ndugu wangu: «jua lisishuke na uchungu wenu hauja kwisha bado; wala musimupe shetani nafasi» (Kwa wa Efeso 4, 26-27). Tena kombana kuuwa ndani yako hii hasira yako toka saa ya kwanza; ile wakati hii hasira ni kidogo ndani yako, konbana kuuwa juu hapana kukomea na kukuharabika.

«Ee Mupenzi, usifuate ubaya, lakini wema. Yeye anayetenda mema ni wa Mungu, lakini yeye anayetenda mabaya hakuona Mungu» (Barua Tatu ya Yoane 11).

## Mapendo

Kwani sasa tunaisha kusema juu ya chuki, sasa ni lazima kusema juu ya fazila ya mapendo.

Chuki inachukia mapendo. Hata buchungu ni chuki, hata hivi utamu na fazila ya mapendo; hata uharibifu inaleta chuki, hata faida inaleta mapendo; hata ma ngapi machungu ni matunda ya chuki, hata kabisa wema ni matunda ya mapendo.

Chuki ni uchungu na kwa watu wengine na kwa huyu anayeiko nayo; lakini mapendo ni utamu na kwa huyu anayependa na kwa wao wanaopendwa.

Chuki inafunga roho, lakini mapendo inamuuhuru na inamufungula.

Chuki inauwa watu, lakini mapendo inazala watu mara ya mbili. Mufu ni huyu anayechukia; lakini huyu anayebakia kwa mapendo anajaza na uzima utamu.

Chuki inataabu watu; lakini mapendo inatulivu, inashangilia na inafurahi.

Chuki ni ugumu na makari; lakini mapendo na upole na wema.

Chuki ni wa majivuno; lakini mapendo ni wa unyenyekevu.

Chuki ni bila wema; lakini mapendo urafiki-wema.

Chuki ni bila uvumilia; lakini mapendo anawema.

Chuki wanaizarau watu wote; lakini mapendo ni wa kupokelwa na wa furaha.

Chuki wanaichukia watu wote; lakini mapendo wanaitukuza na wanaipenda wote.

Huyu anayeishi na chuki ni maskini na musiyefuraha; lakini huyu anayeishi na mapendo ni mwenye heri na mubarikiwa.

Huyu anayeishi ndani ya chuki wanataabu na watu wengine na Mungu; lakini huyu anayeishi ndani ya mapendo na Mungu na watu wanafurahi.

Chuki ni mbego ya shetani; lakini mapendo ni mbego kimungu.

Basi, wale wanafata hii zambi ya chuki ni wapotevu na wenye taabu, hata kama na watu wengine wanawasifa kama wa mungu. Lakini wa heri na ubarikiwa ni hii roho inayejaza na mapendo, hata kama watu wengine wanaikanyanga sawa vile bulongo ya inchi.

Wale ya kwanza wanaonekana ya inje wenye wazuri, lakini ndani yao ni watu mbaya; lakini wenye watu wa mapendo kwa inje wanaonekana kama wasipo utukufu, lakini ndani yao ni wenye wazuri. Wale wanangazia ya inje; lakini ndani ni wa mweusi na wenye giza; hawa wenye mapendo hawaonekane ya kama ni kintu kizuri, lakini ndani yao wekona yoyote matendo zawadi ya Mungu. Wale wanafanana kama muti ya kuoza, lakini hawa wa mependo ni muti nzuri na kunioloka.

«Fanyeni muti muzuri na matunda yake mazuri; ao fanyesi muti mubaya na matunda yake mabaya; kwa sababu muti unajulikana kwa matunda yake». (Matayo 12, 33). Basi, iko lazima kufamia mapendo toka matunda yake, matendo yake, kwa sababu hivi mapendo inafamiwa na hapana na ma neno.

Ee ndugu wangu, kama tulikuwa na mapendo ya kweli! Ilikuwa namna kufukuza mbari ya sisi kila sikitiko na ilikuwa namna kutujaza na heri na furaha. Ma muji na ma mukini na ma nyumba yetu watakuwa vipande ya Paradizo ya kujaza na furaha na wenye heri.

Kama ilitawala mapendo katikati ya watu, hakuna boka toka matendo ya wanyanganyi, mauuwaji, unyanganyi, kwa sababu «mapendo hayafanyi mwenzake neno mbaya; basi mapendo ni utimilifu wa sheria» (Wa Roma 13, 10). Hasikukuwe namna kunyanganya mtu moja kintu ya ndugu zake, kwa sababu mapendo hasifanye kazi kibaya kwa mwenzake. hakuna namna watu kuishi na mahukumu, maaa neno ya haya, mazulumu na mateso ingine, kwa sababu mapendo hasifanye kazi kibaya kwa mwenzake. Watu hakuna namna kulanda watu wengine, ao kuwachokoza, kwa sababu mapendo hasifanye kintu kibaya kwa mukaribifu yetu. Hasikukuwe lazima ma nyumba ya Uhukumu, kwa sababu hawasikukuwe kintu fulani kuhukumu, kwani hakuna watu wanyanganyi na wazulumu. Ma nyumba ya Uhukumu waliyengwa kwa ajili ya kuhukumu mazulumua watu mbaya. Huyu anayependa kweli ni mbali ya hii ma nyumba ya Uhukumu, tena mbali ya kila zambi.

Kama inatawala mapendo, hakuna lazima ya  wa zamu, lazima ya kofiri na ma sanduku ya feza, kwa sababu hakuna wa mwivi na wanyanganyi. Kama inatawala mapendo, hakuna watu ndani ya ma buloko kwa ajili ya ma ndeni yao, ma chuki yao na mambo yao ya kila siku. Mapendo hasiache kufika watu mu buloko, kwa sababu inavumilia (barua ya kwanza  wa Korinto 13, 4). Kama inatawala mapendo, watu hakuna namna kutembea na manguo ya kuarabika kama kilako ao wa bunji, kwani mapendo anaweza kuwavaa. Kama inatawala mapendo watu hakuna namna kuishi bila nyumba. Kama inatawala mapendo hakuna waskini na wenye wanaomba saidio. Mapendo ya watajiri iko namna kuwapatia bintu ya  uzima yao.

Kama inatawala mapendo hakuna namna wakubwa kusirika kupingana ya taifa yao na taifa kupingana ya wakubwa yao, kwa sababu wakubwa watasubuka taifa yao kwa kila mambo yao. Kama inatawala mapendo hakuna mambo ya sikitiko katikati ya wachungaji ya Kanisa na wa Kristiani wao, ao katika ya wakubwa na watumishi wao, katikati ya wazazi na watoto yao ao katikati ya watoto na wazazi yao.

Kama inatawala mapendo katikati yetu, kimbabashi kupingana ya wa adui yetu wasionekana na wasiponekana  ni nguvu sana; kwa sababu pahali fasi ni mapendo, pale ni na Mungu mumoja, Musaidizi na mulinzi ya mapendo.

Ewe mapendo utamu na ufaziliwa-neema!

Bila mapendo yoyote bintu ni mbaya na bila kitumaini. karibu ya mepndo yoyote ni nzuri na mabarikiwa.

Wa kristiani mengi wanatakia na wanakangamana kuishi ndani ya manyumba makubwa, kuikaa ya kula nzuri, kuvaa ma nguo mazuri kabisa, kutembea na ma motokaa yao,  hata kama wanaona pempeni yao na wamaskini na wenye mateso wa ndugu wao. Toka hii mambo inaonekana ya kama wanapenda paka maungo yao, na hapana Mungu na mwenzake yao. Hii ni chemchem ya kila muchoko na mateso na umaskini. Majivuno ni maneno ya kila kazi kibaya!

Ewe Wakristiani Wangu! Uharibifu yetu ni mnene kama hakuna mapendo! Pahali fasi inalofa hii mapendo, inalofa na imani. Imani bila mapendo hasiweze kusimama. Na pahali hakuna imani, analofa Kristu na wokovu wetu. Sisi tunahubiri Mungu anaye eko mapendo. Basi, twende juu ya kupenda moja kwa mwingine, «ili kwa nia moja tuungame Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu».

## Saidio ya Mungu

Kila makangamano yetu, bila neema ma saidio ya Mungu hasiweze kuzala matunda. Mutu moja iko namna bio-bio kutelemuka na kuharabika nafsi yake; lakini kama anataka kutengeneza nafsi yake na kuokolewa, hasiweze kurudi bila saidio ya Mungu. Anaishi  bila mambo katika matakio ya mwili yake, sawa vile na chombo inatembea ndani ya maji ya mutoni. Lakini haina mambo ya teke-teke paka yeye mwenyewe kukombana kupingana kwa matakio ya mwili yake na

kutembea kwa maendeleo ya uzima ya roho. sawa haina kazi teke-tekle moja chombo kutembea kupingana ya pepo nguvu ndani ya mutoni moja. Iko lazima kusaidia watumishi ya hii chombo, pepo na ma nguo ya pepo. Vile na mtu moja kwa uzima yake ya roho na tendo ya wokovu yake, ikona lazima ya saidio ya Mungu. Unapenda kushindi maungo yako; lakini namna gani iko namna kufanyikwa hii kazi bila saidio ya Mungu mwenyezi?

Hali yetu uharibifu ni ngapi! Kwa hivi shetani anakombana bila usimamisho kila mtu na anakombana kumutupa mu zambi na kumubamba ndani ya makila yake. Ma furaha ya utamu ya hii dunia wanatuzunguluka na wanatukokota. Tena na zambi na ma zwezo mbaya wanatukokota karibu yao. Tunaona watu wa mingi, wenye walitubu na walianza kusiha katika sheria ya Mungu, lakini kisha wanatoka ya njia ukweli na wanatelemuka mu zambi na uharibifu.

Toka hii yote ma sauti tunasikia ya kama tusiweze, bila saidio ya Mungu Mwenyezi, kuanza uzima ya heshima ya Mungu, kuishi katika Kristu na kukufa katika sheria ya Kristu. Hawa wanapita ndani ya majaribu, wanajua hii mambo.

Kwa hivi, anatuwambia kweli Bwana Yesu: «Pasipo mimi hamuwezi kufanya neno» (Yoane 15, 5). Kila saa na kila dakika tuko na lazima ya nguvu kimungu. Basi, kama unatakia kuishi na boka ya Mungu, kama Mukristu wa kweli juu ya kuokolewa, omba bila kusimama Mungu saidio ya Mungu. Mungu, katika ubinadamu yake, sawa vile alitutangaza kuomba Kwake na kuomba kila kintu wema, hivi alitulaka ya kama atatupatia ile kintu tunaiomba, nikusema ile ni lazima ya wokovu wetu: «Ombeni, nanyi mutapewa; tafuteni, nanyi mutaona; pigeni mulango, nanyi mutagunguliwa; kwa maana kila mutu anayeomba anapokea; naye anayetafuta anapata; naye anayepiga mulango atafunguliwa» (Matayo 7, 7-8).

Neema Takatifu ni uzima ya nafsi yetu. Bila hii nafsi yetu hakuna namna kuishi. sawa vile mwili yetu hasiishi paka pamoja na nafsi, vile na nafsi hasiweze kuishi paka pamoja na neema takatifu.

Basi, omba daima na omboleza mbele ya Bwana Yesu juu ya akupatia Neema Yake takatifu.

Ee mupendwa wangu, inapaswa ku jua ya kama Mukristu bila sala ni ndege bila mabawa na askari bila bunduki. Omba kwa Bwana Yesu Kristu ya kuendelea na umotoa maungo yako Kwake juu ya kuongoza mu uzima ya milele na wa heri. Lakini fanya nguvu na weye kujichunga; na Yule mukuona sindano yako atakusaidia kwa matendo yako yote.

## Makumbusho ya Mateso takatifu ya Bwana Yesu

Makumbusho ya Mateso takatifu ya Bwana Yesu ni kweli moja nguvu saidio mu sindano kupingana ya zambi na mu saidio ya uzima katika Kristu. Mutume anatuwambia: «Na kama mukimwita Baba, yeye anayehukumu kila mutu pasipo upendeleo, kwa kadiri ya kazi yake, mwendelee na woga katika wakati wenu wa kukaa hapa kama wageni; mukijua mumekombolewa, kwa vitu vinavyoharibika, kwa feza ao zahabu, mupate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa muliopokea kwa baba zenu; lakini kwa damu ya damani, kama ya kondoo asiye na kilema wala alama, damu ya Kristu» (Barua ya kwanza ya Mt. Petro 1, 17-19).

Ee Mukristu wangu, uwaza, namna gani uliokolewa toka zambi, shetani, hadeze na lufu wa milele: hapana na ma zawadi ya bure. Lakini namna gani? katika Damu Uheshimiwa na usifiwa ya Kristu, Mwana wa Mungu. Basi, utapendeza kukosa na mapenzi yako na kuzarau katika zambi yako moja Mufazili mkubwa sawa Huyu Bwana Yesu? Utafanya mara ingine hii kazi kibaya kutupa maungo yako ndani ya hii uharibifu, pahali alikuokoa Yesu na Mateso yake ya uchungu kabisa? Hii inafanana sawa mtu moja alikuokoa toka lufu, toka moto, toka bahari toka utumwa ao buloko ao toka kazi kibaya ingine na weye kisha na mapenzi yako unatoa maungo yako kwa hii kazi kibaya.

Vile unafanya na weye, kama unakosa na unatoa mara ingine nafsi yako kwa shetani na unatupa maungo yako mu uharibifu wa milele.

Zambi inaonekana utamu kwa kila mtu, lakini matunda yake ni machungu na wenye matata. Ni lufu wa milele «Kwa maana mushahara wa zambi ni mauti, lakini zawadi ya Mungu ni uzima wa milele katika Yesu Kristu Bwana yetu» (Wa Roma 6, 23).

Lakini na hazina ya wokovu wa milele hasikuuzwa na namna ingine, paka na Damu umoja ya Yesu Kristu, mwana wa Mungu. Huyu hazina ya uzima wa milele ni kupita ukubwa ya dunia nzima, ya mbingu na inchi na bintu yake yote. Kwa sababu ni wa milele na ni utumizo ya matendo wenye milele na wasipokusikiwa. Aliuzwa na sifa uweshifiwa. Kristu, Bwana ya utukufu na Mungu, alituioa hii hazina katika Damu Yake uweshifiwa.

Hii hazina ukubwa kabisa unapenda kuipotesha? Kristu alikukokota kama Mungu mwenyezi toka uharibifu. Yeye tena alikupatia uzima wa milele na wenye heri. «Maana hivi mutapewa tele kuingina katika ufalme wa milele wa Bwana wetu, mwokozi Yesu Kristu» (Barua ya mbili ya Petro 1, 11).

Usaada pa imani na ulinzi hazina yako toka adui shetani, anayetaka akutumwa na akubeba hii hazina. Umukombana daima.

Tena, basi, kumbuka mateso ya Kristu na hii itakufundisha kila fazila yake.

## Ufwasi ya uzima ya Kristu

Kama unataka kutengeneza maungo yako na kuwa Mukristu wa kweli, mtu ya Kristu, chunga mbele ya macho ya roho yako Uzima Yake na umuangalia juu ya kufata mufano ya Bwana yako. Kama roho yako kwa ajili ya zambi yake, inakataa kufata Mufano ya Yesu, weye umusukuma na umuwambia kufata ma fazila makubwa ya Kristu.

Mara mingi unaangalia mu rikalasi kama ukona machafu ao simoko pa sura yako na kisha unaisafisha. Rikalasi ya roho yako ni Uzima wasipo zambi ya Kristu. Angalia pale kila wakati juu ya kuona hali ya nafsi yako: Roho yako anataka hii kazi anataka Kristu? Anafanya kila kazi alifanya Kristu, wakati aliishi katikati yetu mu dunia? Kama unaona ya kama roho yako anafanya matendo ingine na mbaya mbele ya Uzima ya Kristu na wanaonekana kama ma simoko mara moja safisha roho yako na toba na machozi ya nafsi yako.

Kristu alizarau utukufu, sifa na mali ya hii dunia, lakini ilikuwa namna kuwa na yoyote bintu, wani alikuwa Mukubwa ya ulimwengu. sasa weye unatafuta utukufu na sifa na mali kwa hii dunia?

Kristu aliishi ndani ya hii inchi na unyenyekevu mingi; lakini weye unaishi hivi ao na majivuno na uzima ya furaha?

Kristu alikuwa mbele ya watu wote mwema na mupenda-mwema; lakini weye unapenda ao unachukia watu na ukona kisasi kupingana kwao?

Kristu, wakati walimuchabula, Yeye hasikuwachabula hata. Lakini weye unasitake ndugu yako aliyekuchabula? Ao unachukia huyu ambaye hasikukufanya hata kintu kibaya?

Iko namna watu wengine kusema matusi mbaya kwako ya kama uko mupotevu, munyanganyi, mwivi na ingine matusi. Weye utafata Kristu? Kristu mbele kwa wale walimuchabula, alikuwa mupole. Weye unasema matusi na ma sauti mbaya kwa wale wanakuhukumu?

Kristu hasikujilipiza kisasi hata mtu moja, lakini ilikuwa namna kufanya hivi, na kuharabisha watu wote; lakini weye unalipiza na kisasi watu wengine kwa sababu walikuzulumu?

Krisrtu alivumia mateso yoyote; lakini weye unasirika, kama wanakuzunguluka kwako ma taabu na mateso?

Vile inapaswa kuangalia uzima yako mbele ya Uzima ya Kristu. Na sawa vile unaweka uso yako mbele ya rikalasi, vile weka na nafsi yako mbele ya rikalasi ya uzima usafi ya Bwana Yesu. Kila uchafu, ile utaiona, kombana kuitengeneza na kufata Mufano ukubwa ya Yesu.

Kwa hii namna mimi ninakuwambia kweli ya kama utafanyikwa kila siku kuliko mtu mzuri nawa Kristu; hakuna namna kubakia mtu moja chini, kama anaangalia kila siku rikalasi usafi ya Uzima ya Bwana Yesu.

Huyu anayependa kuishi pamoja na Kristu kwa milele inapaswa kufata Uzima Yake. Inapaswa kwa hii uzima yetu kufanana na Kristu, huyu ambaye anataka utukufu Yake. Hasikusema ya bure hii sauti Yake Kristu: «Kwa sababu nimewapa ninyi mufano, mufanye sawasawa nilivyowafanya ninyi» (Yoane 13, 15) na «Naye aliyechukua musalaba wake na kunifuata hanistahili» (Matayo 10, 38).

Uwaza na pasopo hii ma neno na utasikia na utajikikiri ya kama inapaswa kufata Kristu, huyu ambaye anataka kuokolewa na kuingia mu Ufalme Wake wa milele. Sopoka tena anasema ninyi Bwana: «Kondoo zangu wamasikia sauti yangu, nami ninawajua, nao wananifuata. Nami ninawapa uzima wa milele; nao hawatapotea hata milele, wala hakuna mutu anayeweza kuwanyanganya toka mukono wangu» (Yoane 10, 27-28). Hapa kondoo ni wa Kristiani wa kweli, wenye wanatii mu Fundisho takatifu Yake, wanaishi, sawa vile Yule anawahamuru na wanamufuata kwa imani, unyenyekevu, mapendo na uvumilia. Vile anawaongoza mu uzima wa milele kama wafwasi wake wanamuamini.

Basi, hawa wenye hawakusikie sauti Yake na Fundisho yake takatifu na wanakataa kumufuata hana ma kondoo ya Kristu. Hawa hawataweza kuingia mu uzima ya milele pamoja na Ye.

Hii sauti ni wa matata, Mukristu wangu, lakini ni wa kweli. Kama utawaza paka weye wa pekee hii ma sauti ya Kristu, utaichika ya kama iko vile.

Mukristu mupendwa wangu, inapaswa kufata njia ya kweli, kama unataka kufika mu uzima ya milele. Ni nani hii njia ya kweli? Kama ukona mufano yako uzima ya Kristu. Ishi, basi, hivi na utaokolewa.

# SEHEMU YA INE
# NJIA YA KUPASWA

## Ma kazi ya kupaswa wakubwa

1.

Wa Kristiani mengi wanatakia kupenda ma sifu na mamlaka. Hawa watu wanazarawa hapana paka ya fundisho wa Kristu, lakini toka fundisho ya inje. Yule anayetafuta sifa hana mustahili ya hii sifa. Watu hawajua wanatakia ninyi na mara mingi huyu cheo inafanya kwa mtu moja sawa kisu moja kwa mikono ya mtu moja mazimu. Muti ukubwa wanaipiga ma pepo ma mingi na, wakati itaanguka, inaharabisha na ingine michi ni chini na pempeni yake. Vile na kila mkubwa na mujukumu ya kazi yake. Eko mbele na mateso na masikitiko mengi; kama ataanguka inasikiwa zambi yake mbali kabisa na analeta sharti kwa watu wengine.

2.

Kama watakuita kufanya kazi moja na jukumu, ya kwanza uwaza ma nguvu yako. Sawa vile hasiweze mtu moja kunyanyua kila uzito, vile hasiweze kukamata na kila cheo. Inapaswa ku mbele kufunda juu ya kutembesha maungo yake na kisha ataweza kutembesha watu wengine. Inapaswa huyu mtu kuishi ma fazila na kisha ataweza kufunda na wa ndugu wake.

Mukristu moja anayetumika mu cheo kubwa iko lazima kutumika na akili mingi na moyo wema. Bila akili mingi huyu mkubwa atafanya makosa mingi kama kipofu; na bila moyo wema atahatabisha kazi yake na matendo ya watu wengine.

Cheo moja iko namna kugeuza uzima ya mtu, lakini hapana ya kupanda daima. Watu mengi ilikuwa namna kufanyikwa watakatifu, kama hawasikukuwa na kwa mikono yao mamlaka.

Ee Mukristu, uwaza hii yote na usitafuta ma cheo ya buzito, paka, kama atakuita Mungu. Ile wakati, kama unataka kutoka ya hii cheo, usitaweze kuiepuka.

3.

Huyu mtu anayekamata kufanya kazi moja kubwa iko zwezo kujilaka. Hii malako inafanyikwa juu ya kusubuka huyu mtu kusaidia watu wengine, kutengeneza ma bintu katika moyo yake, kutafuta fundisho ukweli, kuhukumu uzulumu na kutumika na hake.

Lakini wa Kristiani mengi, wenye wanaanza kufanya kazi moja kubwa wanalaka ya bure; kama itapita wakati kidogo, wanasahabu malako yao. Hawa watu wanatumia mamlaka hapana kwa faida ya taifa, lakini juu ya faida yao; na kama wanaonekana ya inje kama wa Kristiani wazuri, ndani ni watu wasipo imani.

Weye usifata hawa wakubwa wa Kristiani, na hivi usitajilipiza mu Uhukumu wa haki ya Kristu, kwa sababu hii uhukumu itakuwa matata na itafanyika ya milele. Hawa wakubwa watapokelewa pale malipizo mengi, hata ngapi mazulumu na matendo mbaya walifanya ndani ya hii dunia. . . Mupendwa wangu, chunga moyo yako. . . Weye onyesha mapendo kwa watumishi wako.

4.

Kwa sababu weko wa Kristiani wadanganyifu na wenye wongo, weye usisadiki bio ma sauti yao mbaya. Sikia na moja risikio na risikio ingine sikia huyu anayependa kujibu. Usikuwe kukamata mipango na haraka. Usisadiki na haraka.

5.

Tafuta na namna mengi sauti ya kweli. Lakini kama ni nguvu kuitafuta, uiache mu uhukumu ya Mungu. Yule ataonyesha na sauti ya kweli na sauti ya wongo. Ni kupita nzuri kumuacha huyu mtu mukosefu bila malipizo na hapana kumulipiza bila haki.

Mu kazi ya wa haki usiachana watu, wa rafiki, wa adui wenye kufamia na wenye wasiyokufamia. Marafiki yako kabisa ni paka ukweli na haki. Unafanya kazi ya Mungu. Kwa hivi angalia matendo yao na hapana ma uso yao. Kwa kila mutu umupatia katika matendo yake.

6.

Kama iko lazima kulipiza mutumishi yako moja, utafanya hii kazi na sikitiko na boka mingi. Kama unafokea mtumishi moja, sopoka usisema ma ssauti mbaya na matusi. Usiseme sawa hivi: «Uko mwenye kulanda, uko mupotevu, uko mwenye kuiba na ma sauti ingine-ingine. Hii ma sauti ni matusi na hapana malipizo. Kama unalipiza, inapaswa kulipiza na hapana kumutesa ao kumuchabulana mutumishi yako. Wakubwa mengi wanaonyesha hata mingi hasira kwa watumishi wao kama ma nyama makari. Lakini weye utalipiza mutumishi yako na mapendo juu ya kumusaidia kutengeneza mufano yake. Hii ni roho ya Kristianisme: Nikusema inapaswa kusikia mapendo mu taabu na umivu ya ndugu yangu. Uwaza ya kama huyu anayelipizwa ni ndugu yako ambaye eko na mwili umoja na weye na mateso mamoja na weye.

7.

Kama utasikia hasira na kisilani mu roho yako kupingana ya mutumishi yako, chunga roho yako, usimuchabula ao kumulipiza ile saa. Ongolea kidogo kushusha nguvu ya kisilani, kwa sababu usitaweze na hali mbaya kumulipiza katika sheria ya Kristu. Kama utafanyia tendo moja na haraka, utamulipiza bila haki na inje ya sheria ya Kristu na kisha wakati kidogo utataabu na usitaweze kumusaidia mufano yake.

Hasira ni kama moja pepo nguvu inayetosha yoyote bintu inayepata mbele yake. Ni kama moto inayelungua yoyote. Mu saa ya kisilani mtu hasiweze kufanya hata tendo moja nzuri, lakini eko na nguvu kufanya paka matendo mazuri.

8.

Uwaza nzuri ya kama uko Mukristu na mkubwa ya wa Kristiani wengine. Wa Kristiani wote ni wa ndugu katikati yao. Kristu, Bwana wetu, hasishaka kuita hawa wa ndugu Wake. Lakini sisi watu wadongo ngapi kupita mingi, iko lazima kuita hawa wakubwa wetu wa ndugu wetu!

9

Basi, sopoka usizarau watumishi wako na usiwaangalia kama kibasa ya miguu yako, sawa vile wanafanya watu wengine. Inapaswa kujua ya kama katikati yao ni na watakatifu na warafiki ya Kristu na ni zambi mnene, sawa vile unasikia, kuwanyenyekevu na kuwachekelea. Kama mamlaka yako na cheo yako inakupanda yulu, lakini ndani yako uwaza ya kama weye usikuwe kuliko mukubwa na tena ya kama matendo yoyote ni ya Mungu. Mungu anaweza moja mutumishi kumupanda yulu ya cheo moja na moja mkubwa kumushuka chini mu cheo ya mutumishi moja. Uwaza, basi, hivi na usijivuna.

10.

Bila saidio ya Mungu hasifanyikwa hata kazi moja, hasikumalizwa hata maendeleo moja. Kwa hivi omba na uvumilia kwa Mungu akusaidia mu cheo Yeye alikupatia na mu matendo unaifanya.

## Ma kazi ya kupaswa watumishi

1. Kila mkubwa anakamata mamlaka toka Mungu, sawa vile inatuwambia Madiko Takatifu: «kwa maana hapana mamlaka ila kwa Mungu; na mamlaka inayokuwa, imewekwa na Mungu» (Wa Roma 13, 1). Kwa hivi, basi, inapaswa kuheshima na kusifu mkubwa yako kwa jina ya Mungu.

2.

Kwa sababu mkubwa yako anakombana kusaidia taifa, pahali ndani uko na weye, inapaswa na weye kumupenda kama baba yako na kumushukuru.

3.

Fanya nguvu kutii kwa kila sauti yake juu ya kupata faida na watu ya taifa.

4.

Sopoka mingi na usisadiki ma sauti mbaya na masimango ile wanasema watu wengine kupingana ya mkubwa yako, kwa sababu mara mingi watu wa bure wanachukia na wanahukumu

wakubwa ya inchi yetu. Ni zambi mnene kama unachukia ao unasimanaga mtu moja na tena ukubwa ni zambi kama huyu mutu ni mkubwa yako. Kwa ajili ya hii masimango inaonekana ya kama hakuna sifa na heshima ya watumishi mbele ya mkubwa yao. Kisha itafata funjo na kelele, inayeiko sababu mnene ya ushirika yetu.

5.

Kama mkubwa yako atakufokea ao atakulipiza, uvumilia hii ulipizo na uvumilia. Kama hii ulipizo ni haki, basi unalipizwa stahili katika matendo yako. Juu ya ninyi, basi, unasirika? Kama malipizo haina haki na hii mara fanya mara ingine uvumilia na sadiki ya kama inakuja toka Mungu kwa ajili ya zambi yako.

6.

Kwa sababu mkubwa yako anasubuka taifa yake, nikusema na kwa weye, na huyu anaomba saidio na nguvu juu ya kupita makizimbirio na materso yake. Basi, omba kwa Mungu na weye kwa mkubwa yako juu ya kumuangazia Bwana na kumusaidia na kumupatia neema yake. Kwa hivi anasema Mtume: «Basi ninaona mbele ya maneno yote, kuomba, na kusihi, na kuombea, na kushukuru kufanyike kwa ajili ya watu wote; kwa wafalme, na kwa wote wenye mamlaka, tuishi maisha ya kimya na salama, katika utawa wote na upole» (Barua ya kwanza kwa Timoteo 2, 1-2). Furaha ao mateso ya taifa moja inatoka ya mkubwa yake, sawa vile toka kichwa inatoka afya na utengo nzuri ya mwili.

Basi, sopoka. Usihukumu mkubwa yako kwani itafika bio pa kichwa yako uhukumu haki ya Mungu, sawa vile ilifanyikwa hii mambo kwa watu Datani na Avironi (Kutoka 16, 31).

## Ma kazi kupaswa ya wachungaji ya roho

Kama tunasema wachungaji tunasikia wa Askofu na wa padri ya kanisa yetu. Jina ya muchungaji inatuonyesha wale watu wanayechunga kundi ya wa Kristiani ya Kristu, nikusema wale watu aliwaumba Mungu katika Mufano wake na aliwauza na Dama Yake. Basi, sopoka hii ma sauti yangu sasa nitakuambia, mupendwa wangu muchungazi.

1.

Hii kazi na mamlaka hasipaswe kuomba weye wa pekee, lakini inapaswa kuongolea mwito ya Mungu.

2. Wakati utaitwa mu kazi ya kuchunga wa Kristiani ya Kanisa, uwaza kama utaweza kunyanyua hii jukumu. Kama usiweze, usikaribie, kwani ni hatari kuanguka mu gehena. Huyu anayetaka kusaidia watu wengine kwa uzima ya roho, inapaswa ya kwanza kusaidia na kusafisha maungo yake. Huyu anayetaka kufundisha watu wengine, ya kwanza kabisa atafundisha fazila kwa maungo yake. Huyu anayetaka kusaidia watu wengine mu uzima ya Kristu, inapaswa huyu mumoja ya kwanza kuwa mufazili katika Kristu. Huyu anayetaka kuwa mkubwa na mwongozi ya watu wengine ku uzima ya milele, inapaswa huyu mumoja kutembea hii njia. Inapaswa kuwa nuru ya dunia na chumvi ya inchi. Huyu anayetaka kuwa watu wengine wa safi na wenye bikira, inapaswa ya kwanza huyu mumoja kuwa musafi na mubikira. Huyu anayetaka kuhukumu watu wengine mu zambi, inapaswa huyu kabisa kuhukumwa toka moyo yake. Na hivi inapaswa kufanya juu hapana kusikia hii sauti ya Kristu: «ee mungaga ponyesha maungo yako».

Uwaza hii yote, mupendwa wangu, na usikaribie hii uzito na jukumu kama ni yulu ya ma nguvu yako.

3.

Muchungaji ya Kanisa inapaswa kushauria bila kusimama watu na kuwaongoza mu toba ya kweli na kupanda ndani ya ma roho yao boka na mapendo ya Mungu. Inapaswa kukumbuka kwa wenye zambi Uhukumu matata ya Mungu, kuwashauria wenye kutubu na rehema ya Mungu na utulivu ya Evangelion na kutosha mafundisho ya wongo toka ma roho yao na kuzimisha mafundisho ya ma ndini ingine.

Fundisho yake inapaswa kuibeba toka ma Kitabu takatifu ya Agano la kale na Agano Jipya, toka neno ya Mungu inayeiko ndani ya hii ma Kitabu.

4.

Makao ya fundisho ni Kanisa takatifu. Lakini ma fasi yote, pahali iko namna kusanyikwa waminifu, anaweza muchungaji kuwafundisha, kwa wakati yake. Tukona mufano ya Bwana Yesu, aliyekuwa muchungaji mkubwa. Yule hapana paka mu Hekalu ya Solomono, lakini na ma nyumba, na ma jangwa na ma fasi ingine alifundisha watu. Muchungaji mwenye kusopoka na mwenye akili atapata wakati nzuri na atatayarisha akili yake atafundisha ninyi. Kwa mufano, wakati anaikaa pa meza ya kula anaweza kufundisha wa ndugu wake juu ya ufalme ya Mbinguni.

5.

Kila sauti unaipenda kusema kwa watu inapaswa ku mbele kuiwaza nzuri na kisha utawaambia. Chakula ya kwanza inatayarishwa, kisha wanaweka ndani chumvi na kisha wanaikabula mu meza utamu. Vile muchungaji inapaswa kutayarisha na chakula ya Mungu, neno takatifu ya kwanza ndani ya roho yake, kuitayarisha na chumvi ya hekima katika Mungu na hivi ataiweka pa meza ya roho kwa watu wenye njaa neno ya roho. Paka vile ni namna kutumika na kitumaini juu ya wokovu ya wa Kristiani wake.

6.

Ma Sehemu ya watu ni  wa wili: Wale wanaishi bila boka ya Mungu na wale wanasikia kihu juu ya kupata amani ya roho na utulivu. Basi, Muchungaji  ya Kanisa eko na kazi ya kupaswa kuhubiri juu ya hasira ya Mungu na Uhukumu Yake kwa wale wanayeishi bila boka ya Mungu, juu ya kuwaongoza mu kitubio na kuvunjika ya roho. Kwa wale wanasikia hali ya zambi yao, atawatoa utulivu ya Evangelio: «Neno hili na aminifu, na linastahili kukubaliwa na watu wote, ya kwamba Kristu Yesu alikuja kwa dunia kuokoa wenye zambi; na mimi ya kwanza wao» (Barua ya kwanza ya Timoteo 1, 15).

7. Uhukumu ya muchungaji mbele ya wa Kristiani yake inapaswa kufanyikwa na namna ingine mbele ya watu wote na namna ingine mbele ya kila Mukristu.

Wakati muchungaji anahukumu waminifu wote pamoja iko namna kuwa kuliko makari na sauti nguvu, juu ya kumusikia hawa wenye zambi kusikia boka na tetemeko ya roho yao, kulamuka toka pumziko ya zambi yao. Hii namna tunaiona na kwa mahubiri ya wa Nabii na wa Mitume. Lakini, wakati unataka kuhukumu paka moja mwaminifu juu ya zambi yake moja, umuambia hii mambo na pasopo mingi na akili mingi na sopoka kutunza kilonda na hapana kufungula kabisa mingi hii kilonda ya roho yake. Tafuta wakati nzuri juu ya kumushauria na namna utamu. Wakati nzuri ni saa ya Maungamo. Ile saa unaweza kumuwambia hii yote ma shauria unataka kumusema hapana na hasira na kisilani. Inapaswa kusikia huyu mwaminifu ya kama unamupenda kweli na unataka kweli wokovu yake.

8.

Wakati watu filani wanazulumu, weye inapaswa kujua nzuri ya kama ni lazima kunyamaza. Inapaswa kuhukumu ma fasi yote na daima mazulumu yao na kinywa yako, kwani aipaswe kufana kama imbwa moja bila sauti, na hasifokee ile saa wa mwivi wanaingia ndani ya nyumba kunyanganya ao ile saa ma nyama makali ya pori wanaingia mu kundi ya kondoo juu ya kuwauwa.

Mupendwa wangu, simama bila kutenga mu kazi yako na timiza malako yako kama muchungaji ya ma kondoo wenye akili, bila kuwaza ya kama watakufukuza ao watakuhukumu watu mbaya. Ukona mifano ma nabii na wa Mitume na wa Askofu watakatifu ya Kristu.

9.

Usichekelee ao usifunike makosa ya wakubwa na watajiri, wenye wanaishi na majivuno na zambi. Na, kama walifanya na tendo moja kubwa, sopoka juu usiharabisha kazi yako kama mwalimu ya roho na utaonyesha  udanganyifu mbele kwake. Usiogope kuhukumu mara moja kila kazi kibaya, kukikiri fundisho ukweli ma fasi yote na daima na kuhubiri neno ya Mungu, kwani ulitumwa kufanya hii kazi. Iko lazima kusikia hawa wote ya kama  weye uko muchungazi na mwalimu yao, ambaya atajibu mbele ya Mungu juu ya wokovu yao.

10.

Usihubiri juu ya kukutukuza na ma sauti butamu watu wengine ao ya kupendeza kwa watu wengine, kwani hivi unaiba neema ya Mungu. Neno ya Bwana ilijipata kwa wokovu ya wa nafsi na utukufu ya Mungu. Hii kadiri iko na Kuhubiri. Kama weye unamaliza nzuri kazi yako kwa wokovu ya waminifu, paka hivi utakuwa na utukufu, bila kuiomba, lakini hapana toka ya watu wote. Waminifu wenye wazuri na wenyekupenda Mungu, watakupenda na watakutukuza. Kupindua wenye mbaya na wavuvi watakuchukia na watakusema ma sauti mbaya. Hakuna namna kupendeza watu wote kwa wengine.

11.

Kila sauti na shauria unasema kwa waminifu wako ya kwanza weye inapaswa kuimaliza kwa maungo yako. Kama uzima yako ni pamoja na ma neno yako, paka hivi utasaidia wa ndugu yako na utafundisha ya kwanza kwa matendo na kisha kwa ma neno ya Mungu. Kwa ajili ya cheo yako uko yulu na wanakuona ma macho ya watu wote. Wanaangalia unasema ninyi na unafanya ninyi. Basi, fundisha ma fazila katika neno na tendo juu ya kusikia watu toka kinywa yako neno jema na kuona na picha ya uzima yako nzuri na hivi watapata faida mingi mu uzima yao. Mupendwa wangu, uwe nuru mbele ya watu yako katika fundisho na uzima yako. Uwe chumvi, uwe mwongozi ku inchi wa milele na hapana kama nguzo moja mu njia. Uwaonyesha njia, lakini tembea ku mbele weye mumoja. ya kwanza chunga weye maungo yako na kisha waminifu yako. Uwafundisha mapenzi ya Mungu, lakini ku mbele utaimaliza weye mumoja. Uwaita mu Karamu kubwa na wa milele ya wenye heri, lakini anagalia ya kwanza kufika pale weye.

12.

Bila saidio ya Mungu hata makangamano moja hata tendo moja hakuna namna kutembea nzuri na maendeleo. Kwa hivi muchungaji ekona kazi kupaswa kuomba nguvu kwa Mungu juu ya maungo yake na kundi ya waminifu yake.

*****

Ma barua wa wili ya Mtume Paulo kwa Timoteo na kwa Tito wanafatula na ajabu muchungaji wa kweli ya Kanisa yetu; ma fazila ma nani wanamupamba na anapaswa kusopoka ngapi mu uzima yake na mu kazi ya wokovu ya waminifu yake. Soma na weye hii ma shauria ya Mtume Paulo na utasikia hii sauti yangu. Ma shauria ya Mtume ni ma stahili ya kusopoka mingi. «. . . Basi imemupasa mwangalizi asiwe na laumu, mume wa muke mumoja, mwenye kiasi, mwenye akili, mutu wa utaratibu, mukaribishaji wageni, mwenye kujua kufundisha; si mutu wa kulewa na mvinyo, si mupigaji, , si mwenye tamaa ya feza; lakini awe mupole, si mutu wa ugomvi, asiwe mwenye kutumani; mwenye kusimamia vema nyumba yake; akitiisha watoto wake kwa utaratibu wote» (Barua ya kwanza kwa Timoteo 3, 2-4).

## Ma kazi ya kupaswa ya watoto ya roho

1.

Kwa sababu, Mukristu yangu, muchungaji, anahubiri neno ya Mungu, weye inapaswa kupokelea hii ma sauti yake na kuimaliza. pa hii mambo Mtume anatuwambia: «Tiini wenye kuwaongoza ninyi na kuwanyenyekea; maana wao wanaangalia kwa ajili ya roho zenu, kama watu watakaotoa hesabu, ili wapate kufanya hivi kwa furaha, wala si kwa huzuni: maana hii itakuwa kwenu pasipo faida» ( Kwa wa Ebrania 13, 17).

2.

Muchungaji ni mutume ya Mungu, anayekuja akuonyesha njia ya wokovu. Anakuja akukuita kwa jina ya Mungu mu Ufalme wake wa milele. Kwa hii neno, basi, umuheshima kama malaika ya Mungu anayekutangaza ma bintu makubwa na anakuita kwa ile. « Yeye anayewapokea ninyi, ananipokea mimi, naye anayenipoke mimi anamupokea yeye aliyenituma» (Matayo 10, 40).

3.

Kwa sababu muchungaji anasubuka juu ya faida ya waminifu wote, katikati yao uko na weye, inapaswa kumupenda kama baba na musaidizi yako na kumuonyesha shukrani yako. Unamuita baba. Unafanya nzuri. Kwa sababu yeye anakuzala katika roho, sawa vile wa Kristiani wote, lakini hapna kwa maisha hii, lakini mu uzima ya milele. Basi, umupenda na weye kama baba yako. Umupenda baba yako aliyekuzala. Lakini kupita mingi inapaswa kupenda baba yako ya roho.

4.

Huyu anasubuka na anasaidia watu wote na weye. na weye usimusahabu ma lazima yake. Umusaidia, umutimiza kila kintu yeye eko na lazima juu ya kutumika nzuri tendo yake. Hivi hii mapendo katikati yenu na wema haitambakie bila maendeleo na faida ya roho.

5.

Mu dunia ni watu mengi wazaifu, wenye awatake kusikia mashauria na malipizo ya wachungaji wao na wanaishi katika mapenzi yao. Hawa wanatafuta na wanazambalala ma fasi yote matusi na masimango kupingana ya wachungaji wao. Basi, wakati utasikia moja sauti yao kibaya kupingana ya muchungaji yako, usisadiki. Funga kinywa yako na usiseme kintu kimoja kwa watu wengine. Kama utasema, utafanya zambi uzito, kwwani utaleta kwazo kwa wa ndugu wengine. Kama ni matata kuhukumu mtu moja ya bure, ngapi ni kibaya kabisa kama utahukumu na utasimanga muchungaji wako! Hii masimango wanazala funjo mnene katikati ya watu. Wanazala uzarau na kukataa utii mbele ya wachungaji wao na hivi machoko ya mkubwa yao inaenda kwa bure na bila matunda ya roho.

Sopoka hii sauti nilikuwambia sasa. Macho yako kamata ya kufungula kila siku na daima. Chunga nafsi yako toka ma sauti mbaya inayezambalisha kupingana ya muchungaji yako. Lakini, kabisa sopoka weye, na usisema na usihukumu baba ya roho yako, kwa sababu utasirika Mungu na Yeye atakulipiza.

6.

Kama utaona makosa filani, mu uzima na kwa watu wenye heshima, usiajabu na usiache kuingia kwazo ndani ya roho yako, lakini uwaza ya kama muchungaji ni na huyu mtu sawa sisi wote.

7.

Kwa sababu muchungaji ya Kanisa niko mbele ya mateso mengi na tena kupingana yake wanasimama kama wa adui shetani na watumishi mbaya yake, kwa hivi na yeye eko na lazima ya saidio ya Mungu na nguvu ya Neema Yake. Sawa vile watu wote ya dunia, vile na weye ukona kazi kupaswa kuomba ya kusaidia baba yako ya ho.

Furaha na heri ya nyumba inatoka ya mkubwa ya nyumba, ushindi ya wa askari inatoka ya jemadari mzuri na safari nzuri ya chombo moja inatoka ya mukubwa mwogozi yake. Basi, omba kwa Mungu juu muchungaji ya kanisa yako kuwa mwenye akili na mzuri na hivi ushirika wa Kristu itaendelea mbio ku mbele.

8.

Kama kwa mufano muchungaji hasimaliza hii ma sauti na shauria anasema na anafanya kupindua, ile saa kumbuka ma neno ya Kristu, ambaye alisema kwa hawa wachungaji: «Waandishi na Wafarisayo wanaketi katika kiti cha Musa; basi maneno yote wanayowaambia ninyi kutenda, muyashike na kuyatenda; lakini musitende kwa mufano wa matendo yao; kwa maana wanasema, lakini hawatendi» (Matayo 23, 2-3).

## Ma kazi ya kupaswa katikati ya mume na muke

1.

Mwanaume na mwanamuke inapaswa kuowa na mapenzi yao na masikilizano yao. Kwa hivi padri mbele ya kufanya Ibada ya Ndoa anauliza hawa wa wili: « Munakuja mu ndoa na mapenzi yenu na masikilizano wenu? »

Uzima yao bila masikilizano yao pamoja wa wili haina ya nguvu. Kwa hivi wa padri, wenye wanaona ya kama hakuna masikilizano ya hawa wa wili watu, lakini wanafanya Ibada ya Ndoa yao, wanakosa uzito mbele ya Mungu. Hawa wa padri katika Makanuni takatifu inapaswa kulipizwa, kwa sababu kwa ajili ya hii si masikilizano, inazaliwa katikati yao kila kintu kibaya.

2.

Ninyi wanayekuja mu Fumbo ya ndoa, inapaswa kuonyesha moja kwa mwingine mapendo na imani mpaka mwisho ya uzima yao. Haipaswe hata mwanaume kumuacha bibi yake, hata bibi kuacha bwana yake mupaka mwisho ya uzima yao. Sawa vile walipatia malako na walisikilizana ile saa ya ndoa yao, vile inapaswa kumbakia bila kuharabisha hii ndoa yao mpaka mwisho yao.

3.

Mwanaume na mwanamuke inapaswa kusingi mapendo yao pa fazila; hapana pa zambi na matakio mbaya yao. Wakati kwa mufano, mwanaume anaona kwa bibi yake moja kosa ao zwezo kibaya, inapaswa kumushauria na namna nzuri na bibi inapaswa kujitii. Vile na, kama bibi ataangalia moja zambi ao zwezo kibaya ya bwana wake, inapaswa kumwambia na yeye kutengeneza kosa yake. Vile mapendo yao itakuwa nguvu, bila kupasula na umoja katikati yao na heri yao itakuwa na usingi nguvu. Hivi, watafurahi kwa maendeleo yao mu fazila na uzima wa heri yao na waotto yao; na neema ya Mungu itapumzika yulu yao.

4.

Mutume Paulo anasema kwa wenye ndoa hivi: «Muke hana amri juu ya mwili wake mwenyewe, lakini mume wake: vile mume hana amri juu ya mwili wake mwenyewe, lakini muke. Musinyimane, ile mumepatana kwa wakati, hata mupate siku za kufunga na kuomba, kisha kujeni pamoja tena. hata shetani asipate kuwajaribu ninyi kwa sababu ya kupunguka kiasi» (Barua ya kwanza kwa wa Korinto 7, 4-5). Hii sauti ya Mtume Paulo kila mutu anaweza kuisikia.

5.

Tena inapaswa kusikia ya kama weko wa Kristiani. Wanasadiki kwa Jina takatifu ya Mungu. Wanamuita na wanaomba Kwake, wanapumunika Komonyo Takatifu. Basi, aipaswe kuishi sawa wenye wasipoimani.

6.

Mwanaume aipaswe kuona bibi yake kama mutumwa yake, lakini kama musaidizi yake; na bibi inapaswa kutii kwa bwana yake, sawa vile anatufundisha na Mtume Paulo: «Ninyi wake, mutii waaume wenu, kama kutii Bwana». Na kidogo chini anasema: «Na muke asikose kuheshimu mume wake» (Wa Efeso 5, 22, 33).

Mu barua ingine mara ingine anandika: «Wake mutii waume wenu kama inavyopendeza katika Bwana» (Wa Kolosayi 3, 18). Kama mwanaume na mwanamuke yake weko na sikilizano mu fazila, hivi maisha yao ni wenye heri na wenye furaha na hivi daima wataishi na mapendo na amani. Paka hivi iko namna kuleta mu uzima yao uzima wa heri.

«Tazama, ni wema na ya kupendeza sana kwa ndugu kukaa pamoja kwa umoja» (Zaburi 1133, 1), anasema Nabii. Lakini shetani ni adui ya nafsi yetu, anakombana kuharabisha ma fazila vema na mapendo na ungano. Kwa hivi mwanaume na mwanamuke iko lazima kuvumilia ma saa ya makelele yao na kuvumilia moja mwingine katika mapendo.

7.

Kama moja katikati ya wili eko na mufano nzuri na mwingine ni mtu na mufano kibaya, huyu wa kwanza anavumilia, ananyanyua musalaba moja. Ile saa eko na lazima na uvumilia mingi; hivi atashinda daima kila zwezo kibaya.

8.

Historia inatuwambia juu ya wanawake mengi, wenye waliharabisha wanaume wao. Kwa hivi wanaume haina nzuri kuonyesha mbele ya wanawake wao ya kama hawakuwa na nguvu na wanawaacha kufanywa hawa wanawake wao kila kazi wanapenda. Iko lazima kusimamisha ma zwezo mbaya ya mufano yao juu hapana kuharabisha wote wa wili pamoja. Nyoka mu Paradizo ya kwanza alikaribia mwanamuke Eva na alimukokota kukataa kutii. Yule kisha alikokota Adamu na alimuongoza mu uharibifu. Hivi inafanyikwa na sasa: Shetani mumoja anakaribia mwanamuke, anamukokota mu fasi yake na kisha anakokota mwanaume yake matendo mbaya kwa ajili yake.

Ee Mwanaume, sopoka, usitimize mapenzi yoyote ya bibi yako, kwani yeye ataikaa pa kichwa yako na atakuongoza pahali fasi yeye anataka. Mwanamuke ekona daima mufano yake. Utamupenda mupaka ile fasi yeye hasiishi kupingana ya mapenzi ya Mungu. Yule bibi yako ataogopa weye, sawa vile anasema Mtume na hapana weye huyu. Huyu bibi atatii kwako na hapana weye kwake.

## Ma kazi ya kupaswa ya wazazi

Mtume Paulo anashauria wazazi hivi: «Lakini muwalee (watoto) katika azabu na maonyo ya Bwana» (Wa Efeso 6, 4); na anawashauria kufundisha watoto wao, sawa vile inapaswa kwa wa Kristiani. Wa Kristiani wote kwa Ubatizo Takatifu walizaliwa kwa uzima upya, takatifu na wa Kristu uzima na walilaka kutumika juu ya kufurahi Bwana katika imani na matunda ya roho. Lakini juu ya kuishi uzima safi wenye kubatiza na hapana kuanguka mu hali kibaya ya zambi na hivi watafata sauti ya Mt. Petro anayesema: «Imbwa amerudia matapiko yake mwenyewe, na nguruwe aliyeoshwa amerudia kugaagaa ndani ya matope» (Barua ya mbili ya Petro 2, 22), iko lazima azabu nzuri ya watoto, ile wakati ni mu kipimo udogo. Azabu nzuri ya kipimo yao udogo juu ya kusaidia watoto hapana kutelemuka mu njia ya zambi. Sisi tunaona na huzuni ya roho mingi watoto mengi, wenye wanarabishwa mu kipimo udogo yao. Na hii uharibifu iko na maneno uvuvi na uzaifu ya wazazi yao.

Wazazi mengi wanatuma watoto wao kufunda ma fundi mingi juu ya kuishi na makuta mingi mu uzima yao. Wengine tena wanapenda kufunda watoto yao ma lunga mageni na wanaripa makuta mingi. Lakini juu ya kusaidia watoto wao mu uzima ya roho, hakuna mafa hakuna mapendo yao, hakuna masubuko. Hawa wazazi wanazala watoto paka ya hii uzima na wanawagunga mulango ya uzima wa milele.

Mt. Yoane Krisostomo tazama namna gani anashauria wale wazazi, wenye hawapenda kufundisha watoto yao na ma nani ni matunda kwa ajili ya hii uzaifu na uvivu yao. «Wazazi, wenye hawasubuka juu ya azabu katika Kristu ya watoto wao, wananguka mu zambi uzito ya kuuwa watoto wao. Kwa sababu wenye wanauwa watoto wao wanachanisha mwili toka nafsi yao, lakini wazazi wenye uvivu wanatupa na mwili na nafsi ya watoto yao mu gehena. Lufu ya mwili hakuna namna kuitoka hata mtu moja ya hii dunia, wote watu watakufa, lakini lufu ya milele iko namna kujiepuka, kama itatoka uvivu na uzaifu ya wazazi. Lufu ya mwili itakuwa ya wakati kidogo, kwa sababu itakuja ufufuo na itafufua wa mwili ya watu wote, lakini lufu ya roho ya ma nafsi hakuna namna kutoka ya gehena, hakuna ufufuo ya nafsi kisha lufu ya mwili yetu. Kwa hivi wazazi musikieni kufundisha watoto wenu katika azabu na maonyo ya Bwana».

Mulimanji ya shamba yake, wakati anataka kupanda muti moja, anaifunga pamoja na bakora moja, inayeweka ndani ya bulongo. Hivi hakuna hatari hii muti kuitosha pepo nguvu na mvula. Tena mulimanji anaisafisha pempeni yake hii muti na mapendo mingi anaisaidia kukomea nzuri. Mufanye hivi na mweye watoto wenu wadogo. Mufunge ma roho yao kwa boka takatifu ya Mungu na hivi hakuna namna kutengwa toka matendo na waovu ya shetani na hawataanguka toka uzima ya utawa. Mutoshe na mukate ma nyasi inaotesha pempeni ya hii muti ya roho yao juu

hapana kuuwa mtu muzima, aliyebatizwa katika Ubatizo takatifu. Kwani tunaangalia ya kama, wakati wanakomea watoto, pamoja wanakomea na ma zwezo mbaya kama ma nyasi makari pembeni ya muti moja.

Basi, wapenzi wangu, mukateni hii mayani mbaya toka muti roho ya watoto yenu na; : «Lakini muwalee (watoto) katika azabu na maonyo ya Bwana» (Wa Efeso 6, 4); Wakati wataanza watoto wenu kujua ni ninyi kazi nzzuri na kibaya na mwenye mwanzezi kazi yenu kwa fundisho ya Mungu.

1.

Ya kwanza inapaswa kuwakumbuka kila wakati Ubatizo yao takatifu kwa ile walilaka kuishi na ufazili na kutumika na imani na mapendo Bwana mu zima yao yote na tena walilaka kuepuka ya kila zambi na uchafu.

2.

Muwaambia mara mengi kila wakati ya kama sisi wa Kristiani wote tunazaliwa katika mwili na kisha tunazaliwa katika roho kwa Ubatizo ya Mungu hapana juu ya hii uzima ya bure, hapana juu ya kupata ma sifa, utukufu na mali ya bure. Inakuja na lufu na hii yote bintu na mapendo ya hii dunia inaharabika lufu. Katika Ubatizo ya Kanisa yetu sisi tunazaliwa ya roho juu ya kuingina mu uzima ya milele. Uzima yetu mzima pa hii inchi kutoka uzalio yetu mpaka lufu ni njia ya kutembea mu inchi ya milele, sawa vile na Mungu alitulaka.

Mukumbukeni kwa watoto wenu, hii ma fundisho ya kweli na hivi mutawasaidia hapana kufata ma zwezo ya hii dunia, lakini watafunda hekima ya milele na hapana hekima ya hii dunia.

3.

Mufundisheni watoto wenu, Mungu wa Kristiani ni nani na anaomba nini. Muwambieni ya kama Mungu hasipenda kila kazi kibaya na anaripa kila kazi kizuri. Kama sisi tusimuone, lakini Yeye anatuona, eko ma fasi yote, anaona kila tendo yetu, anasikia kila neno yetu. Basi, inapaswa kufunda juu ya kumuogopa na kufanya paka kila kazi Yeye anaipenda.

4.

Muwasaidia kufungula ma macho ya ma roho yao juu ya kuangalia Kristu mwenye tunamusadiki na juu ya ninyi Huyu alikuja mu dunia, aliishi, aliteswa na alikua pa Musalaba. Alikuja juu ya kutoka sisi ya ma zambi yetu na kupata furaha daima mu uzima ya milele.

5.

Muwafundisheni sheria ya Mungu. Muwambieni kwao ya kama sheria Yake inaomba sisi tumupenda Bwana na kila mtu bila machanisho; ya kama ma zwezo na zambi ni kupindua mbele ya sheria ya Mungu, na kila fazila ni pamoja na sheria yake.

Sheria ya Mungu itawaulinzi na hivi wataishi mbali ya kila zambi na wataishi na ufazili, sawa vile walijilaka kwa Ubatizo Takatifu. Huyu anayeishi na namna ingine, nikusema kibaya, anasema wongo na anakataa kutimiza malako yake ya Ubatizo. Na, kama hasitatubu kweli na hasitatengeneza uzima yake, atasimama mukosefu mbele ya Uhukumu ya Kristu ile siku ya Uhukumu.

6.

Muwafundisha watoto wenu juu ya uzima ya mwisho, juu ya mauti, uzima ya milele, uzima ya gehena na hivi itazaliwa ndani yao boka ya Mungu. Na hii ma fundisho na ingine mutaweza kama mazimba kupatia chakula nzuri kwa watoto wenu juu ya kukomea na utawa na boka ya Mungu.

*****

Watoto wanamiita «Wazazi». Basi, inapaswa kuwa wazazi wa kweli. Muliwazaliwa watoto yenu katika mwili; basi, muwazaliwa sasa na katika roho. Muliwazaliwa kwa hii uzima; sasa muwazaliwa na kwa uzima ya milele.

Wa Kristiani wapenzi wangu! Na mweye na watoto wenu mutasimama mbele ya kiti ya Kristu ile siku juu ya kujibu juu ya uzima yao. Yule atamiuliza hapana kama mulifundisha watoto wenu ma fundi ya kuachana, kama muliwasaidia kusuburia ma lunga mageni, lakini kama muliwafundisha kuishi maisha katika Kristu.

Watoto wadongo wanasopoka kupita mingi mufano ya wazazi yao, na hapana ma shauria yao. Kwa hivi, kama munata watoto wenu kufanyika wa Kristiani wazuri na wenye utawa, inapaswa kuwa na mwenye ya kwanza wazazi wenye utawa na wazuri. Kama mukona mufano nzuri mutaweza kufundisha watoto yenu katika azabu na maonyo ya Bwana Yesu. Vile na mweye na watoto wenu mutatukuzwa toka Bwana wetu Yesu Kristu na wokovu ya milele.

## Ma kazi ya kupaswa ya watoto

1.

Moyo umoja inajulisha kila mtu ya kama inapaswa kuheshimiwa na kupenda wazazi wake. Wa Pagano walifundisha na waliandika ma sheria yao ya kama kila mtu inapaswa kisha Mungu kuonyesha sifa yake mbele ya wazazi yake. Lakini na neno kimungu inatuwambia kusifu wazazi: «Heshimu baba yako na mama yako». Basi, ee Mukristu, onyesha kila sifa kwa wazazi wako juu ya « siku zako zipate kuwa nyingi katika inchi Bwana Mungu wako anayokupa wewe» (Kutoka 20, 12). Kama unakataa kusifu wazazi wako nani mwingine utamusifu kuliko?

2.

Kwani wazazi ni wafazili wako wakubwa, onyesha kwao heshima na shukrani. Kumbuka maumivu na machoko hawa walipita juu ya kukukomea. Inapaswa kujua ya kama hakuna namna sisi kurudisha hii mafazili na masaidio yao. Tukona sisi ma ndeni mnene mbele yao na hakuna namna kuirudisha kwao. Onyesha, basi, mapendo na wema yako mzima kwa ajili ya matendo yao mazuri waliyetoa kwako.

3. Inapaswa kuwatii wazazi wako: «Watoto, mutii wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki» (Wa Efeso 6, 1). Na mu fasi ingine: «Watoto, mutii wazazi wenu katika maneno yote, maana neno hili linapendeza katika Bwana» (Wa Kolosayi 3, 20).
4. Bila baraka na ruhusa ya wazazi wako usianze kufanya hata kazi moja, lakini inapaswa kuwauliza, kuomba ruhusa na uwazo yao kwa sababu hivi utaonyesha ya kama unawaheshimana unawapenda kweli. Kama usitafanya hivi kazi yako haitatembee mbele.
5. Usiseme na usifanya kazi moja ya haya mbele yao, kwa sababu hivi inakuonyesha na imani na sheria ya Mungu.
6. Sopoka mingi usiwasikitika na ma sauti mbaya. Suburia na wao na uwajibu kwa kila ulizo yao na mapendo na heshima na sifa.
7. Wakati wanakulipiza ya mambo moja, ile unaijua ya kama uko mukosefu, famia na unyenyekevu kosa yako na vumilia na upole hii malipizo. Wanakulipiza juu ya kutengeneza kosa yako na kufanyikwa kuliko muzuri. Kama unazania ya kama usikufanya kosa na moyo yako inakuonyesha ya kama ukona haki, uwaambia na heshima na ma sauti mazuri ya kama uko musiyekosa.
8. Usiwaacha kwa kila mambo na mateso yao, lakini uwasaidia na tumika, kabisa mu kipimo ya uzee yao. Kumbuka, hawa walichoka ngapi karibu yako na walikusaidia ya kukomea nzuri; sasa weye fanya nguvu kuonyesha mapendo na saidio yako mbele kwao.
9. Kama utaangalia makosa na ma zwezo yao mbaya-kwani iko namna kuonekana hii makosa na kwa watu wazuri-weye zibiria hii makosa yao na unyamaza. Tena, kama utaona na kazi moja inayeleta kwazo, sopoka mingi na usiwahukumu na usiseme hii kosa ao zambi yao mbele ya watu wengine. Usifate kwa ili mambo, mufano ya mtoto ya Noe, aliyeitwa Hami, ambaye, wakati aliona baba yake bunji, alienda kusema na kwa wa ndugu yake. Fata weye watoto wengine ya Noe, wenye walibeba nguo moja na walienda na walifunika mwili bunji ya baba yao (Mwanzo 9, 22-28). Na weye, kama utaona kintu kimoya kibaya kwa wazazi wako, acha na uisahabu na sema ya kama usiione.

10. Kama utawaleta huzuni ndani ya roho yao kwa ma sauti na mufano yako kibaya na kisha moyo yako itakuhukumu, tena kama, utaona uchungu pa uso yao, mara moja wende mbele yao na omba hurumia. Fanya hivi na usitaanguka kwa uhukumu ya Mungu. Kama inapaswa kuomba hurumia ya kila mtu kwa mwenye tunamulete huzuni ya roho na tusikilizane na huyu, sawa anatuhamuru na Bwana Yesu, ngapi kuliko mingi ni lazima kusikilizana na wazazi wetu, wenye inapaswa kuwasifu na kuwapenda kuliko ya kila mtu mwingine?
11. Tena na wa Pagano wanaandika ma sheria yao na malipizo wenye makali kwa wale watoto hawapende wazazi wao. Kuliko mingi inafanyikwa hii mambo mu Sheria ya Mungu. Pale mu Sheria Yake iko ya kuandikwa malipizo matata juu ya watoto wenye wanakataa kutii wazazi wao. Yeye anayetukana baba yake ao mama yake, hakika atauawa» (Kutoka 21, 17). Hawa watoto, ao kusema kupita nzuri, mabilulu ya ushirika ubinadamu- Mungu anawachukia na watu ya dunia.

Ni zambi mnene na hakuna shukrani kama mutu moja anaonyesha hali kibaya mbele ya wasaidizi yake na kwa wale walimuzala. Basi, sopoka, mingi, Mukristu yangu, na hivi usitakokota yulu yako malipizo ya Mungu. Kisha Mungu hakuna musaidizi na mufazili yetu, paka wazazi wetu. Na iko kazi kibaya na matata, kama mutu moja hasipende kuonyesha shukrani na «aksanti» moja kwa wazazi wake

12. Inapaswa kujua nzuri, ya kama hii mufano utaonyesha weye kwa wazazi wako hivi na watoto wajko wataonyesha mufano mbele yako, kwa sababu hivi inatuwambia na sauti ya Kristu: « Na kipimo kile munachopimia mutapimiwa» (Matayo 7, 2).

## Ma kazi ya kupaswa ya Watajiri

Mali ni zawadi ya Mungu-«Inchi na kujaa Kwake ni mali ya Bwana» (Zaburi 23, 1). Ee Mukristu wangu, mali inakupatia nyakati nzuri hapana paka juu ya kutengeneza mambo yako, lakini kusaidia na wamaskini, wandugu yako. Utumie toka mali yako na umushukuru Mungu, lakini mara moja uwaza na wenye maskini na uwasaidia. Hii ni kazi nzuri juu ya kutumia mali yako. Uwaza ya kama usiwe weye mkubwa ya mali yako, iliyekupatia Mungu, lakini mujukumu ya kutengeneza nzuri hii mali. Na mbele ya Mungu utajibu na utamupatia jibu ya kila kazi ao uharibifu ya hii mali.

Neno takatifu ya Mungu inatukuza na anasema wa heri kwa ninyi wote ni wenye rehema kwa maskini: « Heri wenye rehema; maana wao watapata rehema» (Matayo 5, 7). «Heri ni yeye anayekumbuka masikini» (Zaburi 41, 1). Matendo ya rehema wanatukuzwa toka Mwamuzi wa Haki Mungu wetu mu fasi yote ya Madiko Takatifu. Basi, kama unataka, Mukristu wangu, kupata heri ya milele, fanyika mwenye rehema na mutajiri ya kusaidia maskini.

Ukona mengi? Patia mengi. Ukona kidogo? Patia kwa maskini kidogo, lakini inapaswa kupatia toka roho yako na katika mapendo. Rehema inaonekana hapana kama ni mingi, lakini kama huyu mtu anasaidia na mapendo ya roho yake; «kwa sababu Mungu anamupenda yeye anayetoa kwa furaha» (Barua ya mbili kwa wa Korinto 9, 7). Sasa unapatia kwa mikono ya wa maskini, lakini utabeba kuliko mara mia (100) ya Mikono ya Kristu. Basi, patia. Usiogope. Hasitapotewa matoleo yako, kwani Bwana Yesu analaka akupatia ma zawadi mengi kwa sababu hasiseme wongo.

Wa Kristiani mengi wanajua ya kama rehema iko na malipo mingi lakini wanachunga ma mali yao kama wa zamu wasipokulala. Wengine wanaharabisha mali yao ma zambi na matakio mbaya ya mwili na maisha yao. Ma zambi ya kila furaha ya dunia wanaharabisha makuta ya wale watu wanafurahi. Wale wanachunga mali yao ao wenye wanaharabisha mali yao kwa zambi ya mwili watapotesha sauti wa heri ya Bwana Yesu na watateswa kama watumihsi wabaya na wazaifu. Ee Mukristu, basi, chunga nzuri mufano yako na ogopa ma sauti ya Mungu!

Mali kwa mikono ya kila mtu iko namna kumupatia faida ao uharibifu. Inaleta faida kama inajitumia katika mapenzi ya Mungu. Inaharabisha mtu kama huyu anauza kila kintu paka ya maisha yake na hasipende kusaidia na wa ndugu wake. Basi, ndugu wangu, fanyika mutumishi mwaminifu ya bintu ya Bwana  na hivi utakuwa kweli mutajiri.
Kama ulifanya mali na namna ya uzulumu, bio, uikabula kwa maskini juu ya usihukumiwa kwa Ufikisho ya Mbili ya Mungu mu dunia ya kuhukumu watu wote. Fata muto zakodi mkubwa Zakayo, aliyeonyesha Bwana Yesu Kama mufano nzuri mbele ya watu wote. Ni kuliko nzuri kuishi mtu moja ndani ya usikini na hapana ndani ya mali aliyepata na uzulumu na namna kibaya. Basi, kabula unataka ninyi na kaburia mali ya uzulumu na hanahaki. Amini ya kama, kama utafanya hivi, Bwana asitakuacha, lakini atakupatia yoyote bintu uko na lazima. Huyu mwenye  hasiacha ma ndege na anawapatia chakula yao, sasa ataacha kiumbe yake?

*****

Wa maskini, wenye wanapokelea huruma moja, inapaswa kushukuru  na  Mungu, anayewaonyesha rehema Yake na mbele ya watu, wenye wanawasaidia. Kwa sababu huyu murehemu ni mustahili ya kila sifa na mapendo.
Wa masikini inapaswa kukumbuka hawa wanawasaidia kwa maombi yao kila siku. Kama watasahabu wa masikini kuwakumbuka na ma sala yao, hii rehema umoja inapanda mbinguni na bila sauti, lakini bila kusimamisha, inaomba kwa Mungu kuliko mingi ya kila mtu.

## Ma kazi kupaswa ya wenye biashara

Wenye biashara mengi pamoja na bintu yao wanauzisha na moyo yao na pamoja na moyo wanauzisha na nafsi yao na pamoja na nafsi yao wanauzisdha na wokovu yao  wa milele na hivi wanabeba gehena. Kwa hii sehemu ni hawa watu:

1. Ninyi wenye wanauzisha kintu kimoja ya kuoza ya kama ni ya nzuri, kwa mufano wanauzisha nyama moja ya kama ni wa afya na muzuri, lakini iko mugonjwa.
2. Ninyi wenye wanauzisha kintu kimoja kwa fasi ya ingine kwa mufano wanauzisha moja rikalasi na wanasema ni diamand.
3. Ninyi watu wanauzisha kintu kimoja na bei kuliko mingi.
4. Ninyi watu wenye wanachanga kwa mufano vinyo pamoja na maji, ao chumvi na buchanga juu ya kuwa kupita uzito na hivi watabeba makuta mengi.
5. Ninyi watu wanalaka kwa Jina ya Mungu na wanasema wongo juu ya kuuzisha bintu yao.

Hawa watu  wanafanya zambi kupingana ya amri ya Bwana «Usiibe» (Kutoka 20, 15); na zambi yao ni kupita mingi kama wanauzisha bintu yao, bila hata kiloko uhukumu ya moyo yao. Kama hawatasimama hii tendo yao uzulumu, watasimama mbele ya Uhukumu ya Kristu kama wa mwivi na wanyanganyi.
Basi, Mukristu wangu, angalia unauzisha ninyi na namna gani unaiuzisha juu ya usiuzishe wokovu wako wa milele. Wakati unauzisha kintu kimoja, sikia mbele na sauti ya moyo yako na chunga  daima hii sauti inakuonyesha ninyi na hivi usitapotesha pamoja na moyo  nafsi yako. « Kila mutu anayetaja jina la Bwana aache uovu» (Barua ya mbili kwa Timoteo 2, 19).

## Ma kazi ya kupaswa wayengaji na watumishi yao

Na watumishi na wakubwa yao ni namna kuanguka ma zambi ya kuachana. Watumishi wanakosa, kama wanabeba ushahara nzuri, lakini hawapende kutumika katika moyo yao na watumika na uvivu na uzaifu na wanapotesha ma saa na ma siku yao. Hawa watumishi

wanaanguka mu kosa ya kuiba; ya kweli hawa ni wa mwivi. Wanasema wongo ya kama wanabeba ushahara kidogo na hivi wanaomba kupita mingi malipo ao wanaiba bintu mageni.

Tena wanakosa na wakubwa wao, kama wanakataa kuripa nzuri watumishi wao ao wanakataa kuwapatia hii ushahara walisikilizana ya kwanza. Hii zambi yao inapaza sauti daima mbele mbingu na inaomba kisasi toka Mungu. «Angalieni mushahara mulionyima walimaji wa mashamba yenu unalia, nayo malalamiko ya wavunaji yamefika masikioni mwa Bwana wa majeshi» (Yakobo 5, 4).

Kwa hivi, basi, huyu mushahara inapaswa kutumika na pasopo na katika moyo yake juu ya kuonekana malipo yake hapana kama kazi ya kuiba. Na mkubwa yake inapaswa kupatia kwa mutumishi yake yote malipo yake juu ya hapana kuleta kisilani na uhukumu wa haki ya Mungu.

## Kazi ya kupaswa ya hurumia

Iko namna mara mingi katikati ya watu moja kulanda ao kuchekelea mtu mwingine. Hii mambo ya sikitiko inatoka hata kwa ma fundi na waovu ya shetani, ambaye hasipende kuona mapendo katikati ya wa Kristiani, hata kwa ajili ya makosa na matakio mbaya yetu. Kama tunataka kufika katikati yao mapendo urafiki iko lazima kufanyika masikilizano.

Watu mengi wanasirika na wanachabula mukaribifu yao na hawasikia huzuni ya roho yao. Tena, sawa hakuna mambo, wanaenda mu Kanisa na wanaomba. Hatari ngapi inafuchama hii hali ya uzima yao! Kwa hivi huyu anayetaka kusikilizana na kuishi na amani pamoja na Mungu, inapaswa bila kuchelewa kusikilizana na mukaribifu yake. Kama hasifanye hivi mwenedo yake mu Kanisa na sala yake iko ya bure na bila kadiri. «Basi kama ukileta sadaka yako mazabahuni, na kule ukikumbuka ndugu yako ana neno juu yako, acha sadaka yako mbele ya mazabahu, uende zako, mwanza patana na ndugu yako, kisha rudi utoe sadaka yako» (Matayo 5, 23-24).

Unaona, Mukristiani wangu, ngapi ni lazima usikilizano pamoja na mukaribifu yetu? Mungu hasipokelee hata ma sala yetu, hata kitubio yetu, hata kintu ingine, kama tusipendane na ndugu yetu. Hata mingi anasifu mapendo na amani inayetawala katikati ya wa Kristiani.

Basi, sopoka. Kama utafananya kosa na utachabula mtu moja, usitoke. Uende bio bila kuchelewa, kusikilizana na ye juu ya usianguke mu hasira ya haki ya Bwana Mungu. Unamuchabula na sauti yako? Utasikilizana naye na sauti yao. Nyenyekevu na umuomba hurumia. Ulimuchabula na matendo mbaya? Sikilizana katika matendo pamoja naye; kwa sababu mauti inatembea bila kuonekana mukongo yetu na mara moja iko namna kutunyanganya. Basi, itafanyikwa ninyi, kama tutakufa na tutasimama mbele ya Kristu, lakini ndani yetu iko uchanisho na kisilani? Kama mambo moja itasamehewa na itatengenezwa ya hii inchi itakuwa usamehewa na mu uzima ya milele.

Basi, sikilizane, mupendwa wangu pamoja na adui yako, ile siku unatembea tena kwa hii njia ya maisha yako. Sawa vile ulifika kwa hii saa kumuchabula, hivi inapaswa kufika kwa saa kusikilizanna naye. Usiache hii hadisi ya kuitengeneza kesho. Usijue kama utalamuka kesho. Mungu, ni kweli ya kama alitulaka rehema yake, kama tutatubu; lakini hasitulake ya kama atatupatia na hii siku ya kesho. Sema kwa maungo yako kuharabisha ma sanamu ya majivuno ya roho yako, unamisha na unyenyekevu mbele ya ndugu yako na umuomba kitubio. Umuomba usamehe, hapana paka na midomo ya mwili, lakini na midomo ya roho yako. Tubu, utaabu, umubusu kweli na hapana katika udanganyifu.

-Iko namna kusema: Mimi nitaomba usamehe ya huyu mtu? Mimi niko mtu ya cheo ya yulu, lakini yeye eko na kizazi unyenyekevu.

Lakini na huyu ni mtu! Na huyu ni mutu na weye uko mtu. Mbele ya Mungu mwenye haki na huyu mkubwa na huyu mudogo tuko mu fasi na cheo umoja. Mungu anakata chuki na

hali kibaya katikati ya wa wili. Kwa Uhukumu Ile ya milele watasimama wote wa wili na huyu mkubwa na huyu maskini.
Unasema ya kama uko mkubwa na toka kizazi utukufu. Basi, tupa moja richo ndani ya ma kaburi ya wa babu yako na pale utaona iko wapi cheo na daraja ukubwa yako! . . .
-Unasema ya kama huyu naye mimi nilimuchabula eko na roho kibaya. Hii haina kazi yako kumuhukumu, kwa sababu usiweze kujua nani katikati wenu wa wili ni kuliko muzuri. Mungu anajua, ambaye anahukumu toka hali ya ndani yetu na hapana kwa ajili ya maisha yetu ile ya inje. « Bwana anajaribu mwenye haki; lakini nafsi yake inachukia mwovu, naye anayependa ukali» (zaburi 11, 5). Tena usijue mwisho yako, namna gani utakufa na namna gani atakufu huyu adui yako. Watu mengi wanaanza uzima yao na ufazili, lakini wanaishi katika zambi. Wengine mara ingine wanaanza mbaya, lakini wanaishi katika utakaso. Mwisho nzuri ni hii inayetengeneza yoyote mambo.
-Iko namna kusema, lakini huyu mutu hasitanihurumie, hata kama mimi nitakuomba usamehe.
Hapana! Unyenyekevu iko na nguvu mnene na inashusha tena na ma roho nguvu kabisa na magumu. Mungu anayependa unyenyekevu atasaidia. Unyenyekevu weye mbele ya ndugu zako na utaona nguvu ya unyenyekevu. Huyu ile saa bila shaka atakubatia na mapendo na furaha na atakubusu na mapendo. Kama hasitafanyikwa hii tendo, jukumu ni kwa huyu mtu anaye eko stahili ya bahati yake.
-Iko namna tena kuniambia: Huyu mtu atajivuna kwa ajili ya unyenyekevu yangu.
Hapana! haina kweli, kwa sababu huyu mukuona unyenyekevu yako na yeye atanyenyekevu. Lakini, kama atajivuna, majivuno yake itamushusha sana. Sawa vile anasema Bwana, « kila mutu anayejitukuza mwenyewe atanyenyekezwa» (Luka 14, 11). Lakini acha yoyote hii ma sauti yako. Huyu atafanya kila kintu anataka kuifanya, lakini weye fanya ile kazi inasaidia nafsi yako na hii amri anakuwambia Mungu.

*****

Kama mtu moja alikuchabula, inapaswa kumusamehe, kama unataka kusamehewa na weye toka Mungu. Na kitumaini hii utaomba kwa Mungu hivi: « Baba yetu. . . utusamehe deni zetu, kama sisi vilevile tunavyosamehe wadeni wetu» (Matayo 6, 12).
Unaona, Mukristiani wangu, matata ngapi ni hii mambno kama usisamehe ma kosa ya mukaribifu yako? «Kama ninyi munasamehe watu makosa yao, baba yenu ya mbinguni atawasamehe ninyi vilevile. Lakini kama ninyti hamusamehe watu makosa yao, Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu vilevile» (Matayo 6, 14-15).
Iko namna ndugu yako alikosa mbele yako, lakini weye ulikosa na unakosa ya kuendelea mbele ya Mungu. Yule ekona deni mbele yako, lakini weye sasa uko na deni mbele ya Mungu. Kama utasamehe mukaribifu yako, tangu ile saa, utaomba kweli na bila udanganyifu utasema hii Sala: Baba yetu uliye mbinguni. . . » Kama usitamusamehe toka ndani ya roho yako, sala yako hasitakupatia faida ya roho na inaonekana mbele ya Mungu kama zambi.
Unaona inaongoza wapi mtu moja hasira na kisilani? Basi, fukuza hasira, umusamehe mukaribifu yako na kuja kusema kweli na ustahili: «Baba yetu uliye mbinguni. . . . utusamehe deni zetu, kama sisi vilevile tunavyosamehe wadeni wetu» (Matayo 6, 12). Ile wakati itakupatia maondoleo ya zambi yako. Kwa sababu nano ya Mungu ni wa kweli. Kila neni anasema ni kweli; kila malako inatimizwa; na kila neno ya malipizo anasema inatimizwa, kama sisi tusitubu.
Sawa vile sisi tunatembea mbele ya mukaribifu yetu, vile anaonyesha Mufano yake na Mungu kwa sisi. Ee Mutu, kwa ajili yako inatoka maondoleo ya zambi ao hapana. Kwa mikono yako inandikwa wokovu ao uharibifu yako. Na unajua weye wenyewe nzuri sana ya kama bila maondoleo hakuna uhaki, hakuna wokovu. Ngapi matata ni hii kintu!

Unakataa kuhurumia ndugu yako, mwenye alinyanyua kichwa yake mbele kwako akuchabula! Lakini Mungu unayemuchabula kila siku na zambi yako ya kuachana ni mukubwa sana na anavumilia. Basi, zambi ma ngapi ni yako mbele ya Mungu na ma ngapi ni ya ndugu yako mbele Yake? Ma zambi ya mukaribifu yako wanafanana kama moja feza mbele ya ma elfu feza weye ukona deni mbele ya Mungu.

Basi, namna gani unaongolea kubeba usamehe juu ya hii zambi mnene na makubwa, bila kusamehe hii zambi udogo ya ndugu yako?

-Unasema ya kama mimi misikumufanyisia kosa moja na yeye bila maneno yangu alinichabula.

Ndivyo, lakini na Mungu, mwenye sisi tunamusikitika, kosa ninyi alifanya kwa sisi? «Kuonyesha ya kuwa Bwana ni haki, yeye ni mwamba wangu, wala uzalimu si ndani yake» (zaburi 92, 15). Tunafanya zambi bila akili na bila haya. Tunamusikitika Mungu. Na Yule, kama tunatubu, anatutuma mara moja rehema yake. Utukufu kwa upenda-wanadamu Yake na wema Wake!

Basi, kama unatakia kusamehewa toka Mungu, samehe na weye huyu anayekosa mbele yako.

Unasema ya kama usikufanye weye kosa; lakini iko namna kumufanyisia na weye kosa moja, kwa sababu hakuna namna ninyi wote wanayeishi ndani ya ushirika umoja hawatakupigwa katikati yao hata mara moja.

-Unasema ya kama weye ulimufanyisia kazi kizuri na yeye alinirudisha kazi kibaya.

Ni kweli ya kama iko nguvu sana kuvumilia hii kazi kibaya inayefanya kwako huyu uliyemusaidia. Lakini nani kupita mingi alitufazilia mu uzima yetu paka Mungu wetu? Lakini sisi tunazarau masaidio Yake na tunakosa kama mazimu mbele Yake.

Kama ukona hii yote mafundisho ndani ya akili yako, funika uso yako na paza sauti kusema toka ndani ya roho yako:

-Nilikosa, ee Bwana, unihurumie! Ninasamehe ndugu yangu. Unihurumie na Weye mimi musiyestahili mutumishi Yako, nilikosa mbele Kwako, Muumba na mufazili yangu.

Usiseme, ee Mukristu, ya kama weye ulionyesha uvumilia mingi kabisa mbele ya adui yako. Kumbuka mara ma ngapi ulikosa toka kipimo udogo yako mbele ya Mungu na ma ngapi Yeye alikuvumilia! Mambo ninyi itakuwa kama Yule Bwana alikuangalia sawa vile ilipaswa na ulikuwa mustahili? Ilipaswa kukushuka Mungu nafsi yako mbele ya nyakati mingi ndani ya gehena.

Unasema ya kama uko mtu na usiweze kuonyesha mapendo na wema hivi sawa Mungu. Ni kweli ya kama hapana usiweze, lakini usitake. Juu ya kutembea kwa mufano pa bahari usiweze, lakini iko nguvu kusamehe?

Kumbuka anatuhamuru Mtume Paulo kwa waKristiani wake: «Basi mufuate Mungu kama watoto wanaopendwa» (Wa Efeso 5, 1).

Umusamehe weye na, kama huyu hasitatubu, Mungu atamupatia katika matendo yake.

Unasema ya kama alikuchabula na matusi mbaya.

Lakini hii matusi haina kupita nguvu mbele ya matusi ya Bwana Yesu na Mwokozi wako! Yule walimuchelelea, walimuchabula, walimutema pa uso yake, walimupiga, walimupingilia, walimuvaa taji ya miimba, walimusulubia. Nani? Mwana wa Mungu, Bwana ya utukufu. Ninyi uko weye mbele ya huyu Uso mkubwa ya Kristu na ninyi uazarau na matusi yako mbele ya mateso na machabulana Yake? Ni kintu ya bure.

Kisha watu wengine hawakutema pa uso yako, hawakupiga, hawakuvaa taji ya miimba. Lakini Kristu alivumilia yoyote mateso yake. Juu ya ninyi? Juu ya mimi, ya weye na yote watoto Wake. Angalia kwa hii rikalasi ya uvumilia(Bwana Yesu) na bila shaka utasamehe kila uzarau na kila chuki ya watu wengine.

-Unasema ya kama, kama mimi mitamusaamehe, watu wengine wataanza kunichekelea.

Inapaswa kujua ya kama kwa wenye kibego na wenye watu ya hii dunia uzima wa Kristu na fundisho ya Evangelion inaonekana kama sharti (kwazo) na uzima ya mazimu, lakini mbele

ya Mungu ni hekima. Weye fanya kila amri inatuwambia Evangelion na hapana kila kazi inapendeza kwa watu ya hii dunia.

Acha ya kucheka hawa wenye ni wastahili ya kucheka. Lakini itakuja nyakati na wataria sana. Lakini ile nyakati itakuwa igariki. Ile wakati itawalumiza moyo umoja yao.

Mukristu mupendwa wangu!

Mambo ni nguvu kabisa. Kwa ajili yake itakuwa namna kupata wokovu ya roho ao kupata uharibifu yetu. Mambo ni usamehe ya zambi yetu, ile tunafanya kila siku. Lakini malalamiko na machozi watakuwa bila matunda, kama tusipende kusamehe makosa ya mukaribifu wetu.

Hapa inafuchamwa hali kibaya, uzima ya bure na usikini ya roho ubinadamu yetu. Ee Mutu, unataka kuhurumiwa ya Mungu, lakini weye unakataa kuhurumia mwenzake yako!

Unataka Mungu akusamehe zambi yako, lakini weye unakataa kusamehe matendo maovu na wasipo haki ile iko namna kufanya moja mukaribifu yako!

*********

Ee, wa Kristiani wangu, Bwana yetu alitupatia na amri ingine moja: «Pendeni adui yenu, muwabariki wenye kuwalaani ninyi, muwatendee mema wenye kuwachukia ninyi, muwaombee wenye kuwazarau, na kuwatesa ninyi» (Matayo 5, 44).

Haina ya kuenea kwa wa Kristiani, kama wanapenda paka wale wanaonyesha mapendo kwao, kwa sababu hivi wanafanya na wenye wasipo imani, wenye hawajue Mungu wa kweli na hawasadiki Kristu. Bwana anasema ninyi: «Maana kama mukioapenda wenye kuwapenda ninyi, munapata zawabu gani? Hata watoza kodi hawafanyi sawasawa? Tena kama mukisalimu ndugu zenu tu, munatenda tendo gani la kupita wengine? Hata Nataifa hawafanyi sawasawa? (Matayo 46-47).

Wa Kristiani, inapaswa kupitisha mu mapendo wale wasipo imani. Hivi wataonyesha uchanisho na ukamilifu yao mbele ya wale wasipo imani.

Baba yetu aliye mbinguni «yeye anaangazia jua lake waovu na wema, naye ananyeshea mvua wenye haki na wasio haki» (matayo 5, 45). Basi, kama watoto yake sisi inapaswa kumufata. «Basi mufuate Mungu kama watoto wanaopendwa» (Wa Efeso 5, 1).

-Unasema ya kama hakuna namna kupenda mimi wa adui yangu na kuwafanye makazi mazuri.

Lakini usiwe na haki. Kwa sababu namna gani iko namna Daudi kuria juu ya wale walijiuwa wa adui yake, Sauli na Abesalomi? Machozi yake haina alama ya kuonekana ya mapendo yake mbele ya wa adui yake? Namna gani ilikuwa namna kwa Mt. Mshahidi Stefano kuomba juu ya waa dui yake, wenye walimupika na maimbwe: «Bwana, usiwahesabie zambi hii. Akikwisha kusema maneno haya akalala» (Matendo ya Mitume 7, 60). Kwa sababu iko namna kwa Watakatifu wote kusamehe wa adui wao, iko namna kufanya na weye sawasawa. Kwani na wale walikuwa watu, sawa weye. Hii hali ubinadamu ukona na weye walikuwa na na wale watakatifu.

Watoto wadogo, wakati wanaenda mu masomo, wanafunda ku mwanzo ma herufi ya Alphabet, kisha pole-pole wanaanza kusema ma herufi wa wili-wili na kisha ku mwisho wanasoma bila mambo. Hii njia inapaswa kufata na wa Kristiani. Ya kwanza watajifunda kufanya kazi kizuri mu fasi ya kazi kibaya; kisha watafunda hapana kufanya kazi kibaya pa fasi ya kazi ingine kibaya, na kisilani pa kisilani ya mtu mwingine ao matendo mbaya yulu ya matendo mbaya ya watu wengine. Ku mwisho inapaswa kupenda wa adui wao, kusaidia ninyi wote wanawachukia na kufanya kazi kizuri pahali wanakutana ma kazi mbaya.

Tazama mugazi kwa ile wa Kristiani wanafika mu Ukamilifu-mapendo kwa wa adui.

Mufalme wa mbinguni anatushauria hapana paka kusamehe ninyi wote wanatuzarau, lakini kupenda wenye adui yetu. Kama tuysifanye hivi inatuongolea lufu wa milele. «Bwana, Bwana atakayeingia ufalme wa mbinguni; lakini yeye anayefanya mapenzi ya baba yangu aliye mbinguni» (matayo 7, 21).

## Kazi ya kupaswa ukamilifu

Wa Kristiani wapenzi! Tunakombana kupata mapendo ndani ya ma roho yetu mbele ya mukaribifu yetu. Hii ni kazi kupaswa ukamilifu.

Tunda ya kwanza ya mapendo wa Kristu ni tusifanye kazi kibaya hata kwa mtu moja. Tunda ya mbili ni kuhuruma na kusaidia mukaribifu yetu.

Huyu anayependa hasifanye kazi kibaya. Anapenda wazazi wake na wakubwa, kwa hivi anatii na anawaheshima. Kazi kibaya ni hasira na kisilani, lakini huyu anayependa hasianguka kwa hii kazi kibaya. Kosa mnene ni matakio ya zambi ya mwili na zambi pamoja na wale waliowa, lakini huyu anayependa hasianguka kwa hii zambi. Kazi kibaya ni kunyanganya ma bintu ya watu wenzake na ma namna mbaya na uovu, lakini huyu anayependa hasianguke kwa hii kazi kibaya. Kosa ni sauti ya wongo, uhukumu, matusi, kulanda, uovu, uzulumu na ukali, lakini huyu anayependa hasianguke kwa hii zambi.

Kazi kibaya ni wakati wachungaji wanazaifu kundi ya wa Kristiani yao na hawatumike wokovu yao, lakini muchungaji muzuri hasifanya hii zambi. Ni kazi kibaya kama bibi moja anapatana na bwana mwingine ao bwana anapatana na bibi mwingine, lakini huyu anayependa hasianguka kwa hii kazi kibaya.

*****

Tunda ya mbili ya mapendo ni mbele ya mukaribifu yetu wema yetu mu mateso na sikitiko yake. Huyu anayependa kweli, kama anaona ndugu yake ndani ya uzima ya usikini, hakuna namna kusimama bila kumuwema na kumupatia mukono ya saidio yake kwani mapendo iko na wema. Mapendo anaona mwenye njaa na anamupatia chakula. Anaona mwenye kihu na anamupatia maji, anasaidia mwenye mugeni na anamukaribisha, mugonjwa na mufungwa na anawatembelea. Na ma sauti kusema kidogo kwa kila sikitiko mapendo inasaidia na inatembea.

Kwa huyu anayependa roho yake inasikia huzuni, kama anaona ndugu yake kuanguka ku mateso moja. Vile alifanya na Mungu mupenda-wanadamu. Aliona mutu, kuanguka ndani ya taabu na uharibifu, alimupenda sana na alitembea bio kumuwema. Alituma Mwana wake wa pekee mu dunia juu ya kumuokoa.

Kisha hii mafundisho tunasikia ya kama watu, wenye wanawaza ao wanafanya kazi kibaya kwa mukaribifu yao na watu wengine, wenye wanasula mbele ya mateso ya wa ndugu yao, hawakuwa na ndani ya ma roho yao mapendo. Kwa hawa ni na wale watajiri wanarabisha makuta yao mu matakio mbaya, bila kuwaza mateso ya wamaskini. Na, kwani hakuna mapendo mu roho yao mbele ya mukaribifu yao, hata Mungu hawamupende.

Basi, iko lazima kujifanya watu wa kweli katika mapendo mingi mbele ya mukaribifu yetu na hivi tutakuwa wa Kristiani wa kweli na hapana wawongo. Kwa sababu kwa ajili ya hii fazila anafamiwa Mukristu moja. «Hivi watu wote watajua ya kama ninyi wanafunzi wangu, kama ninyi mukiwa na mapendo ninyi kwa ninyi» (Yoane 13, 35).

*****

Sisi wote tulipotea kwa ajili ya zambi ya Adamu na Eva ndani ya Paradizo; lakini tuliokowa katika Damu ya Kristu, Mwana wa Mungu, «aliyenipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu» (Wa Galatia 2, 20). Basi, inapaswa kupenda ninyi kwa ninyi.

Mungu alitupenda sisi wote, «hata kutoa Mwana wake wa pekee, ili kila mutu akimwamini asipotee, lakini apate uzima wa milele» (Yoane 3, 16). Basi, inapaswa kupenda ninyi kwa ninyi.

Mungu alipatia kwa sisi wote neno Yake takatifu kama lambi inayeangaza ndani ya giza. Huyu neno Yake inatufundisha mapendo na wema. Basi, inapaswa kupenda ninyi kwa ninyi.

Sisi wote tunaitwa mu imani moja; tunasadiki kwa Mungu moja, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Huyu anatupenda. Basi, inapaswa kupenda ninyi kwa ninyi.

Sisi wote tunaomba mbele ya Mungu moja; Tunamuwambia mambo yetu, tunamusujudu, tunamuhimbia na tunamutukuza. Basi, inapaswa kupenda ninyi kwa ninyi, sawa vile na Yule anatupenda.

Baba yetu aliye mbinguni anatupatia kwa sisi wote mukate, ma nguo, nyumba na ma bintu yote ingine. Basi, inapaswa kupenda ninyi kwa ninyi.

Sisi wote tunaitwa wa Kristiani toka Jina ya Kristu. Basi, inapaswa kupenda ninyi kwa ninyi, sawa vile na Yule anatupenda.

Sisi wote tukona Ubatizo moja, sisi wote mu Ubatizo yetu tulikataa shetani na matendo yake waovu na tulilaka kwa Krisru kuwa na mapendo. Basi, inapaswa kupenda ninyi kwa ninyi.

Sisi wote tukona mwito kwa uzima ya milele na tunasoma Simvolo (Fundisho) ya Imani, «natumaini ufufuo wa wafu na uzima wa milele mbele utakayokuja». Basi, inapaswa kupenda ninyi kwa ninyi.

Sisi wote tunakaribia Meza Takatifu juu ya kupewa Mwili na Damu ya Kristu. Ngapi juu pia ni Huyu Fumbo! Ngapi ni upenda-wanadamu ya Mungu! Basi, inapaswa kupenda ninyi kwa ninyi.

Ewe wa Kristiani! Sisi wote tuko wa ndugu. Tukona Baba moja. Kwake tunaomba na tunasema: « Baba yetu, uliye mbinguni. . . ». Basi, inapaswa kupenda ninyi kwa ninyi.

Tazama ya kama Mukristu moja eko na maneno ma mingi ya kupenda mukaribifu yake. Lakini maneno ukubwa ni hii ya kama Mungo mumoja anamupenda.

Ee Mukristiani mupendwa wangu, utafanya ninyi sasa? Utakataa kupenda kiumbe upendwa ya Mungu, mukaribifu yako? Kiumbe aliyeumbwa «katika mufano na sula ya Mungu, sawa weye? Kiumbe yule aliyeuzwa na Damu ya Kristu, sawa vile na weye? Kiumbe aliyeitwa mu uzima ya milele, sawa vile na weye? Kiumbe huyu Mungu anakuhamuru kumupenda, sawa vile maungo yako? . Basi, ee wa Kristiani wangu, inapaswa kupenda ninyi kwa ninyi, sawa vile na Yule anatupenda.

# SEHEMU YA TANO
# KU UZIMA WA MILELE

## Mukuangalia mbingu

Wa Kristiani wa kweli wanaishi ndani ya hii dunia kama wasafiri na wageni na wenye safari. Na wanaangalia daima na ma macho ya imani inchi wa milele na wanakombana kuingia kwake.

Na weye ufanye ndani ya hii dunia musafiri na mwenye njia. Angalia daima hii inchi ya milele na tumika kuipata. Vile itakufa ndani yako dunia ya zambi, matakio ya mwili, na mapendo ya kila kazi kibaya.

Huyu anayeomba na anakombana kufata uzima wa milele, huyu anaona ya kama ma bintu yote ya hii dunia ni ya nyakati kidogo na anasopoka kutafuta paka ma bintu ya milele na hapana ma bintu ya hii dunia.

Sisi wote tunaumbwa toka Muumba yetu juu ya uzima wa milele na tunaitwa kwa hii uzima na neno Yake takatifu na Ubatizo takatifu kwa ajili yake sisi tulizaliwa mara ya mbili katika roho. Kwa hivi alikuja Kristu, Mwana wa Mungu mu dunia; juu ya kutuita na kutuongoza kwa hii uzima, ile ni ya kweli na wa lazima kabisa. Hii matakio inapaswa kuwa kazi yako ya kwanza na kila tendo yako inapaswa kunioloka kwa hii njia. Bila hii uzima ma bintu hii ya dunia ni ya bure, hata kama ukona mamlaka mu dunia nzima.

Kila zambi na mapendo kwa hii dunia inazibiria hii njia ya uzima wa milele. Basi, chunga nzuri roho yako toka hii bintu ya dunia juu ya usipotesha hii uzima ya milele.

Unasopoka mingi hii uzima yako, lakini unajua ya kama utamuiacha hii uzima na unafanya nguvu kuongeza miaka mingi. Lakini ngapi kuliko mingi inapaswa kusopoka juu ya uzima ya milele na kukombana hapana kuipotesha?

Ma bintu ya hii dunia mbele ya bintu ya uzima wa milele ni sifuri moja. Tafuta hii uzima ya milele kama kintu wa pekee na wa kweli na epuka toka kila kintu inakufunga mulango kwa iungia kwa hii uzima. Mungu mupenda-wanadamu anataka akuokoa. Hii inapaswa kuwa na mapenzi yako. Vile bila shaka utaokolewa. Inapaswa kuitakia na kuitafuta, sawa vile anafanya huyu mwenye njaa na mwenye kihu, wenye wanataka chakula na maji. Paka hivi utakamata katika matakio yako.

Usifate wale wa Kristiani, wenye wanatakia na wanalubata ma bintu ya hii dunia juu ya kuishi ndani ya ma furaha na matukufu. Hawa walisahabu ya kama Mwana wa Mungu aliteswa na alikufa kwa ajili yao na kwa Musalaba na lufu Yake alifungula mulango wa milele, kwa ile aliwaita. Hawa wanatakia na wanakombana paka bile bintu wanaiona na ma macho ya mwili yao; lakinininiyi wote hawaione hawapende na hawatafute.

Hawa kila siku wanafungula mikono yao, sawa vile zamani Adamu. Kwa muti iliyekuwa kutakazwa ya kula matu da yake, lakini hawa watu wanakula toka hii matunda na vile wanatoka na mapenzi yao toka Mungu.

Hawa wanaishi kama watu ya Yuda, wenye, wakati walitoka ya Misiri, walirudia mara ingine mukongo ma roho yao na walitakia ma chakula ya wenye Misiri; vile alisirika kupingana yao Mungu. Hawa wa Kristiani katika neema ya Ubatizo takatifu waliuhuruwa toka utumwa ya shetani, sawa vile zamani taifa ya waYuda toka utumwa ya Mfalme Faraoni, na waliitwa ya kupata ma bintu ya uzima wa milele. Lakini roho yao inajama ma bintu na ma furaha ya hii dunia. Wanazaifu juu ya bintu wa milele na wanalubata yenye ya hii inchi yetu. Kwa hivi Bwana Yesu anasirika kupingana yao na hawa inapaswa kuongolea malipizo hapana ya nyakati kidogo, lakini wa milele.

Weye, usifate hawa wa Kristiani, lakini unioloka imani yako na roho yako ma bintu wasiyoharabika. Mali ya Mukristu, uriti, ma sifu, utukufu, na ma hazina yote hakuna namna

kuipata ndani ya hii dunia, lakini kwa inchi wa mbingu. Pale ni tayari toka Baba wa mbingu yote ma bintu juu ya huyu.

Hii ma bintu ya milele inapaswa kukombana ya kuipata kila siku. lakini ma bintu ya hii dunia utaitumia na pasopo na boka ya Mungu na usisirika Bwana Mungu na upenda-feza yako. Kumbuka tena anaandika ninyi Mtume: «Kwa sababu hatukuleta kitu duniani, tena ni kweli ya kuwa hatuwezi kutoka na kitu; lakini tukiwa na chakula na nguo, kwa vitu hivi tufurahi» (Barua ya kwanza kwa Timoteo 6, 7-8).

Angalia damani ni katikati ya wakati na uzima wa milele, hii uzima na uzima ingine, wenye mzima na wenye kufa na akili yako itaangaziwa juu ya kufamia na kusikia ya kama wale watu wanalokota bintu ya hii dunia na hapana kwa mbingu, wanafanya kazi kibaya. Hivi anatuwambia na Bwana Yesu: «vile ni yeye anayejiwekea mwenyewe hazina ya mali, wala hana utajiri kwa Mungu» (Luka 12, 21).

Wenye kufa wote waliacha dunia na ma bintu yote ya hii uzima. Hivi na weye utaicha, hata kama na dunia yote ni yako. Paka kintu moja inasafiri pamoja na sisi, na hii ni utawa na ma fazila ya Kristu.

Basi, ishi mpaka mwisho ya uzima yako na utawa na boka ya Mungu na chunga hii utawa kama hazina ukubwa ndani ya roho yako.

## Mauti

Uwazo ya mauti iko namna kusaidia mtu moja kwa toba. Mauti sisi tunaifamia na tusiifamie. Tunaifamia, kwa sababu sisi yote tunajua ya kama siku moja tutakufa. Tena tusimufamia, kwa sababu hatujue wakati gani na namna gani tutakufa.

Kama tunaishi miaka mingi, hii uzima yetu inafanyikwa kidogo, kwani ma siku yetu wanabakia madogo na tunakaribia mu lufu. Leo tuko karibu yake siku moja toka jana, saa moja toka saa moja ya mbele. Lufu inatembea pasipo kuonekana mukongo ya kila mtu na anamunyanganya ile saa yeye hasijue na hasiongolee. Lakini watu wote karibu- kabisa wenye afya na wenye nguvu- wanafanya hii mawazo juu ya maungo yao:

-Mimi nitaishi tena miaka mengi. Mwisho yangu ni tena mbari sana. Nitalokota mali na nitafurahi.

Lakini inakuja bio kupingana yao lufu na mawazo na matakio yao wanazimisha. Na anakufa bio huyu anayetumainia kuishi miaka mingi. Na anaacha bintu yake na mwili yake mu dunia yule aliyependa kulokota mali mingi.

Basi, mwisho yetu asiyekufamia, ee wa Ktistiani wangu. Mungu mupenda-wanadamu anaYesubuka juu ya uzima nzuri yetu, alitengeneza hivi juu ya kuwa sisi daima tayari na kukimbia mu toba ya kwli.

Kama mutu atalokota mu uzima  yake ma fazila ya Kristu, pamoja na ile ataenda mu uzima wa milele, kama atalokota zambi, pamoja na zambi atasimama mbele ya Uhukumu ya Mungu.

Ee, ndugu wangu wenye zambi,  tunawaza na pasopo mingi hii ma sauti na tunatubu juu ya tusisafiri mu uzima wa milele na ma zambi yetu na tunasimama hivi mbele ya Uhukumu ya Mungu.

Mungu mupenda-wema alitulaka neema Yake; lakini hasikutulake ya kama tutaishi kesho asubui. Alifanya hivi juu ya kuwa wa tayari, na wakati tunalamuka, inapaswa kukumbuka lufu yetu, kutengeneza maungo yetu, na kutayarisha nafsi yetu juu ya matokeo yetu na kupata mwisho wa heri.

Saa ya lufu ni matata kwa sisi wote. Watakatifu wote waliiwaza na waliria na waliomba Mungu mupenda-wanadamu kuwahurumia ile saa. Hii ni wa ajabu! Wanaria Watakatifu kwa uwazo ya ile saa ya mauti yao na wenye zambi lakini hawapende kukumbuka hata ile saa ya lufu yao.

Ee wenye zambi wamaskini katika roho! Juu ya ninyi tunalala, lakini shetani kama mwivi ananyanganya wokovu wetu? Iko lazima kuandika mu akili yetu saa ya lufu yetu na kukuwa wa

tayari. Kwa ajili ya matayarisho ile saa ya mwisho itakuwa kitumaini ya kama huyu mutu eko mwenye heri wa milele ao mwenye taabu ya milele. Toka ile saa ya lufu inafunguliwa ya kila mtu mulango ya wa milele na njia ya heri wa milele ao taabu wa milele. Tangu hapa mtu anaanza kuishi ao kufa wa milele.

Eko wapi ninyi wote waliishi mbele ya sisi na walipita uzima yao bila toba, katika zambi na machezo? Walitoka ya hii dunia na waliacha hapa ma furaha yao yote. Waliongozwa kila moja mu makao yake kuongolea Uhukumu ya mwisho, na kisha watakamata zawadi ao hapana katika matendo yao.

Kwa hivi, kwa sababu bado kufika ya sisi ile saa ya mwisho yetu, iko lazima kupindula macho ya roho yetu kwa Mungu wetu na kusikilizana pamoja na Ye kwa imani, na kitubio, ni ahivi tutapata uzima wa milele.

*********

Ee Mukristiani mupendwa! Mauti inatufata mwenedo kwa mwenedo bila sisi kuiona na mwisho inakuja ile saa sisi tusiiongolea. Kwa hivi kuwa daima mu hali ya kutubu, tayari daima juu ya hii safari kwa milele.

Mutumishi mwenye akili ni ya kusimama daima na anaongolea wakati gani atamuita Bwana wake. Simama na weye na ongolea wakati gani atakuita Bwana Wako, Kristu katika lufu. Ishi sawa vile ulipenda kufika lufu kwako. Ishi na utawa na «timizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka» (WaFilipi 2, 12). Vile usitapoteshe wokovu wako wa milele, iliyetupatia zawadi Mungu Yesu katika Damu Yake na mauti Yake. Hivi utaishi uzima yako na uatawa, katika Bwana; na « heri wafu wanaokufa katika Bwana tangu sasa» (Ufunuo 14, 13).

## Matisho ya Mungu

Ndani ya Madiko Takatifu tunakutana matisho ya kuandikwa ya Mungu; anatisha na malipizo ya nyakati kidogo na ya milele huyu mutu anayekataa kutubu.

Sawa vile mfalme, anasubuku juu ya kutembea taifa na inchi yake katika sheria yake, pahali ni ma amri ya kulipiza wenye wazulumu; vilevile na Mfalme wa mbinguni Bwana na Mungu anajulisha sheria Yake takatifu kwa watu wote. Inapaswa watu katika hii sheria kuishi na kufata maungo yao; kuepuka toka kila sheria inayekatazwa matendo filani na ninyi wenye wanakataa hii amri wanahukumwa na malipizo ya nyakati kidogo ao wa milele. « Na shoka limekwisha kuwekwa katika shina ma miti; basi kila muti usiozaa matunda mazuri unakatwa, na unatupwa katika moto» (Matayo 3, 10).

« Lakini wenye woga, na wasioamini, na wenye machukio na wauaji, na wazini, na washawi, na wanaoabudu sanamu na wawongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa linalowaka moto na kiberiti» (Ufunuo 21, 8).

«Kama mutu asipogeuka, ataona upanga wake; amepinda upinde wake na kutayarisha. amemutengeneza silaha za mauti; anafanya mishale yake kuwa moto» (Zaburi 13-14).

« Ataonyesha waovu mitego; moto na kiberiti na upepo wa kuchoma zitakuwa fungu la kikombe chao» (Zaburi 11, 6).

«Hamujui ya kama wazalimu hawatariti ufalme wa Mungu? Musidanganywe: washerati, wala wenye kuabudu sanamu, wala wazini, wala wakike, wala wafiraji, wala wizi, wala wenye tamaa, wala walevi, wala watukanaji, wala wanyanganyi hawatariti ufalme wa Mungu» (Barua ya kwanza ya wa Korinto 6, 9-10).

Hii na ingine matisho ya Mungu ni ya matata, llakini mara moja wanatuonyesha upenda, wanadamu ukubwa ya Mungu: Asisaidie hata kintu ingine mtu moja mwenye zambi mu toba kupita sawa matisho ya malipizo.

Mungu katika malako mazuri yake anatuita karibu Yake, mu wokovu wa milele. lakini na matisho ya malipizo Yake anatusimamisha na anatushauria mu kazi kizuri.

Kwa hivi anatisha wenye zambi, kwani asitake kuwaharabisha; kwa hivi anaonyesha hasira Yake juu ya kumuogopa na kutengeneza maungo yetu na hivi tutatoka ya uhukumu wa milele.

Kama boka ya mfalme ya inchi yetu inatuepuka ya ma kosa mengi, ngapi kupita mingi inatuepuka boka ya Mfalme wa mbinguni, inayeweza kutusimamisha ya kila kazi kibaya na hivi itatusukuma kwa toba, kama sisi tutakumbuka daima hasira wa haki Yake kupingana ya zambi yetu na matisho yake wa matata?

Ni kweli! katika boka ya malipizo mtu anafungwa kama kamba moja na asiweze kutelemuka mu zambi! Ndivyo, asitaweze kukosa, kama mbele ya ma macho yake eko na bila kuizimisha kumbusho ya moto wa milele, iliyetayarishwa juu ya wenye zambi.

Kumbusho ya malipizo hasitamuacha kuanguka mu ulipizo, na uwazo ya gehena, hasitamwacha kuanguka mu gehena.

Ee Ndugu wangu, tuko na ma deni mengi kwa Mungu wetu, tena kwa sababu alitufunua gehena na ile malipizo! Kwa sababu, sawa hivi tulisema, hii makumbusho ya matisho inatusukuma mu toba kuliko ya kumbusho ma bintu ya mbingu kwa malako wa milele.

*****

Ee Ndugu wangu, fungula sasa, risikio ya nafsi yako na sopoka ninataka akuonyesha ninyi:

Ni uharibifu mbaya sana kama mtu moja anazarau matisho ya Mungu na kisha asipende kutubu na kutengeneza maungo yake. Ni kweli; uisikie na uipokee bila shaka: Huyu anayezarau matisho ya Mungu anakokota pa kichwa yake hasira Yake.

Hakuna kintu ingine kuliko wa hatari kama mtu moja anazarau amri ya Mungu. Ataanguka mu gehena huyu anayepotesha boka ya Mungu; hasitatoke toka lufu wa milele huyuy anayezararu lufu wa milele; anakokota yulu yake hasira ya Mungu huyu anayesiogopa hasira ya Mungu.

«Kwa sababu Mungu wetu ni moto wa kuteketeza» ( Wa Ebrania 12, 29). «Ni neno la kuogopa kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai» (Wa Ebrania 10, 31). «Mungu hazihakiwi; yo yote mutu anayopanda, ndiyo atakayovuna» (Wa Galatia 6, 7). Mungu ya wakati mingi anaonekana murahimu na mupenda, wanadamu; lakini ni na mwenye haki; «atakayelipa kila mutu kwa kadiri ya matendo yake» ( Wa Roma 2, 6).

Ee Wenye zambi, ni lazima kuchunga nguvu ndani ya akili yetu hii neno: Ni uharibifu mbaya sana kama mtu moja anazarau matisho ya Mungu.

Mungu alikatisha wa babu wetu mu Paradizo: « Lakini wa muti wa kujua uzuri na ubaya usile kwa maana siku unapokula, hakika utakufa» (Mwanzo 2, 17). Hawa walikanyanga amri ya Mungu na walipata lufu. Walizarau ma amri takatifu watu wengine ya ile wakati ya Noe na walikufa ndani ya maji ya ulimwengu nzima. Waliizarau na waaatu wa muji Sodoma na Gomoro na walikufa katika moto. Wanaizarau na sasa wenye zambi na wanaharabishwa.

Walikufa ndani ya maji wenye wazulumu, kwani hawakusadiki ma Kuhubiri ya mwenye haki Noe. Leo wanaongolea ninyi na hawa watu wenye wanachabula Mungu na wanazarau sheria yake? Na hawa watakufa na kuliko matata ni ya kama watakufa kwa nafsi yao.

Moto ya mbingu ililungua wenye watu ya mji Sodomo kwa ajili ya zambi yao kwa mwili. Wanaongolea ninyi na wenye zambi, wenye zambi ya mwili na wengine yoyote wa leo? Paka moto ya gehena wa milele, pahali watalunguwa kwa milele.

Watu mengi ya taifa ya Yuda walipizwa mu jangwa kwa ajili ya makosa yao na wawakuingie mu inchi ya Palestina; hii mambo itafanyiwa na kwa kila Mukristu mukosefu: Hasitaingine mu Ufalme ya Mungu: atafungwa inje.

«Lakini inje ni imbwa, na wachawi, na wazini, na wauaji, na wanaoabudu sanamu, na kila mutu anayependa uwongo na kuufanya» (Ufunuo 22, 15).

Ee Wenye zambi, muchunga mu akili yenu hii neno na mutubuni. Uharibifu wa leo ni matata sana: kupita matata ni ile wa milele. Iko lazima kuiogopa na kurudia kwa Mung na hivi

utaiepuka. Watu wenye muji Ninevi waliogopa uharibifu iliyekuwa, kwani walitubu na hawakuharabishwa, lakini walipta rehema mu upenda-wanadamu ya  Mungu. Tuende kupindula na sisi  na roho yetu yote kwa Mungu, tuende kutubu na tunasimama kumusirika Mungu na ma zambi yetu na hivi tutabeba rehema Yake.

## Uhukumu wa matata

Wa Kristiani wapenzi! Ninaogopa na ninatetemeka wakati ninasikia na ninawaza hii ma neno ya Mungu: «Tazama, ninakuja upesi na mushahara wangu ni pamoja nami, kulipa kila mutu kama ilivyo kazi yake» (Ufunuo 22, 12).

Nani anasema hii ma neno? Mungu mukubwa na mwenye matata. Anasema ninyi? Ya kama atakuja Yeye mumoja kuhukumu ulimwengu na atapatia kwa kila mutu katika matendo wake.

Ee Wenye zambi wamaskini! Inapaswa kuwaza ninyi kama munasikia hii ma neno? Mungu mumoja anakuja amuhukumu na amipatia katika matendo wenu! Muogopeni na musiendelee zambi yenu! Yeye anakuja akuhukumu! Anakuja na nguvu na utukufu mingi! . . .

Ee Bwana utuhurumie, Hurumie kiumba Yako! Hakuna hata mutu moja wasipo zambi, paka Weye wa pekee.

*****

Wa ndugu wangu, ile siku na saa, wakati atakuja Bwana akuhuhukumu wenye zambi ni matata kabisa. Tunatetemeka kama tunawaza  uhukumu moja  ya inchi yetu: lakinimkuliko matata itakuwa ile uhukumu ya milele

Hata wanahukumu watu wenye kufanana na sisi: lakini kwa ile Uhukumu ya mbingu atahukumu Mungu!

Hapa weko washuhuda wenye wanasitake ao wanalinzi mukosefu moja: pale hakuna lazima ya washuhuda, kwa sababu Mungu anajua yote matendo ya watu wote ya dunia.

Hapa iko namna watu kutengeneza ma kosa yao na namna mbaya ao mutajiri moja atahukumwa na namna ingine na maskini moja na namna kuliko kibaya: Lakini pale Mwamuzi hasiangalia nani eko huyu ao fulani mutu, lakini anahukumu katika moyo  yake matendo na ma neno ya kila mtu.

Hapa ku ma nyumba ya Uhukumu wanakuja na wanasaidizi na wa avokat. Wanahubiri wenye wakubwa juu ya kusaidia wa ndugu wenye wakubwa na wa hali umoja. Wanahubiri watajiri juu ya kusaidie wenye watajiri. Warafiki wanapenda kusaidia warafiki wao: lakini pale mu Uhuikumu ya Mungu kila mtu atajibu juu ya maungo yake.

Hapa mara mingi watajiri wanasaidia watu wao na makuta na mali mingi: lakini pale hakuna namna.

Hapa wanhubiri na namna ya kuachana: lakini pale watanyamasha wote na watabakia bila sauti yao.

Hapa mukosefu moja anajitake na anahukumwa mbele ya watu wadogo: lakini pale mu mbinguni huyu mwenye zambi atahukumwa mbele ya watu wote ya dunia.

Hapa wanaangaliwa matendo ile iko namna kuonekana: lakini pale wataonekana na matendo wasipoonekana.

Hapa wanahukumwa matendo wa uovu:  akili kwa ile uhukumu watahukumwa na ma neno ya bure: «Kila neno bule watu watakalolisema, watatoa hesabu ya neno hili siku ya hukumu» (Matayo 12, 36).

Basi, kama ya kila neno bule tutahukumwa, pale, basi wanaongolea ninyi ninyo wote wanajaza na uchefu ya zambi  ma nafsi na ma mwili wao? Watasema ninyi wenye kuiba wenye wanawake mbalaka na wenye watoto yatima? Tena niniyi wote wanaiba na wananyanganya ma bintu ya wageni? Ninyi wote wanatengeneza kisu yao juu ya kuuwa mukaribifu yao? Tena ninyi

wenye kulanda wakaribifu wao? Na ninyi wenye zambi wanaishi kila siku kama mukate na kila zambi yao?

*****

«Tazama, ninakuja upesi na mushahara wangu ni pamoja nami, kulipa kila mutu kama ilivyo kazi yake».

Ee Kizazi ukubwa ya wa Kristiani, tuliona ufikisho ya kwanza ya Kristu na Mungu wetu. Tutaona na Ufikisho Yake ya mbili, sawa vile na Mumoja anatuwambia: «Tazama, ninakuja upesi». . .

Ufikisho Yake ya kwanza waliituwambia ma Nabii Yake na ilitimizwa. Ufikisho ya mbili wanatuhubiri Waalimu ya Kanisa yetu: Tazama anakuja upeso mara ingine Kristu mu dunia. Atakuja mara moja.

Ufikisho Yake ya kwanza ilifanyikwa na kimya na unyenyekevu. Ile wa mbili itakuwa na utukufu na matata sana: «Kwa maana kama umeme unavyokuja toka mashariki na unaaonekana hata mangaribi; hivi kuja kwa Mwana wa watu kutakavyokuwa vile» (Matayo 24, 27).

Mu Ufukisho Yake ya kwanza alimuona watu ya dunia ya kutesa na kukufa kwa ajili ya zambi yetu. Mu Ufikisho ya Mbili atamuona kuikaa pa Kiti ya utukufu Yake ya kuhukumu wenye zambi kwa ajili ya zambi yao na atawapatia kwa kila moja katika matendo yake.

Sasa anasema kwa wenye zambi «mutubuni»: , ile wakati atawambia» Mujibuni»! Sasa anawaita karibu yake hawa wenye zambi-«ukujeni kwangu»- lakini ile wakati atawafukuza, kama hawatatubu- «mwendeni mbali yangu». Fasi wapi? «Mwende katika moto wa milele uliotengenezwa kwahetani na malaika zake» (Matayo 25, 41). O, hii neno ngapi ni wa matata!

Ee wenye zambi wamaskini! hasikukuje tena hii siku. Mwamuzi Mukubwa tena «lakini ni muvumilivu kwenu asiyetaka mutu mumoja kupotea, lakini wote wafike kutubu» (Barua ya mbili ya Petro 3, 9). Anaongolea tena kitubio yetu. Hasituhukumu tena, lakini anatupatia kama zawadi rehema yake kwa huyu anayetubu na anamuomba.

Basi tuende kutubu na sisi juu ya kupata rehema Yake, kustahiliwa akusimama mu fasi ya kuume na kusikia sauti yake wa furaha:

«Kujeni, ninyi muliobarikiwa wa Baba yengu muriti ufalme muliotengenezwa tangu kuumbwa kwa ulimwengu; » (Matayo 255, 34).

*****

Lakini wapenzi wangu, hii neno na wa matata kabisa: «Nitakuhamakia, na kuwaweka taratibu mbele ya macho yako»(Zaburi 50, 21). Na hii neno anaiambia ya mutu gani Mungu Mukubwa wetu? Anaimbia kwa mwenye zambi, sawa vile na kidogo yulu ya hii zaburi anasema hivi: «Lakini waovu Mungu anawaambia» (Zaburi 50, 16). Alimuwambia ninyi? Ya kama atamuhukumu juu ya zambi yake yote na atamuonyesha mbele ya ma macho yake yote matendo mbaya yake. Fasi wapi? Mbele ya watu ya ulimwengu. Pale pahali watakuwa wa malaika watakatifu na pahali watasanyikwa watu wote wenye waliishi tangu mwanzo ya dunia.

Kwa hii Makusanyo ya ulimwengu atahamakiwa kila mwenye zambi. Matendo yake aliyeifanya bila moyo, wataonekana mbele ya ma macho ya watu yote ya dunia.

«Nitakuhamakia, na kuwaweka taratibu mbele ya macho yako».

Weye, ee mwenye zambi, ulifanya hii kazi na hii na hii? «wakati ulipoona munyanganyi, ulimukubali, na umeshiriki na wazini. Unatoa kinywa chako kwa mabaya, na ulimi wako unatengeneza hila. Unaketi na kusengenya ndugu yako: unasingizia mwana wa mama yako mwenyewe» (50, 18-20).

Ee Mwenye zambi! Weye ulikanyanga sheria yangu na ulitupa ma neno yangu mukongo»! Na unazania ya kama hii yote ma kazi yako itatoka mbele Mimi kuilipiza?

Hapana, hapana! haitakuwa hivi, sawa vile weye unazania na uwazo yako kibaya juu ya kulanda maungo yako!

Mimi ile matendo yako yote uliyefanya nitaihamakia na matendo, ma neno, mawazo, ma naziri na yoyote ma kazi yako nitaileta mbele ya ma macho yako!

Ndivyo, weye mwenye zambi uliwaza bila boka ya sheria yangu na ulitenda, ulitakia na ulisema sawa vile weye ulipenda bila boka. Lakini ma neno ya kinywa yangu takatifu, uliikanyanga! «Nitakuhamakia, na kuwaweka taratibu mbele ya macho yako».

Kwa huyu mwenye zambi ya mwili na wa chabulana Bwana ataleta mbele yake matakio yake ya mwili, ma neno, ma macho ya uovu yake na matendo ya zambi ya mwili yake. Atamuonyesha fasi wapi na wakati gani alitenda na mtu nani alifanya hii zambi ya mwili.

Kwa mtu munyanganyi atamuonyesha kwa mutu nani na namna gani alifanya kazi kibaya na wakati gani alimupatia kubwa sumu ya kufa ao alimufanyisia kintu ingine kibaya: mtu nani na mbele ya mutu nani alimuchabula na namna gani alifanyikwa sababu ya matusi, udanganyifu na taabu na ingine-ingine.

Huyu mwivi na mwovu wataona mbele yao ma kazi ya kuiba yao yote sawa walifanya hii matendo yao kwa siri na namna uovu sawa ya kuonekana: wataona kintu ninyi, fasi wapi na ya mtu nani walinyanganya bintu yake na mtu nani walimulanda.

Mu kazi ya biashara wataonekana bintu ma ninyi waliiuzisha bila moyo na bila haki na walilanda watu wengine: ma nani bintu waliikuwa ya kuoza, wale waliiuzisha sawa ya nzuri na bei kuliko mingi. Itajionekana maji ngapi walichanga pamoja na vinyo, mara ma ngapi na ya bintu ma nani waliongeza ma bei mingi na hivi walikanyanga moyo yao.

-Ndivyo, na weye utasikia kwa ile wakati uliuzisha bintu yako na bei mingi na hivi ulilanda watu na ulikanyanga moyo yako na sheria yangu juu ya kuiba wa ndugu yako.

Mbele ya mwenye kuchabula na kusema matusi wataonekana mbele yake matusi na ma chabulana yake yote, ile alisema kupingana ya Mungu ao ya wa ndugu wake na ya watakatifu wetu; tena itajionekana fasi wapi, wakati gani na kwa mutu nani alisemaka hii ma sauti.

Mbele ya mkubwa mwenye zambi itajionekana uvivu na uzaifu yake mbele ya watumishi wake, hasira, chuki, ugumu na matendo yake ingine yenye karibu.

Mbele ya muchungaji ya Kanisa muvivu watajionekana mazaifu yake juu ya kundi ya waminifu wake na ma zambi yake ingine.

Mwamuzi aliyepokewa makuta juu ya kusema ma sauti ya wongo watajionakena mbele yake malako yake ya wongo, ukanyango ya sauti ukweli na haki ya Mungu na ma zambi yake ingine.

Wazazi wazaifu wataona uvivu yao mbele ya kukomea nzuri watoto wao na kwa ajili ya uharibifu ya watoto wao mu njia ya upotevu, tena watahukumwa juu ya kwazo yao mbele ya watoto wao.

Juu ya kusema na sauti paka moja kila mtu mwenye zambi sawa alifanya matendo mbaya yake kwa siri sawa alifanya ya kuonekana, hii matendo yake watamufata pale kwa ile saa ya Uhukumu, pahali yoyote ma kazi yake watakuja mbele yake.

Wataonekana na kwa mweye ee, mwenye wapenzi ya dunia na zambi ya mwili matendo yenu yote. Watajionekana machezo na macheko na machakula wenu, mazambi na masafari na ma furaha yoyote wenu. Mweye mulipindula ma roho yenu toka Mungu, kwa mwenye mulisema ya kama munamusadiki na ma fasi ingine mulipindula mapendo ya ma roho yenu. Hapana kwa Mungu na Ufalme Wake lakini ndivyo ma furaha ya dunia na matakio mbaya na zambi yenu. Ile wakati, basi, musiriti furaha, lakini mutapima malipizo wa milele, taabu, sikitiko na ombolezo. «Nitakuhamakia, na kuwaweka taratibu mbele ya macho yako».

Ile wakati atahamakiwa kile mwenye zambi na atasikia:

-Tazama mtu ninyi uko weye na tazama matendo yako ni ninyi.

Hii sauti ya Mungu ataisikia na huyu mwenye zambi ya mwili, mwivi, munyanganyi, mwovu, mudanganyifu, musiyehaki na mkubwa musiye hukumu ya moyo yake, mutumishi musiyemoyo, mwamuzi mwenye kubeba makuta na kila muuwaji na muchungaji mubaya ya

kanisa, kila mwenye zambi mwenye bado kusafishwa katika toba toka zambi yake. Atasikia kila mtu hii sauti ya Mungu, atasikia haya na atamukamata boka, tetemeko na ajabu.

Watapaza sauti kusema kwa ma imbwe na ma kilima: «Mutuangukie, mutufiche mbele ya uso wake yeye anayeketi juu ya kiti cha ufalme, na gazabu ya Mwana-Kondoo. Kwa maana siku kubwa ya gazabu yake imekuja na nani anayeweza kusimama? » (Ufunuo 6, 16-17).

*****

Ee mwenye zambi wamaskini! Hasikukuje tena ile siku. Bwana anapokea tena toba yetu. Anasamehe tena zambi ya huyu mtu anayetubu. Tuende kurudie Kwake na toba na kusimama kufanya zambi. Machozi yetu iko namna kuzimisha zambi yetu na hivi hawataonekana kwa ile makusanyo ya watu wote ya ulimwengu.

Ee nafsi wa zambi, ria, ria mingi! Umivu na omboleze kwa sababu ulikosa mbele ya Mungu. Ombe, tafuta na piga mulango juu ya akufungula Bwana mulango ya rehema Yake. «kwa maana kila mutu anayeomba, anapokea; naye anayetafuta anapata; naye anayepiga mulango atafungulia». (Matayo 7, 8).

## Uzima wa milele

Hakuna kintu ingine ya kusukumu kupita mingi mtu moja mu toba, ya makumbusho ya uzima wa milele; na hakuna kintu kuliko wa faida ya roho mbele ya hii kumbuko ya hii uzima ya milele.

Uwazo ya uzima wa milele inakamata mtu ya kila zambi, inasimamisha ma zwezo mbaya, inaepuka ya kila furaha ya dunia, inachunga roho, inazala machozi, inaongoza roho mu sala na inaleta maombolezo ya roho.

Kumbuko ya uzima wa milele iko namna kutengeneza tena na yule mtu wa zambi mingi kabisa.

Kumbuko ya uzima wa milele ilijaza majangwa, na milima na ma pango na watawa mengi.

Kumbuko ya uzima wa milele ilipatia nguvu kwa Watakatifu wetu na Washahidi juu ya kuvumilia mateso ya matata kabisa na hapana kutii kwa mapenzi ya wenye wafalme pagano na hivi kukataa Kristu.

Kumbuko ya uzima wa milele alisaidia watu wenye zambi ya kuachana, sawa wanyanganyi, wauwaji, wenye zambi ya mwili na wengine juu ya kugeuza uzima yao na kufanyikwa Watakatifu ya Mungu.

Utukufu kwa upenda-wanadamu ya Mungu? Anafungula mulnago ya rehema Yake kwa wenye zambi yoyote wakubwa.

Tunastajabu sisi kwa sababu wa Kristiani ya hii wakati, hata na kama wanasikia Madiko Takatifu inayewaambia juu ya uzima wa milele, lakini waliziama ndani ya ma furaha ya hii dunia. Wanaomba na wanatafuta ma sifu, matukufu, mali, wanalokota ma bintu ya bure, wanatengeneza ma nyumba na ma shamba. . . na wanaishi sawa hawatakufa hata siku fulani. Lakini hivi wanasahabu juu ya ninyi walikuja mu dunia na roho yao inajaza na giza.

Wa Kristiani wapenzi wangu! Tuende kuandika mu akili yetu uzima wa milele. Inapaswa kuwa daima mu hali ya toba wa kweli, na roho ya kuvunjika na kwa ombi ya Mungu. Tusiziama hata ya furaha moja ya hii dunia. Tunazarau kila zambi, saw vile tunaepuka ya nyoka wa sumu. Hii yoyote inaonekana kama mazzuri ya hii dunia, kwa sisi inapaswa kuwaepuka.

*****

Kweli, Munajua ninyi uzima wa milele? Ni uzima bila mwisho. Itaanza bila kuzimisha hata wakati fulani. Hii ni uzima wa milele! Ma miaka yote ya hii dunia mbele ya hii uzima wa milele ni

kama alama moja kidogo mbele ya ulimwengu sawa ni dakika moja mbele ya ma milioane miaka. Hii ni uzima wa milele!

Uzima wa milele ni ya wili: Uzima wa milele wa heri ndani ya paradizo na uzima wa milele ya taabu ndani ya gehena.

Mu uzima wa milele ya Paradizo itazambalishwa ufalme wa Mungu. Tutaona Mungu Uso ku uso; itawala furaha usiyekusema na shangilio; nafsi na mwili watapata furaha yao na mutu atastahiliwa kupata ma bintu wa milele «jicho halikuona, wala sikio halikusikia, wala hayakuingia katika moyo wa mutu, Maneno Mungu aliyotengenezea wenye kumupenda» (Barua ya kwanza wa Korinto 2, 9). «Halafu wenye haki watangaa kama jua katika ufalme wa Baba yao» (Matayo 13, 43).

Mu uzima wa milele ya sikitiko itakuwa mbali ya Mungu na kila taabu na mateso ya mwili na nafsi. Ile wakati wale watu ya gehena watapenda kufa, lakini hasitakuwe mauti ingine.

Ee mtu wa zambi! Tunasikia toka neno ya Mungu juu ya uzima wa milele na tunaona ya kama ni wa wili, ile ya Paradizo na ile ya gehena. basi, inapaswa kutubu na kusafisha na machozi zambi yetu na hivi tutaepuka toka mateso na sikitiko na tutaingina mu uzima ya wa heri.

Kisha Uhukumu wa matata ya Kristu kila mtu atatembea mu uzima wa milele yake. Muhukumu Kristu ataonyesha ile wakati kwa watu wote ma fasi yao ya milele. Kwa wenye haki atawafungula milango ya uzima ya ufalme Wake. «Kujeni, ninyi muliobarikiwa na baba yangu, muriti ufalme muliotengenezwa tangu kuumbwa kwa ulimwengu» (Matatyo 25, 34)

Lakini kwa wenye zambi atasema: «Ondokeni kwangu, ninyi muliolaaniwa, mwende katika moto wa milele uliotengenezwa kwa Shetani na malaika zake» (shahiri 41).

«Na hawa wote watakwenda kuingia katika azabu ya milele; lakini wenye haki watakwenda kuingia katika uzima wa milele»!

## «Lakini kitu kimoja kinahitajiwa»

Hii ma neno «Lakini kitu kimoja kinahitajiwa» (Luka 10, 42), ndugu wangu, anasema Mwokozi wetu kwa sisi wote. Wa Kristiani mengi wanapenda kusindana wakati ingine ya hii kazi na nyakati ingine ya kazi ingine. Lakini mara mengi hata wale hawajue wanataka ninyi. Kwa sababu Bwana Yesu alijua hiimatendo ya bure ya watu alitwambia kwa sisi wote hii sauti yake: «Lakini kitu kimoja kinahitajiwa».

Hii ni kazi ya kwanza kwa wa Kristiani. Iko kweli ya kama tukona lazima ya ma bintu ingine ya maisha yetu sawa ma nguo, chakula, nyumba na ingine joo vile tunaomba kwa Mungu kila siku «Utupe sisi leo mukate yetu kila siku». Lakini ni kupita lazima wokovu wa milele, kwa sababu bila wokovu ma bintu wengine haina kintu «kwani ni faida gani kama mutu akipata dunia nzima, na kupata hasara ya uzima wake? » (Matayo 16, 26). hakuna kintu kwa mutu moja kama atapotesha wokovu yake.

Faida gani tutakuwa na kama tutapata dunia nzima, lakini tutapotesha uzima yetu? Tunasopoka uzima yetu ya hii dunia kupita mingi ya uzima yetu wa milele. Lakini hii kazi yetu haina nzuri; kwani ni lazima kuonyesha mafa yetu kuliko mingi juu ya ma bintu ya milele.

Kwa kila mtu kazi yake ya kwanza ni namna gani atapata kazi moja juu ya kupata makuta ya maisha yake. Kwa mufano kwa mwamuzi moja kazi yake ni juu ya kuhukumu, kwa mulimanzi ni ya kutumika ma shamba yake, kwa mwenye biashara ni ya kuuza na kuuzisha bintu, kwa muchungaji ni ya kuchunga ma kondoo yake, kwa mwalimu ni ya kufundisha mwanafunzi wake, kwa mwanafunzi ni yakufunda na hivi-hivi. Kwa Mukristu moja kazi ya kupaswa ya kwanza ni namna gani atamufurahi Mungu katika imani na matendo yake, kwani hivi anatumainia kupata ya Huyu uzima wa milele. «Kitu kimoja kinahitajiwa».

Ee Ndugu wangu, tusikuumbwa juu ya hii uzima ya bure, lakini juu ya wa milele; katika neema ya Ubatizo Takatifu tulizaliwa mu uzima ya roho upya; neno ya Mungu ilituita mu uzima wa milele; Kristu, Mwana wa Mungu, alikuja mu dunia, alitesa, alikufa pa Musalaba juu ya kupata

sisi uzima wa milele. Unaona namna gani aliripa Mungu juu ya wokovu wetu? Alifanya matendo yoyote juu ya hii wokovu yetu.

Huyu mumoja alikuja mu dunia juu ya hii kazi. Basi, inapaswa na kwa sisi kuwa paka hii usubuko na matakio; wokovu wetu.

Shetani anakombana kutunyanganya na kutuharabisha wa milele. Basi, sisi aipaswe kulala, lakini kuchunga hazina ya wokovu yetu.

Tunaona, lakini, na tunataabu ya kama wa Kristiani mengi hawaonyeshe mafa juu ya hii tendo ya kwanza. Hawaonyeshe mafa wale wenye wahapende kumufurahi Mungu, lakini kufurahi kwa hii dunia na wanakombana namna gani watafuraha matakio yao ya mwili. .

Hawa wote na wale wanawafanana na matendo wao wanazania ya kama hazina ya wokovu ya milele iko kintu ya bure, kwa sababu wanasahabu ya kama aliteswa Mungu mzima katika lufu pa Musalaba kwa ajili ya saidio na wokovu wetu. Vile, lakini wanazarau, Huyu aliyeteswa na mapenzi Yake na alimazikwa na alifufuka.

Kwa wa Kristiani ya hii wakati kintu ukubwa ni kama wanapokea ma sifu, matukufu, mali na mabintu ya hii dunia. Tendo ya mwisho waliweka kazi ya wokovu yao, lakini Yesu Kristu alituwambia; : «Kitu kimoja kinahitajiwa»; hii inapaswa kuwa kazi yetu ya kwanza.

Musikieni na mweye wenye zambi na  mweye mubarikiwa Wakristiani. Wokovu wa milele iko namna kuipata ao kuipotesha hapa ya hii maisha yetu. Iko lazima kuweka hii sauti ndani kabisa ya akili na roho yetu.

Ee ndugu wangu wa zambi, kumbuka hii malako sisi wote tulipatia ile nyakati ya Ubatizo yetu, na tubu na hivi usitakuwa mukanyanga ya sheria ya Mungu.

Kumbuka saa ya lufu na tubu, kwa sababu haipaswe kutoka ya hii dunia bila kitumaini ya wokovu wako.

Kumbuka Uhukumu wa matata ya Kristu na tubu juu ya usitaonekane pale pamoja na zambi yako.

Kumbuka utamu ya uzima wa milele na uchungu ya lufu wa milele na rudia kwa Mungu na machozi ya toba yako na hivi Mungu atakufungula mulango ya rehema na Ufalme Wake.

«Uturudishe tena, ee Mungu wa majeshi; na uangazishe uso wako, nasi tutaokolewa» ( Zaburi 80, 7).

UTUKUFU KWA  UTATU MUTAKATIFU
MONASTERI YA MUTAKATIFU GRIGORIOS
KILIMA TAKATIFU
GREKIA 1998